Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 29 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:**

Taarifa ya Kwanza ya Mwaka ya Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Mwaka 2003 *(The First Annual Report of the Tanzania Education Authority for the Year 2003).*

Taarifa ya Mwaka ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2001/2002 *(The Annual Report of Activities and Audited Accounts of the Tanzania Commission for Science and Technology for the Year 2001/2002).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 139

**Nyenzo katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro**

**MHE. OSCAR T. MLOKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Morogoro uko katikati ya barabara kuu tatu yaani Dar es Salaam -Morogoro, Dodoma - Morogoro na Iringa- Morogoro, ambapo mara nyingi ajali za barabarani hutokea na kusababisha maafa makubwa kwa watumiaji wake na kwa kuwa Hospitali ya Mkoa inao upungufu mkubwa wa nyenzo za kukabiliana na tatizo la mivunjiko ya viungo:-

Je, isingekuwa vyema kwa Serikali kuiwezesha hospitali hiyo ya Mkoa ili iweze kukabiliana na maafa hayo kama ilivyo kwa Hospitali ya Kibaha inavyosaidia sana kuhudumia watu wanaopatwa na ajali zinazotokea katika Mkoa wa Pwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mji wa Mogororo uko katikati ya barabara kuu tatu za Dar es Salaam - Morogoro, Dodoma-Morogoro na Iringa - Morogoro, ambazo mara nyingi ajali za barabarani hutokea. Aidha, ni nia ya Serikali kuziwezesha hospitali zote pamoja na Vituo vya Afya kukabiliana na maafa yatokanayo na magonjwa ya mlipuko au ajali mbalimbali pale uwezo wa fedha unaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mkoa wa Mogororo imekuwa ikihudumiwa na Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Maafa kukabiliana na matatizo na maafa kwa kutoa misaada mbalimbali. Kupitia Kitengo hicho, Wizara ya Afya imetoa gari moja jipya la wagonjwa *(Ambulance),* aidha, kuna *radio call* nne zinazofanya kazi, moja iko kwenye gari ya wagonjwa, mbili zimefungwa hospitalini na moja iko Ofisini kwa Katibu Tawala wa Mkoa. Vile vile kuna Kompyuta moja kwa ajili ya kutunza kumbukumbu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile Hospitali ya Mkoa wa Morogoro inayo madawa ya kutosha pamoja na vifaa vya tiba tayari kutumiwa wakati wowote yakitokea maafa. Aidha, Wizara ya Afya imeahidi kuipatia madawa na vifaa mbalimbali hospitali ya Mkoa wa Morogoro kupitia Misaada toka *USAID.* Baadhi ya Madaktari na Wauguzi wamehudhuria mafunzo maalum yaliyoandaliwa na Wizara ya Afya , kwa ajili ya kuhudumia watu waliopatwa na maafa. Mafunzo haya yataendelea kufanyika kwa watumishi wengine wa Hospitali hiyo.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali moja ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na upungufu wa nyenzo pia upo uhaba wa Madaktari. Kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Morogoro iko karibu sana na Dar es Salaam ambapo kipo Chuo Kikuu Kishiriki cha Muhimbili chenye utaratibu wa kuwapeleka wanachuo wake katika mafunzo kwa vitendo katika hospitali ya Muhimbili na hospitali zingine mbalimbali. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubali au atakuwa tayari kuchukua ombi langu la kuwasiliana na Uongozi wa Chuo hicho ili Madaktari hao wakati huo ufikapo basi waweze kuletwa na Morogoro ukizingatia kwamba Morogoro na Dar es Salaam ni pua na mdomo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na rai yake lakini kwa kuwa jambo hili liko chini ya Wizara ya Afya basi tutaliwasilisha katika Sekta inayohusika.

Na. 140

**Utalii Maeneo ya Kusini**

**MHE. OMAR M. MWENDA** aliuliza:-

Kwa kuwa shabaha kubwa ya Serikali kupeleka Utalii Kusini imefanikiwa na sasa Watalii wengi wanafika Kilwa na wanapofika wanahitaji kutembelea visiwa vya Songomnara, Sanje ya Kati, Sanje ya Majomo na Songosongo na kwa kuwa hakuna chombo cha uhakika cha kuwavusha, na hivyo hushindwa kutembelea visiwa hivyo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kutokuwa na chombo cha uhakika cha kuwavusha kwenda kutembelea visiwa hivyo kunazorotesha utalii na hivyo kunawakosesha wananchi mapato yatokanayo na biashara ya utalii?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa wakati umefika wa kupeleka boti huko Kilwa ili kukamilisha azma ya Serikali ya kupeleka Utalii Kusini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la msingi lenye sehemu (a) na (b) la Mheshimiwa Omar Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Omar Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, kwa kutambua jitihada za Serikali ya kupiga hatua kubwa katika kufikia lengo lake la kukuza utalii katika Kanda ya Kusini hususan Kilwa Kisiwani, Sanje ya Kati, Sanje Majomo, Songomnara na Songosongo na ninafurahi kusikia kwamba Kilwa sasa inafaidika na ongezeko la Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Omar Mwenda, yana utajiri mkubwa wa historia na ni vivutio vya utalii wa urithi wa utamaduni. Maeneo haya yana masalia ya majengo ya kihistoria ya ustaarabu wa Kiswahili katika kipindi cha karne ya 12 hadi ya 16. Kwa sababu ya umaarufu na umuhimu huo magofu ya Kilwa Kisiwani na Songomnara yaliorodheshwa chini ya Orodha ya Urithi wa Dunia mwaka 1981 chini ya usimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO).*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua tatizo la huduma ya usafiri wa majini wa kutembelea Kilwa Kusini pamoja na Visiwa vingine Wilayani Kilwa. Aidha, tatizo hili pia limeainishwa katika Mpango wa Uhifadhi na Uendelezaji wa maeneo ya kihistoria Wilayani Kilwa, ulioandaliwa na wataalamu wa Wizara kwa

kushirikiana na wataalamu kutoka nchini Ufaransa, hususan Visiwa ya Kilwa Kisiwani na Songomnara. Pamaoja na kwamba Wizara yangu inayo boti *MV. Kale* inayotumiwa na Idara ya Mambo ya Kale huko Kilwa katika kupunguza adha ya usafiri kati ya Kilwa Masoko na Visiwa vingine kama sehemu ya utekelezaji wa mpango huo, suala la ununuzi wa boti mpya na lenye hadhi stahili limezingatiwa. Ni nia ya Wizara yangu kuhakikisha kwamba kabla ya kukamilisha mradi huo suala hili liwe limepata ufumbuzi stahili. Wizara yangu itaendelea kuzungumza na kujadiliana na washirika wa mradi huu ili kuweka mkakati wa kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa Uhifadhi na Uendelezaji wa maeneo ya Kilwa Kisiwani na Songomnara unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kilwa, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO),* Serikali ya Japani na Serikali ya Ufaransa.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali dogo tu la kumuuliza. Kwa kuwa ametambua umuhimu wa Utalii na pia ametambua tatizo lililopo, je, atakuwa tayari kwenda kuviona Visiwa hivyo ili azidi kuthibitisha tatizo lililopo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Omar Mwenda, anaelewa kwamba nilishafika Kilwa Kisiwani na nikaangalia na ndiyo maana baada ya hapo nikafanya utaratibu huu. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Ukanda huo wa Kusini unaotakiwa kuendelezwa kiutalii ni pamoja na Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kutumia mbinu hizo hizo alizofanikisha mafanikio ya Utalii huko Kilwa kuzihamishia katika Mkoa wa Ruvuma ili kukuza Utalii ulioko katika Mkoa wa Ruvuma?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina mipango kamambe *(Master Plan)* ya Utalii ambayo inaangalia Mikoa yote pamoja na Mikoa ambayo Mheshimiwa Jenista Mhagama, ameitaja. Lakini labda niseme kwamba upande wa Kilwa Kisiwani hili ni eneo ambalo limehifadhiwa kwa hiyo, mpangilio wake utakuwa tofauti.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo Wizara imeshatembelea pia Mikoa hiyo ambayo Mheshimiwa Jenista Mhagama ameitaja.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali ndogo la nyongeza. Kwa kuwa katika Visiwa vingi kuna kila maajabu na mojawapo ni Kisiwa cha Ukerewe ambapo Mheshimiwa Spika anatoka, kuna jiwe ambalo likipigiwa muziki linacheza. Sasa Utalii kama huo, je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna haja ya kuweka mkakati maalum tutumie Utalii wa namna hiyo ili tuweze kuendeleza maeneo kama hayo?

**SPIKA:** Jiwe hilo liko katika Kisiwa cha Ukara siyo cha Ukerewe! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa marekebisho hayo ambayo umeyafanya kwa sababu mimi nilishafika huko katika Kisiwa cha Ukerewe. Lakini niseme kwamba tunafurahi tunapopata mawazo kama hayo kwa sababu ni vigumu kwa kweli kwa Wizara kuelewa kila kitu kilichokuwepo. Sasa sina uhakika kama ni muziki wa aina gani ukipigwa jiwe hilo linacheza lakini hata hivyo watu wangu nitawatuma. *(Kicheko)*

Na. 141

**Madhara ya Wanyamapori kwa Wananchi waishio Jirani na Mbuga hizo**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:-

Kwa kuwa Hifadhi ya *Arusha National Park (ANAPA)* iliyoko Arumeru Mashariki imepakana na maeneo ya mashamba na makazi ya wananchi wa Ngurdoto, Sakila, Mareu, King'ori, Luguruki na Olkung'wado:-

(a) Je, ni wananchi wangapi wamepoteza maisha yao kwa kuvamiwa na wanyamapori na ni nani anawajibika kuwafidia?

(b) Je, wakazi wa maeneo yaliyotajwa ambao mazao yao yaliharibiwa na wanyama hao na walishatuma madai yao Serikalini (kama wakazi wa Mareu), watajibiwa lini maombi yao ya fidia na fidia hizo zitatolewa lini?

(c) Je, ni nani mwenye jukumu la kuwalea watoto wanaoachwa yatima kutokana na wazazi wao kuuawa na wanyamapori wanapovamia makazi yao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kipindi cha mwaka 2002 hadi 2004 wananchi 14 walipoteza maisha kwa kuuawa na wanyamapori wakali. Naomba nichukue fursa hii kutoa pole kwa ndugu na jamaa wa Marehemu na Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli wakazi wa maeneo yaliyotajwa mazao yao yaliharibiwa na wanyama wakali hususan nyati na tembo katika kipindi cha mwaka 2002/2003. Wizara yangu kupitia kumbukumbu zilizopo imeona kwamba wananchi wa kijiji cha Sakila waliwasilisha maombi ya kulipwa fidia ya jumla ya shilingi 8,577,000/= kwa Shirika la Hifadhi za Taifa mwezi Julai, 1999. Madai haya ni kulingana na tathmini iliyofanywa na Ofisi ya Kilimo na Mifugo, Wilaya ya Arumeru iliyopo Kikatiti,

ambayo imeonesha kwamba mazao mbalimbali ya migomba, mahindi, maharage na kahawa yenye jumla ya ekari 344 yaliharibiwa. Shirika la Hifadhi za Taifa liliwaelekeza wananchi kufikisha taarifa hizo Wilayani ili zifanyiwe kazi kwa vile janga la ukosefu wa chakula linaweza kushughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Sakila aliwasilisha taarifa hiyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru mwezi Agosti, 1999. Kamati ya Maafa ya Kata ya Kikatiti ilikaa tarehe 18 Aprili, 2000 kujadili suala la njaa kutokana na uharibifu wa mazao uliosababishwa na wanyamapori kwa kijiji cha Sakila. Ofisi ya Kata iliandika barua tarehe hiyo hiyo ya kuomba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya itoe msaada kwa kijiji cha Sakila ili wananchi wake waweze kujikimu maisha yao kutokana janga hilo.

Mheshimiwa Spika, dhana ya kulipa fidia kwa wananchi inayosababishwa na wanyamapori ni nzuri lakini kutokana na mtawanyiko wa maeneo ya wanyamapori na ukubwa wa tatizo la uharibifu wa mazao, suala la fidia kwa wananchi itakuwa ni mzigo na gharama kubwa sana ambayo Serikali itashindwa kumudu.

Hata hivyo, Wizara yangu imekuwa ikitoa kifuta machozi kwa familia ya marehemu baada ya kupokea taarifa stahili kutoka katika Halmashauri za Wilaya husika.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haijaweka utaratibu wa kulea watoto wanaoachwa yatima kutokana na wazazi wao kuuawa na wanyamapori wanapovamia makazi yao. Kama nilivyoeleza kwenye sehemu (b), Wizara yangu imekuwa ikitoa kifuta machozi kwa familia za marehemu baada ya kupata taarifa stahili.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa mpaka hivi sasa kifuta machozi cha aina yoyote hakijalipwa kwa wananchi wa kijiji cha Sakila au Kikatiti, je, Wizara ina mpango gani sasa hivi wa kutekeleza kuwalipa kifuta machozi cha aina yoyote?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nafikiri nilieleza katika jibu langu la msingi jinsi gani ambavyo suala hili lilishughulikiwa, ni kwamba lilishughulikiwa kwa kupeleka taarifa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa sababu mazao yalikuwa yameharibika na kwa maana hiyo kuleta upungufu wa chakula. Sasa labda ningemwelekeza Mheshimiwa Talala Mbise, afuatilie hilo. Lakini kama kuna watu waliouawa na mpaka sasa hivi hawajalipwa kifuta machozi naomba Mheshimiwa Talala Mbise, tuwe pamoja ili kuhakikisha kwamba hili linarekebishwa.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niulize swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini kutokana na hali halisi ya Liwale tayari tulishapeleka orodha ya wananchi wa Liwale ambao waliathirika au kuuawa na simba au wanyama wakali wa aina mbalimbali miaka miwili iliyopita na ilikuwa imeishahakikiwa na Afisa Wanyamapori wa Wilaya kutoka kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Liwale. Hadi hivi

sasa wananchi hao hawajapata kifuta machozi cha aina yoyote. Sasa nini tufanye ili wananchi hao waweze kupata kifuta machozi chao haraka iwezekanavyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, nalielewa. Kwanza tufikiria kwamba maelezo hayo yalikuwa hajaidhinishwa na Afisa Maliasili lakini akatueleza kwamba yameidhinishwa. Mimi mwenyewe binafsi nimeyafuatilia pamoja na Mkuu wa Idara ya Wanyamapori. Napenda kumhakikishia kwamba suala hili tutalimaliza.

Na. 142

**Muungano wa Vyama vya Soka**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

(a) Je, *Taifa Stars* ni Muungano wa nchi mbili au ni Vyama viwili vya Soka vya *ZFA* na *FAT?*

(b) Kutokana na kupatikana kwa uanachama wa soka Zanzibar katika *CAF,* je, kama jina hilo likibakia haitakuwa kuvaa madaraka ya nchi mbili za hapo mwanzo kisoka?

(c) Je, jina hilo kuanzia sasa litakufa au litaendelea kuwepo?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, ningeomba kwanza kuwapongeza vijana wetu wa Simba kwa kuifunga timu ya *Express.* Hii inadhihirisha maneno yangu niliyosema kwamba ukiwa na kocha mahiri utacheza mpira mzuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *Taifa Stars,* si Muungano wa nchi mbili na wala si Vyama vya *FAT* na *ZFA* bali ni timu ya Taifa ya Tanzania. Timu hiyo huundwa na wachezaji wa kutoa Bara na Visiwani ingawa suala la mchezaji kutoka upande upi hutegemea sana mtazamo wa kocha kuhusu wachezaji wanaofaa kuunda timu hiyo. Kwa hiyo, hakuna ushirikiano wa nusu kwa nusu inategemea tu ni vijana gani wanafaa kwa wakati ule.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) jina la *Taifa Stars* litaendelea kutumika katika michezo yote ambayo Tanzania Bara na Visiwani tutawakilishwa na timu moja. Pale ambapo timu za Bara na Visiwani hushiriki kwa uwakilishi wa upande mmoja kama vile *Challenge Cup* majina ya timu husika huitwa

*Kilimanjaro Stars* kwa Tanzania Bara na Timu ya Taifa ya Zanzibar kwa Tanzania Visiwani.

(c) Mheshimiwa Spika, jina la *Taifa Stars* litaendelea kutumika kwa misingi niliyoeleza katika sehemu (b) hadi hapo tutakapoarifiwa vinginevyo.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali ndogo la nyongeza. Kutokana na majibu mazuri ya MheshimiwaWaziri nitauliza kama ifuatavyo:-

Kwa vile kuna manung'uniko na malalamiko katika uteuzi wa wachezaji na makocha wa Timu ya Taifa, je, katika suala hili Mheshimiwa Waziri haoni kuwa ushirikiano huu unaweza ukavunjika kwa sababu viongozi wa *ZFA* wanalalamika sana kuhusu uteuzi wa kocha na wachezaji katika timu ya Taifa?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, suala la uteuzi ni suala la kitalaamu. Ni vyema na sisi Waheshimiwa Wabunge tusishabikie uteuzi unaokwenda kwa misingi ya kisiasa vinginevyo tutakuwa hatufanyi vizuri. Kwa hiyo, mimi naendelea kuwasihi wenzetu wa Zanzibar pale ambapo kama hata ikibidi timu itoke upande mmoja itoke huko, kama hata ikibidi makocha watoke upande mmoja watoke huko ili nchi kama Tanzania tuweze kufanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa jina la Timu ya Taifa hasa ililengwa Timu ya Taifa ya Tanzania Bara na kwa kuwa suala la michezo siyo suala la Muungano, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba Timu ya Taifa ya Tanzania Bara iendelee kuitwa *Taifa Stars* badala ya kuitwa jina lingine hususan kwa sababu baada ya Zanzibar kupata usajili katika *CAF* hivyo waliacha jina kwenye timu ya Taifa ya Tanzania Bara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ulishajibu hilo lakini hebu sisitiza.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunisaidia.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba *Taifa Stars* ni jina la timu ya Tanzania kwa maana ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Timu ya Tanzania Bara inaitwa *Kilimanjaro Stars* na hilo jina ni nzuri. Kwa sababu michezo vile vile ni sehemu ya kunadi raslimali ya utalii tuliyonayo katika nchi hii. Kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Lucas Selelii, tukubaliane kwamba *Kilimanjaro Stars* ni jina zuri linavutia na linaitangaza nchi hii pamoja na maliasili zilizomo.

Na. 143

**Mkopo kwa Ajili ya Akinamama na Vijana**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa muda mrefu sasa imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi vya akinamama na vijana na kwamba mikopo hiyo imekuwa na manufaa makubwa kwa jamii ya Kitanzania:-

(a) Je, Wizara ilitoa fedha kiasi gani (kwa takwimu) kwa vikundi vya akinamama na vijana Wilayani Geita katika miaka ya fedha ya 2002/2003 na 2003/2004?

(b) Je, Wizara inapaswa kisheria kutoa fedha kiasi gani na kwa asilimia ngapi ya Bajeti yake kwa ajili ya mikopo ya vikundi hivyo?

(c) Je, ni hatua gani zinazostahili kuchukuliwa na ni nani anawajibika kuchukua hatua hizo Wizara inaposhindwa kutoa au kutenga fedha kwa ajili ya mikopo hiyo?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mwaka 1993/1994 Serikali ilibuni na kuunda Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa lengo la kuwapatia vijana mikopo yenye masharti nafuu ili kuwajengea uwezo kiuchumi *(Economic Empowerment).* Fedha kwa ajili ya mfuko huo hutolewa na Serikali yaani kwa kupitia Hazina na jukumu la Wizara yangu ni kuratibu na kusimamia uendeshaji wa mfuko huo. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inaratibu na kusimamia mfuko kwa ajili ya vikundi vya Akinamama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanzisha mifuko hii, kila Halmashauri/Miji/Manispaa zimeelekezwa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya mifuko hiyo ya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa napenda kumjibu Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 3,089,756/= kwa ajili ya mikopo kwa vijana katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Aidha, kiasi kama hicho cha fedha kiligawiwa katika kila Halmashauri ya Wilaya/Mjini/Manispaa nchi nzima hivyo kufanya jumla ya fedha zilizotolewa katika kipindi hicho cha mwaka wa fedha kufikia shilingi 370,770,777/=.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004 Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 500,000,000/= kwa ajili ya mfuko huo. Utoaji wa fedha hizo unatarajia kukamilika kulingana na taarifa za hali ya marejesho ya fedha kwa mikopo iliyotolewa kwa mwaka 2002/2003, kwa kila Halmashauri, Miji na Manispaa ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Geita.

Napenda kutumia fursa hii kutoa changamoto kwa Waheshimwia Wabunge kuwahimiza watendaji wa Halmashauri, Miji na Manispaa kusimamia kikamilifu zoezi la urejeshaji wa mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake vilivyopatiwa mikopo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali hutenga fedha kwa ajili ya mfuko wa Maendeleo ya Vijana kulingana na hali halisi ya Pato la Taifa. Hata hivyo nia ya Serikali ni kuona kuwa kiasi cha fedha zinazotolewa kwa ajili ya mfuko huo zinaongezeka kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu kila mwaka.

(c) Mheshimwia Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa inatoa fedha kwa ajili ya mfuko wa vijana kila mwaka, hatua zinazostahili kuchukuliwa ni kila Halmashauri, Miji na Manispaa, kujitahidi kuimarisha mfuko huo kwa kutenga asilimia 10 ya mapato yake, kusimamia utoaji wa mikopo kwa vikundi mbalimbali vya vijana na wanawake na pia kusimamia urejeshaji wa mikopo hiyo kwa wakati, ili vikundi vingi zaidi viendelee kunufaika na mifuko hiyo.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba kiasi cha shilingi milioni tatu kwenye Wilaya yenye vikundi 50 ni sawasawa na kila kikundi kupata shilingi 60 ambazo zitatumika tu kufungua akaunti, kufanya maandalizi ya miradi na wakati wa kufanya mradi wenyewe fedha zinakuwa zimekwisha?

La pili, kama kuna tatizo la upatikanaji wa fedha kwa ajili ya vikundi vya akinamama na vijana, je, Serikali iko tayari kutenga asilimia fulani ya fedha zinazopatikana kutokana na kusamehewa madeni yaani *HIPC* ili ziende moja kwa moja kwenye vikundi hivi ili kusaidia kuondoa umaskini vijijini?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli shilingi milioni tatu kwa Wilaya hazitoshi ndiyo maana katika sera tukasema na Halmashauri zichangie asilimia 10 ya pato lake. Mheshimiwa James Musalika ni Diwani katika Halmashauri yake kwa hiyo, mimi nina hakika kama Halmashauri itaheshimu maagizo haya ya Serikali Kuu fedha zitakuwa zaidi ya shilingi milioni tatu katika mfuko wa vijana na zaidi ya shilingi milioni tatu katika mfuko wa wanawake. Tukichangia nguvu kwa pamoja hapo mimi nina hakika fedha zitakuwa nyingi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, vile vile fedha hizi zinatolewa kutokana na hali halisi ya uchumi wa Pato la Taifa. Tungependa tutoe zaidi kama nilivyoeleza katika

jibu la msingi lakini ukweli unabaki pale pale kwamba unajikuna pale ambapo mkono unafika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwamba kupeleka fedha moja kwa moja kwa vijana kule kama Wizara hatuwezi kwa sababu sisi hatuwajui vijana lazima tupitie kwenye Halmashauri. Katika vikundi 300 vilivyoko Halmashauri ya Geita iangalie ni vikundi gani vinaanza kupewa kipaumbele kwa sababu Halmashauri ndiyo zinawajua vijana hao. Kutegemea sisi huku tupeleke fedha moja kwa moja itakuwa si sahihi.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa utoaji wa fedha hizi kwa vikundi vya wanawake na vijana ni kama unalingana lingana kwa Wilaya zote lakini Wilaya hizo zinatofautiana kwa ukubwa na wingi wa watu, je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa kwamba ni wakati muafaka wa kuweza kugawa hizo fedha kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na wingi wa watu, ukubwa wa Wilaya lakini pia hali ya umaskini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, katika kugawa fedha hizo tulichoangalia sisi ni umaskini. Umaskini uko karibu sawa katika nchi nzima, unaweza ukakuta mahali ambapo kuna watu wachache lakini wana umaskini uliokithiri zaidi kuliko hata mahali ambapo kuna watu wengi.

Kwa kuanzia tukasema kigezo cha umaskini kwamba nchi nzima tuna tatizo la umaskini. Lakini tunapenda kukiri kwamba tumepokea wazo la Mheshimiwa Mbunge, tutalifanyia kazi tendo ambalo tunaweza tukashirikisha sana katika migao ijayo. Lakini itabidi tufanye kwanza utafiti wa kutosha. Wakati tunafanya utafiti zoezi la kugawa hela litaendelea.

**MHE. TEDDY L. KASSELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa fedha hizi zinatolewa kwa mikopo kwa vijana na wanawake bila kujali itikadi na kwa kuwa wengine hawarudishi wakati muafaka, je, Serikali inasemaje kwa hawa ambao hawarudishi kwa wakati muafaka ili wapewe na wengine?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Teddy Kassela-Bantu, kwa kutambua kwamba Serikali inaposukuma maendeleo haijali itikadi. Hiyo ni *observation* nzuri na ndiyo Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi inapaswa ifanye kazi zake hivyo. *(Makofi)*

La pili, ni kwamba ni kweli tunatambua kwamba kuna baadhi ya vijana na wanawake hawarejeshi. Ndiyo maana katika utaratibu huu mpya sisi kama Serikali Kuu itabidi tuwekeane mkataba na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri kuhakikisha kwamba wao wenzetu kule tunawapa jukumu la kuwabana wale wasiorejesha na waweke

mikakati ya kuhakikisha fedha zile zinarudi ili waweze kupewa na wengine. Kwa sababu mfuko huu ni wa mzunguko. Sasa kwa Mheshimiwa Mbunge kutumia Halmashauri ambayo na wewe ni Diwani hebu tusaidie kusukuma huko na kuwabana wale wasiorejesha, mnaweza mkatunga hata *by-laws* pamoja na kwamba mnaweza mkapambana nao kuhakikisha kwamba hawaathiri ukuaji wa mfuko huu.

Na. 144

**Mradi wa Maji**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kwa kuwa upo mradi wa maji wa muda mrefu wenye maji mengi ulionzishwa katika miaka ya 1970 kwa lengo la kupeleka maji katika mji wa Kabila, Wilaya ya Magu pamoja na vijiji vya Kadashi penye chanzo cha Maji, maeneo yote ya Mji wa Nyashana na sehemu linamopita bomba, Kijiji cha Mwabuchuma, baadhi ya maeneo ya Kijiji cha Bugandando, Kijiji cha Nyanghonge, Shule ya Msingi Nyashana na baadhi ya maeneo ya Iseni (Ibindo) na kwa kuwa ujenzi wa barabara ya Bukwimba - Bugandando umesababisha baadhi ya mabomba kukatwa na hakuna fidia yoyote iliyotolewa na baadhi ya mabomba yaliibiwa na kwa kuwa Serikali katika mradi huo imejielekeza katika kurekebisha, kufufua na kuviimarisha vyanzo vyote vya maji kwa kushirikiana na wananchi na kwa kuwa mtandao wa mabomba kwa sasa sio mzuri kwa baadhi ya maeneo hasa eneo la Wilaya ya Magu na Kabila ambako kuna tanki:-

(a) Je, Serikali kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo niliyotaja ina utaratibu gani wa kufufua mradi huo ili ufanye kazi kikamilifu kuliko hivi sasa ambapo unahudumia eneo dogo hasa ikizingatiwa kuwa Halmashauri zetu hivi sasa hazina uwezo mkubwa kifedha?

(b) Kwa kuwa mtambo uliopo sasa umechakaa na unahitaji matengenezo makubwa, je, Serikali iko tayari kusaidia upatikanaji wa mtambo mpya na mabomba mapya ili wananchi wa maeneo ya Maligisu, Kadashi, Mwabuchuma na Nyashana waweze kupata maji kama hapo awali?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Kadashi ulijengwa na kuanza kutoa huduma mwaka wa fedha 1972/1973 kwa lengo la kuhudumia vijiji vitatu vya Kadashi, Nyashana na Mwashwengele, Wilayani Kwimba na Mji Mdogo wa Kabila katika Wilaya ya Magu. Huduma ya maji katika vijiji vya Nyashana na Mwashwengele ilisitishwa mwaka 1992 kutokana na sehemu ya bomba kuu la kusambaza maji katika vijiji hivyo kukatwa na baadhi ya mabomba kuibiwa. Bomba hilo lilikatwa wakati wa matengenezo ya barabara

ya Bukwimba-Bugandando mwaka 1992 na tangu wakati huo ukiondoa Kijiji cha Kadashi vijiji vingine havipati huduma ya maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(Health Through Sanitation and Water - HESAWA)* uliotekelezwa kwa msaada wa Serikali ya Sweden, wananchi wa maeneo ya Nyashana, Bugandando, Mwashwengele, Kadashi, Maligisu, Mwabuchuma na Ibindo walishiriki kikamilifu kwa kuchimba visima vifupi 51 kwenye maeneo yao. Uchimbaji wa visima hivyo vifupi umesaidia sana huduma ya maji kuendelea kupatikana katika vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, sera ya maji inasisitiza ushirikishwaji wa wananchi katika kubuni, kujenga na kuhudumia miradi yao ya maji vijijini. Ufufuaji wa mradi wa Kadashi utatekelezwa chini ya utaratibu huo ambao utahakikisha wananchi wanaumiliki mradi wao na kushiriki wakati wa ukarabati ili uweze kutoa huduma endelevu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge aendeleze ushirikiano wake na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kama anavyofanya hivi sasa, ili wananchi wa maeneo haya wahamasishwe na kuomba ukarabati wa mradi huu uingizwe kwenye Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini utakayoanza kutekelezwa Wilayani kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005. Programu hiyo inatekelezwa kwa utaratibu wa wananchi wenyewe kuchagua miradi yao kulingana na kipaumbele walichojiwekea. Ni imani yangu kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba itaweka kipaumbele chake kwenye mradi wa Kadashi ili utekelezwe chini ya programu hiyo.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na maelezo mazuri kabisa ya Mheshimwa Naibu Waziri, sababu kinachozungumziwa hapa ni kwamba uwezo wa Halmashauri zetu sasa hivi ni mdogo na Serikali yetu kupitia Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo inasimamia na kuvikarabati visima, malambo na kadhalika, je, sasa kwa sababu uwezo wa Halmashauri yetu hii ya Kwimba ni mdogo haiwezi kupata fedha hizo za kuweza kununua mtambo mpya, Serikali inaweza kutusaidia kununua mtambo mpya?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa jibu katika kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Wilaya ya Kwimba ni mojawapo ya Wilaya ambazo ziko kwenye mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Kwa hiyo, ombi langu napenda nirudie kwamba wauingize mradi huo wa maji wa Kadashi katika programu hiyo kwa sababu chini ya mradi huu wa Benki ya Dunia wananchi na uongozi husika wanachagua ni mradi upi ambao wanataka waanze nao. Nina hakika kulingana na fedha zilizopo kwa ajili ya kila Wilaya tulizozitamka kwenye mradi huo, fedha zitatosha kabisa kuhudumia mradi huo na miradi mingine ambayo itaondoa kwa kiwango kikubwa matatizo ya maji. Naomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na kuhakikisha kwamba mradi umeingizwa katika programu hiyo. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa suala la maji ni tatizo katika sehemu nyingi nchini likiwemo jimbo la Kigamboni. Kwangu kuna visima vingi vimechimbwa lakini katika visima hivyo mashine zilizowekwa kwa ajili ya kuvuta maji zimekuwa hazifanyi kazi zaidi ya mwezi. Waziri anaweza kutuambia ni kwa sababu gani mashine hizo zinatumika na kwa nini wasibadilishe utaratibu wa mashine hizo?

**SPIKA:** Eeeh, hilo ni swali jipya.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo kuhusu mradi wa Kadashi.

Kwa kuwa huu mradi mimi naufahamu na nilikuwa nautembelea mara kwa mara. Kwa kweli tatizo la mtambo wa maji ni kubwa Kadashi kama vile ambavyo tatizo liko Mkalama na Igonia, je, Waziri atayachukua yote kwa pamoja haya na kwa sababu Wilaya zote ziko kwenye mpango wa Benki ya Dunia na wananchi wa Mkalama wasaidiwe? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Aaahh, na hilo nalo kwa kweli ni swali jipya. Hayo mapya yaletwe kwa taratibu za kawaida.

Na. 145

**Kulipia Huduma za Maji**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taifa limepania kujikwamua kutoka katika dimbwi la umaskini kwenye sekta zote ikiwemo sekta ya maji na upatikanaji wake kwa kufufua na kuanzisha miradi mipya ya maji kwa ushirikiano wa Serikali na wadau mbalimbali mijini na vijijini na kwa kuwa miradi hiyo inapaswa kuwa endelevu kwa walengwa kuwajibika kulipia huduma za maji:-

Je, ni mikakati au mbinu gani zitatumika ili kuwabaini na kuwasaidia wananchi wasio na uwezo wa kulipia huduma hizo za maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Sera ya Maji ya mwaka 2002 inatambua umuhimu wa kuwapatia maji wananchi wenye kipato kidogo mijini na vijijini. Kifungu Na. 4.4 kinasomeka kama ifuatavyo, nanukuu: "Lengo ni kuwa na huduma ya Majisafi na Majitaka katika maeneo yenye

wakazi wenye kipato kidogo na maeneo yasiyopimwa pembezoni mwa miji." Kwa upande wa Maji Vijijini, kifungu Na. 4.9 kinasomeka kama ifuatavyo na nanukuu: "Lengo ni kuwa na huduma endelevu inayokidhi mahitaji ya makundi mbalimbali ya watumiaji maji."

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza sera hiyo, Wizara yangu kupitia Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini na Taasisi nyingine zinazotoa huduma za maji, inahakikisha kwamba suala la kuwapatia maji wananchi wenye kipato kidogo ambao hawawezi kumudu gharama halisi za huduma ya maji linazingatiwa katika kupanga bei za maji.

Ili kutekeleza azma hiyo, mwaka 2003 Wizara yangu ilitoa agizo la kuzitaka Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini kufanya zoezi la mara kwa mara la kuwatambua wasio na uwezo kabisa wa kulipia huduma ya maji. Ili kuwatambua na kuainisha vyema wananchi wasiokuwa na uwezo wa kulipia maji, Serikali huwashirikisha viongozi mbalimbali katika ngazi za Mitaa, Kata na Wilaya. Vigezo vinavyotumika ni kuangalia hali ya kipato, ulemavu, umri na magonjwa kama vile UKIMWI na Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini kwa maelekezo ya Wizara yangu zinaendelea na zoezi la kuwatambua wananchi wasiojiweza mijini. Hadi sasa jumla ya Kaya 421 zimetambuliwa kama ifuatavyo:-

Mamlaka ya Tabora Kaya 84, Tanga 47, Morogoro 216, Arusha 31, Mtwara 19 na Moshi 24 ambapo kaya hizi sasa zinapatiwa kiasi cha ndoo tano hadi nane kwa siku chini ya utaratibu huu.

Vile vile Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini zimejenga vituo vya kuchotea maji kwa gharama nafuu ya shilingi 2 hadi 5 kwa ndoo ya lita 20, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 20 hadi 100 inayotozwa na watu binafsi wanapouza maji *(Water Vendors).* Jumla ya vituo 923 vimejengwa katika mamlaka mbalimbali nchini kote hadi sasa.

Kwa upande wa Maji Vijijini, huduma ya maji kwa wasiokuwa na uwezo hutolewa kulingana na utaratibu unaowekwa na Serikali ya Kijiji kwa kushirikiana na Kamati za Maji. Serikali itaendelea kuvishauri vijiji na Kamati za maji ili kuhakikisha kwamba wananchi wasiokuwa na uwezo wanapewa huduma hiyo bila ubaguzi wowote.

Na. 146

**Masharti ya Wafadhili Kwa Misaada**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha alipokuwa akitoa maelezo mbele ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi mwezi Machi, 2004 alisema kuwa kuna kukwama kidogo na kwamba mipango yetu haiendi vizuri jinsi tulivyotaka kwa sababu

baadhi ya wafadhili wamekataa kutoa misaada yao kwa sababu ya kutokubaliana na masharti yao ambayo ni magumu kiutekelezaji Kitaifa na kwamba kama tukikubaliana na misaada hiyo ndani ya masharti waliyoweka ni dhahiri kwamba Taifa letu litadhalilika:-

(a) Je, makubaliano ya awali na hao wafadhili hayakuwa na masharti na kama yalikuwepo, ni masharti yapi hayo na kati ya hayo ni yapi tumeyakataa na ni kwa sababu zipi?

(b) Kama masharti yote yalikuwepo na tuliwekeana saini katika mkataba halafu wakaleta masharti mengine nje ya mkataba wa makubaliano, je, huko si kuvunja mkataba, jambo ambalo ni kosa kisheria na linaloweza kupatiwa ufumbuzi kisheria?

(c) Je, ni madeni kiasi gani tunayodaiwa sasa, ni nchi ngapi zimetufutia madeni, ni zipi hazijaamua kutufutia madeni hayo na ni nchi zipi zimegoma kutoa misaada au mikopo nafuu waliyoahidi kwa sababu ya kutokubaliana na masharti yao na ni kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDILSALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, misaada yote inayotolewa na wafadhili hutolewa chini ya makubaliano maalum kwa njia ya kutiliana sahihi mkataba kati ya Serikali na Mfadhili husika kuhusu miradi au programu maalum za kutekelezwa, ufadhili utakavyokuwa na namna utakavyosimamiwa na pande zote mbili yaani mfadhili na Serikali.

Kutokana na makubaliano hayo, mara nyingi kunakuwa na vigezo vinavyokubaliwa na pande zote mbili kwa lengo la kuweza kufikia malengo yaliyotarajiwa. Hivyo, kukataa masharti hayo baada ya kuwekeana sahihi mikataba husika ni kukiuka maelewano ya mkataba huo.

Hata hivyo, kwa tahadhari, mikataba mingi hutoa utaratibu wa kufanya mabadiliko ya makubaliano ya awali endapo mazingira ya mkataba kama ulivyokubalika yatabadilika na kuonekana vigumu kutekeleza makubaliano. Wakati wote Serikali huwa huru kukubali au kukataa masharti yoyote ya ufadhili.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza miradi kwa misingi ya makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na wafadhili, uwezekano wa vigezo tulivyokubaliana kutotekelezwa kwa wakati uliotegemewa hujitokeza. Jambo hili huweza kusababisha ucheleweshaji wa kupokea fedha za mfadhili na hata kuzikosa endapo vigezo hivyo vitachelewa au kushindikana kutekelezwa hadi muda wa mkataba kuisha.

(c) Mheshimiwa Spika, deni la nje hadi mwishoni mwa Mei, 2004 lilifikia shiligi bilioni 8,858.6 sawa na dola za Kimarekani milioni 7,934.3. Hadi sasa Serikali imepata

msamaha wa madeni kutoka nchi 12 kati ya 13 za Kundi la Paris. Nchi hizo ni Austria, Ubelgiji, Uholanzi, Ufaransa, Urusi, Ujerumani, Canada, Uingereza, Norway, Italia, Marekani na Japan. Brazil ndiyo nchi pekee ambayo bado hatujafikia makubaliano nayo katika kundi hili.

Aidha, Serikali imesamehewa madeni ya Kiserikali *(Sovereign Debts)* toka nchi zisizokuwa za kundi la Paris *(Non Paris Club)* ambazo ni India, Bulgaria na China. Iran imekubali kimsingi kuahirisha muda wa malipo ya deni kwa miaka 40.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa hiyo miradi haikuweza kufanikiwa ndiyo ambayo ilikuwa ipewe hiyo misaada, je, ni miradi ipi ambayo haikufanikiwa? Nafikiri imeeleweka?

Swali la pili, je ni nani anayetathmini mradi mbaya au mzuri na kama ipo ni vipi miradi mibaya kama *IPTL* ilipitishwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDILSALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, swali lako la mwanzo ni swali jipya kabisa. Miradi hii haikufanikiwa, labda ulilete kwa njia ya utaratibu unaokubalika ili tuweze kukujibu ni vipi imefanikiwa.

Lakini ile miradi ambayo haifanikiwi ambayo sikuitaja kwa sababu fulani lakini anayetathmini ni pande zote mbili. Kwanza kwa sisi kama ni nchi ama Serikali tunatazama maslahi ya mradi wenyewe. Kabla haujafika mbali basi tunaweza kusema kwamba mradi huu hautuafiki wala hautoleta vifaa na tija kwa nchi.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kuna mikataba mingine ambayo masharti yake yanawaumiza wananchi hii inatokea vipi Serikali inakuwa haipo au inakuwa haina uwezo wa kufanya majadiliano

**SPIKA:** Kwa mfano mikataba gani?

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Kwa mfano Mkataba wa Uzalishaji wa Umeme wa *IPTL*. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mikataba yote ambayo inatekelezwa katika nchi yetu ni kwa maslahi ya Taifa letu. Hakuna mkataba ambao Serikali inaweka sahihi eti labda kwa sababu ya shinikizo fulani.

Kuhusu Mkataba wa *IPTL* kama tulivyokwishaeleza mara nyingi hapa. Mkataba huo au mtambo huo ulikuja wakati ule tulipokuwa na matatizo makubwa sana ya umeme na ndivyo *PPA* zote duniani zinavyofanya kazi. Kama leo tusingekuwa na *IPTL* hivi leo tunatumia mradi wa *IPTL*. Kama tusingekuwa nao kwa vyovyote viwanda vingi sana vingefungwa.

Kwa hiyo, kila jambo lina gharama zake, hakuna jambo ambalo unalipata bure. Lakini si kwamba mkataba huo labda Serikali haukuuona, tuliuona lakini ilikuwa ni mkataba ambao lazima tuuingie kwa sababu tulikuwa na matatizo makubwa ya umeme na hata sasa umeme huo umetusaidia sana mwaka huu ambapo mpaka sasa tunavyofahamu bwawa la Mtera bado halijaanza kufanya kazi. Tungekuwa tumeumia sana kiuchumi kama sio kuwa na umeme kutoka mtambo wa *IPTL*. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABOUD MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza suala moja la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa Mataifa mengi yamesamehe madeni kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, je, Zanzibar imepata msamaha kwenye eneo hilo na kama imepata ni kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, Zanzibar pia imeingia kwenye Mpango wa *HIPC* kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilivyoingia mpango wa *HIPC*. Kwa hiyo, kuna mpango maalum uliotengenezwa wa *Poverty Strategy Paper* yao na kutokana na hiyo ndiyo misaada yote itapitia upande huu. Kwa hiyo, ile ambayo imefanywa kwa *HIPC* kwa mujibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni tofauti na ile ambayo itafaidika Zanzibar kwa mpango kama huo. Lakini ukiniuliza kiasi gani siwezi kujibu nafikiri jawabu litakuwepo kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar watajua ni kiasi gani wamepata fedha hizo kwa *HIPC* waliyoitengeneza kwa msaada huo kwa *World Bank*. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kinachosamehewa kama nchi ikitusamehe deni inasamehe deni hakuna kipande cha lile deni ambalo inadaiwa Zanzibar, ni deni la Jamhuri, likisamehewa kwa hiyo, kila mmoja katika Jamhuri ameingia katika msamaha huo. *(Makofi)*

Na. 147

**Ukusanyaji wa Mapato**

**MHE. FRANK G. MAGHOBA (k.n.y. MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA)** aliuliza: -

Kwa kuwa suala la ushuru na ukusanyaji wa mapato na misaada ya nje ni mambo ya Muungano: -

(a) Je, Idara ya *TRA* imekusanya mapato kiasi gani kwa upande wa Tanzania Zanzibar katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2003?

(b) Je, katika fedha hizo, gawio la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kiasi gani kwa kipindi hicho nilichotaja?

(c) Je, katika miaka hiyo mitatu, Tanzania imepata misaada kiasi gani na katika hiyo fungu la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lilikuwa wapi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA ( MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, naomba kutoa maelezo yafuatayo: -

Kodi zinazosimamiwa na kukusanywa na *TRA* kule Zanzibar ni zile za Muungano tu. Kodi za Muungano zimetajwa katika aya ya 10 ya nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Kodi hizo ni kodi ya mapato, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa. Aidha, kutokana na jukumu lake la kudhibiti uingizaji wa bidhaa nchini, *TRA* hukusanya pia Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT).*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kugawana mapato yanayotokana na kodi za Muungano baina ya Serikali zetu mbili ni ule uliopendekezwa na Tume ya Mheshimiwa William Shellukindo, nao ni wa kufuata kanuni ya mahali mapato husika yanapokusanywa *(derivation principle).* Kwa utaratibu huu, mapato yote yanayokusanywa upande wa Tanzania Bara yanatumiwa na Serikali ya Muungano, wakati yale yanayokusanywa upande wa Tanzania Visiwani, yanatumiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gondo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2003 *TRA* ilikusanya jumla ya shilingi milioni 66,664.6 kwa upande wa Tanzania Bara.

(b) Mheshimiwa Spika, mapato yote yanayokusanywa na *TRA* kwa upande wa Tanzania Zanzibar hutumiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hivyo, kiasi hicho sha shilingi milioni 66,664.6 kilitumiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2000 hadi 2003 Tanzania ilipata misaada yenye jumla ya shilingi milioni 572,100.0 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipata mgao wa kiasi cha shilingi milioni 30,598.0. Mgawanyo huo ulizingatia mapendekezo ya Tume ya Mheshimiwa William Shellukindo kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ipate asilimia 4.5 ya misaada yote tunayopata kwa mwaka.

**MHE. ISSA MOHAMED SALIM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba Sheria ya Kodi ya Forodha ya bidhaa zinazoingia kutoka nje ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani ni moja, je, kwa nini mizigo inayoingizwa Zanzibar ikija Tanzania Bara inatozwa kodi upya. Imekuwa kodi ya Zanzibar haikubaliki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, mizigo inayotoka Zanzibar kama itakuwa imechekiwa kwamba kuna wasi wasi kodi iliyotozwa haikukamilika ni ile ni kodi ya juu ambayo haikulipwa ndiyo analipishwa mfanyabiashara. Mara nyingi hayo yametokea kwamba biashara iliyoleta *load declare* katika *container* wakati mwingine ame-*under declare* na inapochekiwa kufanya *double check* inapatikana kuwa kuna ushuru ambao haukulipwa kama inavyotakikana na ndio pale tu mizigo hiyo inapotozwa kodi lakini sio kwamba analipa kila kitu. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Zanzibar ni kisiwa na kisiwa kinategemewa sehemu nyingine kufanya biashara nazo, je, Waziri haoni kwamba Zanzibar kama itakuwa kodi iko sawa sawa na Bara watashindwa kufanya biashara yoyote na hali ya maisha ya wafanyabiashara wetu itaanguka zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, Zanzibar kweli ni kisiwa, lakini kama ni biashara ambayo itafanyika kiulimwengu, Kimataifa bila shaka kodi lazima zitakuwa hazilingani na kama utakuwa umelipa kodi kasoro na biashara ile ile unataka uipeleke Tanzania Bara na wafanyabiashara vile vile wa Tanzania Bara hatukubali kwamba hao wanatozwa kodi zaidi na kuwa na *margin* yao ya *profit* ikawa ni ndogo na wale ambao wanatoka sehemu nyingine kwa upendeleo maalum kwamba tu iwe hivyo. Lakini kama kwa mfano *VAT Sale Tax* si ya Muungano ni ya Zanzibar peke yake. Kwa hiyo, *VAT* inaweza ikasimamiwa Zanzibar na wakalipa kwa mujibu wa *VAT* ya kule na wakawauzia wananchi ili waweze kunufaika kwa bei ndogo ya bidhaa kwa sababu *VAT* yao ni ndogo zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibiwa. Leo yalikuwa maswali 9 badala ya 10 kwa sababu mwenye swali Na. 10 aliliondoa ndiyo yamekwisha kabla ya wakati wake.

Kuna tangazo moja la kikao linatoka kwa Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake *(TWPG).*

Mheshimiwa Anne Makinda, anawaomba Wabunge wote Wanawake wakutane leo tarehe 29 Juni, 2004 kuanzia saa 7.00 mchana baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge katika chumba Na. 231 ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Kanuni za Bunge kifungu namba 55(3) naomba kupata mwongozo wako.

**SPIKA:** Mmh.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, Wote sisi Wabunge hapa ni mashuhuda kwamba wewe mwenyewe binafsi unatujua Wote tuliomo humu ndani kwa majina yetu, Majimbo yetu, Vyama vyetu na tunakotoka na nakumbuka katika kipindi cha mwaka 1995 mpaka mwaka 2000 tuliambiwa hapa Bungeni kwamba Waandishi wa Habari wanaokuja kuandika taarifa zetu ni wale ambao wamepata taaluma ya uandishi, wenye kujua wajibu wao na wenye kujua majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha ni kwamba mwandishi aliyebobea wa Gazeti la Mwananchi la Jumapili, tarehe 27 Juni, 2004 ameniandika mimi. Maelezo yangu kwa kweli sina utata nayo, lakini inasikitisha, inaonyesha hata jiografia ya Tanzania haielewi. Jimbo la Koani kwanza amesema ni Pemba, Chama changu ni *CUF*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kupata mwongozo wako. Mwandishi wa Habari kama huyu kweli anajua kazi yake? Kama haelewi Chama changu ni kipi, hata Katibu wa Bunge angeshindwa kumwuliza au hata mimi mwenyewe anashindwa kuniuliza?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu ningeomba ...

**WABUNGE FULANI:** Ni Spika.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, samahani. Unajua kwa nini nakosea kila wakati, tangu nilipoona taarifa ile lita mbili za damu katika mwili wangu zimepungua kwa sababu maisha sitokuwa mwanachama wa *CUF,* mimi nasema. Napenda kupata mwongozo wako. Ahsanteni. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Wote tumesikia tatizo la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, sasa mwongozo wa jumla ni kwamba, Waandishi wa Habari wanawajibika kuandika Habari za Bunge kwa usahihi kabisa na inapotokea kosa la wazi kama hilo lililompata Mheshimiwa Haroub Said Masoud, dawa yake ni kulipeleka kwenye Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili huyo mwandishi aitwe aweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2004**
***(The Finance Bill, 2004)***

*(Kusema Mara ya Kwanza)*

*(Muswada wa Sheria ya Ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wa Sheria ya Fedha *(The Finance Bill)* umesomwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, sasa utapelekwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ili uweze kushughulikiwa kwa taratibu za kawaida.

Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005**
**Wizara ya Kilimo na Chakula**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pole nyingi kwa familia ya Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye alitutoka si muda mrefu hapa Dodoma. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja nianze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Charles Keenja, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala na wataalam wote wa kilimo. Kwa kweli kama kawaida wameandika vizuri hotuba ambayo inaeleweka vizuri, lakini kwa kuwa Wizara hii kwa kweli imerushiwa madongo mengi yaani lawama nyingi zimekwenda kwao, ningependa nijikite kwenye ushauri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Kilimo na Chakula ni Wizara ambayo ndiyo tunaiangalia wote. Ni Wizara ambayo ndiyo inatufanya tuwepo kwa sababu Kilimo na Chakula ndiyo uhai. Kwa hiyo, nianze kwa kuchangia sehemu ya bei za pembejeo.

Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia habari ya bei za pembejeo. Mimi natoka kwenye Wilaya ambayo iko katika moja ya Mikoa ambayo imepewa ruzuku ya Serikali. Tunashukuru sana kwa mipango hiyo. Wilaya ya Kilolo siku zote nimekuwa nikisema kwamba ni Wilaya ambayo inafaa kwa kilimo, ni Wilaya ambayo inaweza kuwa ni Wilaya mkombozi kwa chakula, lakini bei za pembejeo zimetukatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamekata tamaa kabisa na kilimo. Nina hakika kabisa pamoja na mpango mzuri wa Serikali, lakini bado tulikuwa hatujajitayarisha kwa jambo hili, laiti kama tungejitayarisha vizuri, nafikiri mipango ingekuwa mizuri. Mafanikio ya kilimo siyo wingi wa miradi inayoendeshwa kiofisi, bali ni wingi wa ubora

wa mazao yanayotokana na kilimo. Nikisema hivi nina maana kwamba program zipo, lakini kwa kiwango kikubwa zinaishia ofisini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo kuhusu watu wa mipango. Mipango ya kilimo imekuwa ni mizuri lakini utekelezaji wake umekuwa na matatizo. Ukienda nchi zinazotuzunguka mipango mingi ambayo inaendeshwa katika nchi hizo inatoka Tanzania, lakini cha ajabu sasa sisi tumekuwa wazuri tu kuandika miradi lakini utekelezaji wake umekuwa una matatizo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji umekuwa na matatizo sana na nitatoa mfano mmoja kwamba kule kwetu Iringa nikizungumza Kihehe, Mgogo ananielewa na Mgogo akizungumza Kigogo, Mhehe anamuelewa, lakini tatizo linakuwa pale ambapo Mhehe anataka kuzungumza Kigogo, Mgogo hamuelewi na Mgogo anapozungumza Kihehe, Mhehe hamuelewi.

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni kwamba, sisi katika utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, wataalam wakizungumza kitaalam sisi Wanasiasa tunawaelewa na Wanasiasa tukizungumza kisiasa, Wataalam wanatuelewaa. Lakini pale sisi Wanasiasa tunapogeuka kuwa Wataalam inakuwa tatizo kwa wataalam kutuelewa. Pia, Wataalam wanapotaka kutoa majibu ya kisiasa sisi Wanasiasa hatuwaelewi, kwa hiyo, ni tatizo. Sasa, sisi tufanye kazi yetu ya siasa na kwenye kilimo Wataalam wafanye kazi yao ya kitaalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema wazi kabisa kwamba kilimo ndicho ambacho kinaweza kutukomboa, lakini mpaka leo hatujajua wapi tuanzie. Tuna mabonde mazuri ya umwagiliaji lakini je, ni bonde gani ambalo tumeamua tukaelekeza nguvu zetu pale kwenda kufanyia kazi? Hakuna, tunagusagusa tu!

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya ya Kilolo kwa mfano, kuna mabonde mazuri kule Nyanzwa. Nashukuru safari hii Mheshimiwa Waziri amenipa pesa na mwaka 2003 amenipa pesa, lakini zile pesa ni ndogo ndogo. Ule mradi ulikuwa uishe siku nyingi, lakini kila mwaka tunapewa kidogo kidogo sana mradi hauishi. Tuache kuchanganya maendeleo na siasa kwamba nisipopeleka pesa kidogo pale kwa Mwamoto atachukia. Peleka sehemu moja, elekeza nguvu sehemu moja tumalize watu waone mfano sehemu mojawapo. Lakini ukitaka tupeleke kidogo Hanang', kidogo Mbulu, kidogo Iringa, kidogo Kilolo, kidogo Sumve, hatutafika, *impact* haitaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia habari ya benki. Nataka niseme wazi kabisa kwamba, nina hakika pamoja na nia nzuri ya Serikali, lakini ile Benki ya Kilimo ya kusaidia Wananchi, ambayo tunategemea kuianzisha haitaanza na kama ikianza kwa sasa hivi haiwezi kufanikiwa kwa sababu tayari itakuwa sehemu moja tu. Nafikiri itakuwa ni sehemu moja kwa sababu *infrastructure* inatakiwa, tutatumia pesa kiasi gani? Nafikiri badala ya kupoteza nguvu hizo kwenye benki ambayo tunafikiria kuianzisha, tuchukue hata Posta tu ambayo iko nchi nzima tuiimarishe ile iwasaidie Wananchi tuache ndoto, au *CRDB* au *NMB* pamoja na kuwa iko mahututi, inaishi kwa matumaini, lakini tukiiamsha kwa njia hiyo basi itaamka tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho kinatukwamisha ni mipango iliyokosa takwimu na pia watu wa utabiri wa hali ya hewa. Tuna mipango mizuri kabisa, lakini takwimu za uhakika hakuna! Njaa isingetokea maana watu wa utabiri wa hali ya hewa wao walikuwa wanajua kabisa litakalotokea kesho, tungekuwa tumeshajiandaa na chakula kingekuwepo. Nafikiri ushirikiano bado siyo mzuri kati ya watu wa mipango, takwimu na hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, leo tunapata njaa, tunakwenda kununua chakula Ethiopia na Kenya, inasikitisha. Sisi tuna maji ambayo kwa kweli ni mengi, maji ambayo tungeyatumia kwenye kilimo cha umwagiliaji ambacho ni kilimo cha uhakika, tusingekuwa hapa tulipo. Tuna Maziwa, Mito, leo hii tunasema Watanzania tunakufa kwa ajili ya kukosa maji, ni kitu cha ajabu, hatueleweki!

Mheshimiwa Spika, sisi hatujaanza kuchimba maji chini, bado tunatumia maji tu yaliyoko juu. Sasa hivi wenzetu wa Misri kwa sababu ya mipango yao mizuri wanaanza ku-*reserve* maji, maana maji sasa hivi duniani kwa taarifa ambazo zipo yanazidi kupungua. Kama maji yanazidi kupungua wameshaanza kuweka mipango ya kutunza maji kwa miaka 500 ijayo, lakini sisi bado hatujui hata tufanyeje. Lakini inawezekana mipango hiyo mizuri imeandikwa hapa Tanzania. Sisi tuna tatizo gani?

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, kitu kikubwa alichofanya ni kwamba aliweka nguvu na mkazo kwenye kilimo. Binafsi nasema hakuna wasomi wazuri kama watu wa kilimo, huko ndiko walikojikita wasomi. Napenda nimsifu yule mama anayeshughulikia Mfuko wa Pembejeo. Yule mama amefanya kazi kubwa sana, lakini wanamkwamisha kwa sababu ya masharti. Masharti yaliyopo pale hayakulenga wakulima, masharti yale yamelenga sisi tunaokaa Mjini, siyo wale wakulima haswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kweli tuko *serious,* basi tuelekeze nguvu zetu Vijijini ili Mheshimiwa Charles Keenja afanye kazi yake kwa uhakika. Tuna mazao ambayo tayari yameshaanza kuonyesha kweli ni mazao ambayo yanaweza kutusaidia. Kuna zao la *Paprika,* mimi nimelipigia pipa sana, siyo debe. Kuna zao la Mlonje, Vanilla, sikuona kama limezungumzwa. Kwa hiyo, nafikiri twende tuwasaidie wananchi kuwa wabunifu pamoja na mambo mengine yatakayomsaidia mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaingia kwenye utandawazi, athari za utandawazi jamani ni mbaya sana. Sisi Tanzania tusipoangalia tutageuzwa kuwa jalala la watu wengine kama mpaka leo hii tunaendelea kulima kwa jembe la mkono halafu tunasema kilimo kipo, tunashangaza dunia! Tunashangaza ulimwengu kwamba sisi tunataka ku-*export* mazao ambayo unalima kwa mkono, kwa ubora gani? Huwezi kulima kwa mkono zao likawa bora hata kidogo, itakuwa ni kujidanganya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimwambie Mheshimiwa Charles Keenja, kwamba wale watu ambao wameonyesha nia ya kuendeleza kilimo kwa njia za matrekta na mashine wasaidiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze suala la Wataalam. Wataalam walioko huko vijijini kwetu wanayumba maana hawajui wako Wizara gani na hawajui nani ndiyo bosi wao, matokeo yake wao wenyewe wanakaa Mjini. Sasa watakaaje Mjini wakasimamia kilimo? Wao wanatakiwa wawe mfano, kama ni sera basi itungwe sera kwamba wakae Vijijini na wawe mfano bora kwa wale wanaowasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa wa 23 kuna zile fedha za *PADEP,* kwa kweli nitaomba ufafanuzi kuhusu matumizi yake. Sidhani kama yametumika kama inavyotakiwa kwa sababu kilimo ninakwenda sambamba kabisa na wenzetu hao wa UKIMWI. Wakati semina, kongamano na warsha zinaendelea, wananchi wanaendelea kufa kule majumbani kwa UKIMWI, hatujaanza kuwaangalia.

Sasa wakati kilimo kinaendelea kufa, bado semina zinaendelea, bado kongamano, bado sijui mikakati, bado tuko mbioni na kadhalika. Nafikiri hatutafika, tupunguze siasa na matumizi mabaya ya fedha. Huko Vijijini sasa hivi hakuna hata pikipiki, magari wala baiskeli za kufika kule kwa walengwa. Magari yote yako Dar es Salaam. Kwa hiyo, nafikiri itakuwa ni vema sasa tukajibadili tukaenda na kilimo ambacho kinatakiwa kama kweli tuko *serious,* lakini kama hatuko *serious,* tuache, tutaendelea kufa na njaa.

Mheshimiwa Spika, kuna Mikoa ile ambayo ilipendelewa ikapewa ruzuku maana ina mvua nyingi. Sehemu zenye mvua nyingi maana yake miundombinu yake inakuwa si mizuri. Sasa kwa sababu tumeamua kupeleka nguvu zote pale, tuimarishe miundombinu ya ile sehemu moja. Nawapongeza sana kwa kuamua kupeleka zile fedha pale, tuanzie pale basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Keenja, ushirikiane na Mheshimiwa John Magufuli, barabara zile zitengenezwe ili njaa isitokee tena, tutakuja kulaumiana pasipokuwa na sababu wakati uwezo tunao. Mwisho kabisa niseme wazi kwamba, Sera za CCM ziko wazi na naomba ninukuu: “Sera ya kujitosheleza kwa chakula nchini...”

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pole kwa familia ya Mbunge mwenzetu Marehemu Yete Mwalyego. Vile vile, nitoe pole kwa familia ya Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Luka Kitandula.

Mheshimiwa Spika, baada ya pole hizo, nianze kuchangia Wizara ya Kilimo na Chakula, kwanza kwa kumpongeza Waziri, Naibu wake na watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya Jimboni kwangu. Toka mwaka 1995 nilikuwa napiga kelele

kwamba Iramba Mashariki kuna maeneo yanayofaa sana kwa umwagiliaji na kwa kweli Waziri alinisikia na sasa hivi tuna miradi miwili ya umwagiliaji huko Mwangeza na mwingine Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba watu wa kilimo waende Mwangeza na Msingi waone wananchi wanavyojituma kutekeleza hiyo miradi kusaidiana na Serikali ili kilimo cha umwagiliaji kianze. Vile vile, niwapongeze Maafisa wote wa Umwagiliaji wa Makao Makuu na wale wa Tabora ambao tunashughulika nao huko kwetu, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, niipongeze *IFAD. IFAD* kwa kweli ni chombo ambacho kimeamua kuwasaidia Wananchi wa Tanzania. Vile vile, nipongeze Mfuko wa *Tanzania Japan Food Counterpart Fund.* Kwanza wametoa shilingi milioni 125 Iramba Mashariki kwa ajili ya bwawa la umwagiliaji. Pia, wametoa shilingi milioni 118 kwa ajili ya kuchimba mabwawa nane katika Vijiji vya Matongo, Ikolo, Mwangeza, Msiyu, Niganga, Nduguti, Nkungi, Singa na Kinapundu. Kwa kweli tunawapongeza na wananchi wa Iramba Mashariki wanawapongeza kwa hilo na nina imani ahadi ya yale mabwawa 10 yaliyobaki watatupa hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri atume Wataalam wake wa umwagiliaji tena waende kwenye Mito ifuatayo:-

Mto Malasagi, una maji mengi ambayo yanaishia mbugani. Huu Mto ukitengenezewa bwawa unaweza ukamwagilia zaidi ya hekta laki tano. Vile vile, Mto Malela, nao una maji mengi ambao utasaidia Vijiji vya Malela na Mazangili. Pia, eneo la Msiyu, kuna Mto Msiyu ambao hata kiangazi una chemchem nyingi sana za maji zinatoka na Wananchi kwa *scale* ndogo wanatumia kwa umwagiliaji wa kilimo cha vitunguu. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iende iangalie pale ili iweze kusaidia hizi shughuli za umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna Mto Ikolo ambao unaweza ukamwagilia hekta zaidi ya laki tatu. Mwisho ni Mto Ndurumo ambao unaanzia Mkoa wa Manyara unapita Iramba Mashariki unakwenda mpaka *Lake Eyasi.* Wajapani walishakwenda pale wakafanya utafiti na wakaandika *paper.* Mimi niko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Waziri na watendaji wake ili huu mradi uweze kuanza. Huu unaweza ukamwagilia zaidi ya hekta laki saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wizara ya Kilimo na Chakula, sasa hivi haifanyi kazi inavyostahili na matatizo mengine yanaletwa na mambo ya utawala. Kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamekwishasema, Maafisa wa Kilimo wametawanywa, hakuna ile *coordination,* karibu wote wako Halmashauri za Wilaya. Huko Halmashauri za Wilaya wanashindwa kupata uangalizi, wanashindwa kufanya kazi zao za kitaalam, wanakuwa wanafanya kazi za kiutawala.

Kwa hiyo, umefika wakati sasa Serikali iangalie upya irudishe wataalam wawe *answerable* moja kwa moja Wizarani, hapo ndiyo tutaona mapinduzi ya kilimo. Sasa

hivi tutaendelea kuwalaumu Waziri na watendaji wake, lakini ni lazima tusahihishe. Kama tunataka kilimo kitukomboe, kiwe moja kwa moja kutoka Makao Makuu, akikohoa, Afisa Ugani aliyoko Mwangeza asikie kwamba bosi wake kasema hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi habari inatoka Wizarani inapita TAMISEMI, TAMISEMI ndiyo inakwenda kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa ndiyo aipeleke kwa *DED, DED* naye... Ni mgogoro mtupu, hatutafanikiwa bila kubadilisha utaratibu wa sasa! Tuchukue kilimo kama mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, ile kugawanya au kutenganisha kilimo na mifugo kule Wilayani imetuletea matatizo sana. Kuna Maafisa Ugani kule ambao walisomea mifugo na kilimo na wako wengi na wengi wao wamekwenda Wizara Maji na Maendeleo ya Mifugo. Sasa, kule Maafisa ambao wanatakiwa wafanye kazi na wanavijiji wamebaki wachache sana. Kwa hiyo, uangaliwe utaratibu, itafutwe njia jinsi ya kusaidia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni la vitendea kazi Ingekuwa hawa watu wako chini ya Wizara moja kwa moja, kwa kweli wasingekuwa na matatizo. Kule Halmashauri mipango inakuwa mingi, *DED* ana majukumu mengi ya kutekeleza na hata Wizara sasa kwa sababu watu wake hawako chini yao inashindwa kupeleka vitendea kazi. Kwa makusudi kabisa sisi tunaomba Serikali iingilie kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tena kwamba kwa kulima kilimo cha kutumia jembe la mkono hatutajikomboa kamwe. Tutaendelea kuhangaika na njaa itaendelea kutusonga na huku tuna maeneo safi. Tungeomba Serikali ianzishe mradi wa matrekta, haya matrekta yaende kila Wilaya, hiyo ndiyo peke yake itatukomboa. Wananchi wetu wako tayari kukodisha matrekta, lakini hawajui wayapate wapi.

Naomba kama wenzangu walivyosema, waanzishe mpango maalum wa kuinua kilimo hapa nchini la sivyo tutaendelea kulaumiana humu ndani siku hadi siku. Jembe la mkono halitatufikisha mahali, kilimo cha kutegemea mvua hakitatupeleka mahali. Sasa ni lazima tuachane na hii kupanga mipango tu, haitekelezeki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazishukuru Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara ya Afya, wameamua kufanya kweli na wanafanya. Sasa hivi Wizara ya Afya kuna *Basket Fund,* Wizara ya Elimu na Utamaduni kuna MMEM na sasa hivi tunahamia kwenye MMES, kwa nini isiwe kilimo ambayo ndiyo Wizara tunayoitegemea sisi wote? Nina imani kabisa Serikali itaangalia juu ya uwezekano huo na uanze mapema, tusisubiri tena kipindi kingine kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri alivyotuambia ananunua matrekta tisa, huo ni utani. Hayo matrekta tisa yaende kwenye Vituo vya Utafiti wa Kilimo, sisi tunataka matrekta mengi yaende kwa wakulima na yafanye shughuli ya makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo, lakini bado kuna kitu ambacho kwa kweli kimenikera na nilizungumza hapa wakati nachangia Bajeti. Nilikuwa natembelea Wilaya zetu, nikafika Morogoro pale *Morogoro TANSEED,* kwa kweli ni aibu!

Mheshimiwa Spika, ile mali pale inaharibika, ma-*godown* pale yanayaharibika. Kuna *godown* moja kubwa amekodisha mtu analipa shilingi laki moja kwa mwezi, maana yake kwa mwaka ni shilingi milioni moja na laki mbili. Kama *TANSEED* Arusha na kwingine zimeshauzwa hivi Morogoro kuna nini? Kuna wawekezaji wamejitolea kununua. Kuna mtu mmoja aliniambia amejitolea kununua kwa shilingi milioni themanini. Sasa kwa nini pale paendelee kuharibika? Kama sasa tunataka kutumia tuweke mikakati na tuanze kutekeleza. Kwa kweli inasikitisha sana. Mimi kwa hili nimwombe Mheshimiwa Charles Keenja, kama kule ameweza kufanya kazi nzuri kwa nini pale asifanye vizuri? Kwa hiyo, naomba aende aangalie na achukue hatua za haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho nizungumzie juu ya wakulima wa pamba niliowakuta Kilosa na Morogoro, jinsi ambavyo Bodi ya Pamba inawapa madawa yasiyofaa. Wao wenyewe kwenye shamba la pamba wanatumia zile dawa nzuri. Niliikuta hali hiyo nilisikitika sana, usiku ule ule nikampigia simu Mheshimiwa Charles Keenja, sikumpata lakini nikampata msaidizi wake na upande wa pamba nikampata Dr. Kabisa.

**SPIKA:** Mbunge anavunja kanuni anamkinga Spika asikuone. *(Kicheko)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu dakika zangu chache zimepotea kwa hiyo, naomba uniruhusu kuongezewa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, iliniuma sana wananchi wa Morogoro wameamua kulima pamba na kwa kweli ukienda yale mashamba ni ya mfano. Lakini Bodi ya Pamba inawapelekea dawa isiyoua wadudu, inasikitisha sana. Mimi kwa hili ningependa nipate maelezo wakati Waziri anajibu anieleze hatua zilizochukuliwa na kwa nini wale waliozembea na kutoa zile dawa hafifu wasichukuliwe hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, mwingine naye anavunja kanuni hakuna ku-*cross* katikati ya Spika na Msemaji. Endelea Mheshimiwa Philip Magani.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Kabla sijaendelea nichukue fursa hii kama walivyofanya wenzangu kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Ruangwa kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, pamoja na wapiga kura wake, nawapa pole sana kwa msiba uliowapata.

Baada ya kusema hayo niseme moja kwa moja kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo machache tu ya kuchangia hapa na pale. Mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, waliotangulia, mengi nina hakika yale ambayo yaliyozungumzwa miaka iliyopita tunarudia yale yale. Kwa hiyo, ningependa kutoa ushauri, sina hakika kwamba Waziri Mheshimiwa Charles Keenja, anayo majibu ya papo kwa papo ya kujibu hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Ningeshauri kwamba achukue hoja hizo na ushauri ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge, akae chini na watalaamu wake watafakari na kujaribu kutafuta jinsi gani wanaweza kujiondoa katika hali ya kilimo duni tuliyonacho sasa hivi. Tatizo kubwa waliozungumzia Waheshimiwa Wabunge, waliotangulia mimi nadhani tatizo kubwa ni ukosefu wa mipango iliyo wazi ya maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilimo bila mipango huwezi kuendelea, utajaza ma-*book* maandishi mengi ambayo kwa kweli hayatupeleki mahali popote. Ni sawa sawa na kule kwetu sisi tunakula ugali na kitoweo, nyama au mbaazi au choroko ndiyo unakuwa mlo. Sasa ukileta ugali peke yake bila kitoweo bado haujawa mlo. Ili uwe mlo ni lazima ule ugali pamoja na kitoweo. Sasa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa maana hiyo inatuletea hapa ugali bila kitoweo.

Mimi nashauri kwamba iwekwe mipango iliyo wazi. Katika mipango ya kilimo ni lazima tubaini mazao yetu tunayotaka kuyalima katika maeneo yapi, tunataka kuyapanua kwa kiasi gani? Kwa mfano, ukichukua pamba unasema sasa hivi tunazalisha mathalani beli laki nne kwa mwaka, unaweka lengo kwamba baada ya miaka mitano tunataka tuwe tumefikia beli bilioni moja.

Sasa baada ya hapo ni lazima uweke mikakati ambayo itakuwezesha wewe kufika kwenye mabeli milioni moja. Utazingatia eneo lilipo, utazingatia matatizo ambayo yamejitokeza yamebandikwa kwenye *Research Institutions* zetu na kubaini wakulima hao wako wapi na kutayarisha maofisa ugani waende wakawasaidie wakulima wale katika upanuzi wa eka zao pamoja na ushauri wa kutumia pembejeo za kisasa. Wakati huo huo lazima ufuatilie mwaka hata mwaka, ni kiasi gani cha *acreage* kimeongezeka na kiasi gani cha zao lile kimeongezeka na hivyo kuona kama unaelekea kwenye malengo ambayo umejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano zao la korosho katika mwaka 1962 ndiyo mwaka Serikali iliamua kutoa kipaumbele kwenye zao la korosho, uzalishaji wakati huo ilikuwa tani 35,000 kwa nchi nzima. Lakini watalaam wakiongozwa na Wizara ya Kilimo, walikaa chini wakaamua kwamba zao hili ni ukombozi wa watu wa Kusini walikaa chini wakaamua kwamba zao hili ni ukombozi wa watu wa Kusini kwa hiyo tutapanua uzalishaji wa korosho. Walichofanya ni nini, kwanza kabisa walizingatia kuwa kuna maeneo ambayo yanafaa kupanda korosho, lakini maeneo yale yalikuwa hayana barabara kwa hiyo, Halmashauri zikapewa jukumu la kutengeneza barabara ya kupeleka kule. Halafu wakulima wakahamasishwa waende kwenye maeneo mapya, kisha maofisi

ugani walitayarishwa, wakapewa mbegu waende wakasambaze kule na kusimamia upandaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi ule ulifana sana ukizingatia kwamba kwa bei tuliyokuwa nayo wakati ule ilikuwa inachukua miaka kumi kufika *maturity* ile ambayo inazaa kwa uwingi ambao ungetarajia uzae, korosho zile ambazo zilipandwa kuanzia mwaka 1961, 1962, 1963 ndiyo zilileta mazao ya korosho kufika tani 145,000 miaka kumi iliyofuata mwaka 1973/1974. Ni kitu ambacho kinawezekana, ukifanya kwa kila zao.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa kwamba tutaweza kupanua kilimo chetu kwa nchi nzima. Tumeona hapa kwa miaka mitatu, minne, iliyopita ukuaji wa kilimo umekuwa kwa wastani kati ya asilimia mbili, asilimia nne kama alivyosema mwenyewe. Waziri mwenyewe anakiri kwamba ili kilimo kisaidie katika uondoaji wa maskini, kilimo kinatakiwa kikue kwa wastani wa asilimia kumi. Sasa mimi hapa sioni mipango ambayo imewekwa ya kuhakikisha kwamba ukuaji wa kilimo unafikia asilimia kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala walilozungumzia Wabunge wengi nalo ni suala la pembejeo. Suala la pembejeo nadhani sina la kuongeza sana isipokuwa ningeshauri kwamba Serikali izingatie ushauri ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge na vile vile izingatie hali halisi hapa nchini ikoje katika upatikanaji, uagizaji na usambazaji wa pembejeo. Matatizo yamejionyesha na tukae chini tuyamalize matatizo ili wakulima waweze kupata pembejeo zao wakati muafaka na kwa bei nafuu.

Katika hilo hilo tunazungumzia hapa juu ya pembejeo, watu wote waliozungumzia juu pembejeo ya kemikali. Lakini katika ulimwengu wa leo pembejeo ya kemikali imepigwa vita. Kwa hiyo, napendekeza kwamba Wizara irudi nyuma tena twende tukaanzishe kilimo kinachoitwa *mixed farming,* siyo *mixed cropping, mixed farming* maana yake ni kwamba unakuwa na mifugo pamoja na mazao ya kawaida. Katika hali kama hiyo, mkulima unajipatia kile kinyesi cha ng’ombe pamoja na majani au mabua ya mahindi unayachanganya unapata mboji *(farmyard manure, organic manure).*

Mheshimiwa Spika, ukiitumia ile ndiyo inakubalika katika soko la chakula katika dunia ya leo. Uzuri wa *organic* kama *farm yard manure* uzuri wake ni kwamba huna haja ya kuweka kila mwaka, kwa sababu *farmed manure* ubora wake unakaa kwa muda wa miaka mitatu, minne, mitano ile mbolea bado inabaki tu chini kwenye udongo wake, kwa hiyo huna haja ya kununua pembejeo kila mwaka.

Kwa hiyo, nashauri kwamba katika sehemu ambayo kuna mifugo, utaratibu huu unazishwe. Kule ambako hakuna mifugo ipelekwe mifugo ili utaratibu uendelee. Hivyo ndiyo jinsi ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo.

Niongelee juu ya kilimo cha umwagiliaji. Nashukuru sana kwamba Wizara imetuletea katika Wilaya ya Ruangwa, katika Vijiji vya Chikoko, Mkowe na Mnacho mradi wa *irrigation.* Ni matumaini yangu kwamba mradi huu utawasaidia sana wakulima

wa sehemu zile kwa sababu mpaka leo wakulima wale ukienda sehemu yao wakati wa kiangazi utakuta kote kuko *green,* kunanyweshwa maji, lakini wanatumia ndoo.

Sasa katika mipango hii ambayo imebuniwa na Wizara ni matumaini yangu kwamba tutafanya utaratibu wa ma-*dam* kule kwenye milima ili kuvuna maji, maji ambayo yatasaidia katika kuboresha *irrigation scheme* katika maeneo ambayo nimeyataja. Katika hilo hilo watu wengi wameongelea juu ya kuvuna maji kwenye malambo, kwenye visima na kadhalika. Lakini tunasahau kwamba maji haya yanatokana na mvua hata maji mnayosema *irrigation* kwenda kule Egypt ni mvua ambayo inanyesha Kagera, kama Kagera hakuna mvua ule Mto Nile utakauka, maji hayaendi Egypt au siyo?

Kwa hiyo, ili upate mvua tunahitaji kuhifadhi misitu yetu katika *catchment areas.* Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba sekta ya misitu amesema atakapoleta hoja yake hapa umuhimu wa kuhifadhi misitu yetu katika *catchment areas* ili tuweke *sustainable supply* ya maji kwa kupitia mvua. Tusipofanya vile tutakuwa sahara nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia napenda kusema kwamba kilimo ni fagio la chuma la umaskini. Kama tukiweza kuandaa miradi muafaka tutakuwa tumesaidia kuondoa umaskini uliokithiri hususan vijijini. Katika Wilaya ya Ruangwa, tumeanzisha utaratibu wa kilimo kwa vijana unaitwa Kijiji Mtoto. Hii maana yake ni kwamba katika kila kijiji tunaweka maeneo mapya ambako vijana wanakuwa *encourage* kwenda kuonyeshwa mashamba huko badala ya kugawana mashamba ya wazazi wao hapa. Wakaanzisha mashamba kule na Serikali inawasaidia kupata mbegu na ni imani yangu kwamba msaada utaongezeka kwa kuwapatia utalaam vile vile. Tunadhani hii ni njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba vijana badala ya kukimbilia mijini watabaki vijijini. Namwalika Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula aje aangalie jinsi tunavyojitahidi kuondoa umaskini kwa kupitia vijana katika utaratibu tuliouanzisha wenyewe wa Kijiji Mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sina nyongeza zaidi, isipokuwa ningependa tena kum-*encourage* Waziri aweze kuyatafakari yale ambayo yamezungumzwa hapa, ikifika siku ya siku tukae tuweze kutengeneza mradi wa maendeleo ya kilimo hapa Tanzania kama ilivyopendezwa na Kamati ya Kilimo na Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe rambirambi zangu kwako wewe Mheshimiwa Spika, familia ya Mheshimiwa Yete Mwalyego, pamoja na wananchi wa Jimbo lake la Mbeya Vijijini kwa kuondokewa na mpendwa wao. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa Bajeti hii nzuri ya Kilimo. Naamini Serikali inajitahidi sana katika suala zima la kusimamia kilimo. Kwa kuwa kazi kubwa ya kilimo inapendwa na wananchi wote katika nchi hii, kwa hiyo nadhani bado anayo kazi ya kuhakikisha na kudhibiti suala zima la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naomba niunge mkono kwa asilimia mia kwa mia, Bajeti hii ya kilimo. Suala la kilimo nadhani limezungumzwa na mimi nitajitahidi tu kusema kwa upande wangu jinsi ninavyoona katika suala hili la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo kinaonekana sasa hivi ni kama vile hakionyeshi mabadiliko, pamoja na kwamba Serikali inajitahidi na kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza katika hotuba yake na alivyoonyesha jinsi Serikali inavyotumia hela nyingi katika kushughulikia miradi mbalimbali inayohusu kilimo. Lakini sijui kwa nini bado haionekani kwamba kazi hii inafanywa na kwa kweli inaonekana hata fedha zinazotumika na kwa ujumla inagusa karibu Wilaya zote, Mikoa yote.

Sasa labda kwa kuwa inafanyika katika vipande vidogo vidogo, lakini mimi nasema kwa maeneo ambayo tayari Serikali imeshashughulikia ni vizuri tukawapongeza na kuonyesha kwamba Serikali imefanya kazi. Sasa sisi tusemee tu yale maeneo ambayo tunadhani kwamba tukichangia Serikali itatusikia na itayashughulikia maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo, ili kilimo kionekane kwamba kinaleta tija nzuri au kinaleta mapato mazuri ni pale kinapoboreka. Kuboreka kwake kuna taratibu zake. Naamini watumishi na watendaji wa kilimo wajitahidi sana, si leo tu kuanzia huko nyuma, kuanzia hata baada ya kupata uhuru ilikuwa ikizungumzwa kilimo, idara imejitahidi kutoa mafunzo ya aina mbalimbali, imeendesha semina za aina mbalimbali, imefanya kazi kubwa katika kuhakikisha kwamba wananchi tunaelewa na tunatumia maelekezo hayo au kanuni hizo za kilimo. Lakini mpaka leo bado kilimo kinaonekana si kamilifu.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niishauri Serikali, ninavyoamini na nadhani wananchi wanavyoamini kwamba ili kilimo kionekana kinafanya kazi lazima kuwe na maeneo yanayoonekana kwamba sasa hii ndiyo kazi inayofanywa na Serikali.

Moja, ni kuhakikisha suala la matrekta tusaidiwe na Serikali. Mimi ningeiomba Serikali isijitoe kabisa kwamba sasa suala la matrekta liachiwe wafanyabiashara kwamba wafanyabiashara wanunue wapeleke kwa wakulima au wakulima wakatafute matrekta hili kwa kweli bado idara itakuwa inaonekana au Wizara itaonekana kwamba haifanyi kazi.

Lakini ikaweka utaratibu mzuri kabisa kwamba kila Wilaya au kila Mkoa ukapatiwa matrekta ya kutosha, labda kwa mfano sisi wa Mkoa wa Dodoma tukaambiwa

labda sasa matrekta 50 au matrekta 100 yanakuja kwa ajili ya Mkoa wa Dodoma. Basi Mkoa ufanye utaratibu wa kuyagawa katika maeneo fulani fulani.

Kwa hiyo, kwa utaratibu huo, ni kweli kabisa itaonekana Wizara inafanya kazi. Lakini wananchi wanaposikia kwamba ili kilimo kiendelee basi tunatengeneza miundombinu ya barabara wanaona kwamba barabara bado hazina uhusiano na kilimo. Lakini ukiwapelekea trekta wataona sasa kwa kweli kilimo ndiyo kinafanya kazi.

Kwa hiyo, mimi nina ombi kwamba matrekta yatafutwe. Ni vizuri Serikali itumie hela nyingi katika suala la kununua matrekta. Tunavyo vyuo, tunavyo vitengo mbalimbali ambavyo vinaweza vikasaidia kusimamia matrekta haya. Kwa hiyo, mimi naomba kabisa Serikali isijitoe katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine kama tunavyofahamu kwamba akinamama ndiyo wakulima wakubwa huko vijijini kwa sababu mjini hakuna kilimo hata wa mjini wanatoka mjini wanakwenda kulima vijijini. Sasa ni nani ashughulikie suala la kuona kwamba hawa akinamama wanashughulikiwa kikamilifu katika kazi zao za kilimo, wote tunafahamu kwamba akinamama ndiyo wakulima wakubwa. Sasa usipomsaidia huyu mama kwanza unampa hali ngumu kwa sababu kama tunavyojua mama anafanya kazi nyingi sana. Mama ni mlezi wa watoto, mama ni mtunzaji wa watoto, mama ni mkulima, mama ni msaidizi wa shughuli nyingi ndani ya nyumba. Kwa hiyo, unaposhindwa kumsogezea huduma karibu ya kilimo maana yake ni kwamba unamwongezea mzigo. Lakini ukimpunguzia kwa kumsogezea trekta, angalau basi mama anaweza akapunguza shughuli zake au akatumia muda wake vizuri katika kutimiza mipango ya kazi zake au kulima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ningeomba sana Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha nguvu kazi ya akinamama inatumika vizuri. Hilo Mheshimiwa Waziri kwa kweli tungeomba wakati wa kujibu hoja, basi utuambie kwamba sasa akina mama wa Tanzania Wizara ya Kilimo na Chakula inatusaidiaje. Kwa hiyo, naliomba hilo na ni vizuri akalitolea majibu kwa sababu akina mama wanatusikiliza vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nilikuwa naomba nizungumzie juu ya fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Fedha zilizotolewa na Serikali katika kipindi kilichopita zinaonekana ni nyingi sana kwa sababu zinafikia shilingi bilioni tatu na zaidi. Sasa hivi fedha kama zingewekwa katika miradi michache ingewezekana kabisa miradi hiyo ingekamilika vizuri na ingefanya kazi vizuri.

Suala la kutawanya fedha kwa miradi mbalimbali na fedha kidogo kidogo bado hiyo ndiyo itaonekana zaidi Wizara ya Kilimo na Chakula haifanyi kazi. Ni suala tu la kuweka utaratibu au la kuweka ratiba kwamba sasa fedha za Mkoa huu kwa mfano labda Mkoa wa Dodoma ili kukamilisha mradi wa umwagiliaji vizuri, basi itakuwa ni Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Singida, Mkoa wa Iringa, mikoa mitatu kwa mwaka huu na ratiba hiyo ikajulikana ya mwaka hadi mwaka ni jinsi gani fedha zitagawiwa kwa ajili ya kukamilisha miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la kupeleka hapa shilingi milioni mia tano, shilingi milioni 20, hapa shilingi milioni 30 kwa kweli labda tu tunataka kwa sababu basi tuonekane Serikali inagusa gusa maeneo. Lakini sasa tabia ya kugusa gusa maeneo bado haitusaidii kwa sababu haisaidii kukamilisha miradi vizuri na inawezekana kabisa katika kukamilisha hiyo miradi ni kwamba miradi inakuwa ni midogo midogo na bado hiyo miradi midogo midogo haitoshelezi katika suala zima la kumwagilia. Sasa mimi niombe tu Serikali kwa ujumla kwa kweli hebu ianze kufikiria upya kwamba fedha hizi izigawe namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naishauri Serikali ifanye hivyo. Hata ukiangalia basi katika suala la matumizi ya fedha za kuendesha miradi, bado nazo vile vile ni kidogo. Sasa utatoa shilingi 200,000/=, kufuatilia mradi fulani kweli hizo kweli huo mradi kweli utakamilika? Maana yake ni kwamba ni watalaam wanakwenda mara moja wakirudi fedha zimekwisha, matokeo yake ni kwamba huo mradi hautasimamiwa. Ndiyo mimi nashauri kwamba pengine hizi fedha itolewe ratiba na zigawiwe vizuri na ili kukamilisha miradi na miradi iwe mikubwa itusaidie kilimo cha kiangazi ambacho kwa kweli kitasaidia kupunguza tatizo la njaa.

Mheshimiwa Spika, vile vile niiombe Wizara kwamba pamoja na miradi hii ya umwagiliaji pamoja na kuonyesha hapa kwamba fedha za matumizi hapa ndivyo zinavyoonekana lakini wakati mwingine ni vizuri watendaji wetu wakawa wazalendo kwa kwenda kufanya kazi kwa maana kwamba waonyeshe Wizara yao inafanya kazi. Pamoja na kwamba ni kweli mimi naamini Wizara inafanya kazi lakini matatizo yanayojitokeza ni kwamba ile miradi inakuwa haikamiliki au inaonyesha kwamba bado haifiki katika hatua inayotakiwa katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la kuhifadhi chakula. Sasa hivi Ofisi ya Waziri Mkuu, ndiyo inayoshughulikia suala la kununua chakula na kuhifadhi. Wenzangu wamesema sasa sijui mpaka sasa wamenunua kiasi gani. Lakini nataka nishauri Serikali kwamba suala la kuwa na Kitengo Ofisi ya Waziri Mkuu, bado ni tatizo kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu, ni ofisi ambayo inaheshimika na inaonekana katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa mara nyingi kuifanya iwe ndiyo ya kununua akiba ya chakula kwa maana ya kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula, mimi ningeomba suala hili pengine lifikiriwe upya. Kwa sababu linapotokea tatizo si vizuri kuilaumu Ofisi nzito kama hii. Mimi nafikiri suala la akiba ya chakula lingeanzishwa rasmi kabisa na Serikali isimamie katika maeneo ya Kata, Wilaya na kwa kweli ndio wako karibu na wananchi.

Kwa mfano, Kijiji au Kata ikaweka akiba ya chakula na kikawekwa kwa utaratibu ambao wananchi watashirikishwa. Sasa kama wananchi watashirikishwa maana yake ni kwamba watakuwa wanajua kwamba kila mtu kaweka akiba kiasi gani. Kwa hiyo, ni yeye mwenyewe atawajibika kutumia vizuri chakula alichonacho ndani na kuona kwamba kile alichonacho cha akiba atakitumia wakati gani.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nafikiri pengine ni vizuri basi kitengo hiki kihame kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kiende Wizara ya Kilimo na Chakula ili Wizara ya Kilimo

na Chakula ikishushe chini. Zile fedha zinazotengwa kwa ajili ya kununua chakula cha akiba basi zipelekwe katika Halmashauri na ziweze kununua chakula katika Halmashauri hizo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili hiyo, unga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Kengele ya pili!

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mmh! Jamani. Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie hoja hii. Kwanza kabisa naomba nitoe pole zangu kwa ndugu na marafiki na Bunge zima kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi hii kumpa hongera Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge mwenzangu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, mjibu maswali mahiri wa Wizara hii, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Bwana Wilfred Ngirwa na Watendaji wake wote kwenye Idara zote na vitengo vyote kwa kuandaa hoja hii kiufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Wizara hii ya Kilimo na Chakula, Jimbo la Kilombero kupitia uwakilishi wangu, limekuwa mgeni wa kila siku hasa kwenye hoja za pembejeo, zana za kilimo, uwekezaji hususan kwenye Kampuni ya Sukari ya Kilombero na hasa kabisa pale ambapo Taifa letu lilipokuwa linakabiliwa na janga la njaa. Nawashukuru sana kwa ushirikiano wao, mwongozo na uvumilivu pale nilipokuwa nikienda kuomba msaada kwa ajili ya Jimbo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie hoja hii kwa kuelekeza mawazo kwenye sehemu ya XVII ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri hususan ibara ya 118 mpaka 129 ambapo Wizara imeelekeza lengo la kuweza kuongeza uzalishaji kwenye Sekta hii na hatimaye kutuwezesha kuwa na hifadhi ya chakula nchini kwa huko Kilombero.

Mheshimiwa Spika, ningeiomba kwa kutekeleza hili tuwezeshwe kupewa zana za kilimo, kuimarisha miundombinu hususan barabara, huduma za ugani pamoja na mbegu bora na umwagiliaji rahisi. Uzalishaji huu wa tija utawezekana sambamba kabisa na hotuba ya Rais ya tarehe 12 Februari, 2004 ambapo Serikali imezungumzia uwezo wa kuwawezesha wananchi kupata mitaji na hiyo imeelezwa vizuri kabisa kwenye hotuba ya Waziri kwenye ibara ya 120 kwenye kifungu kidogo cha (a), (b), (c) na (d) na hasa kabisa

kile cha (b) ambapo anazungumzia uanzishwaji wa *SACCOS* na kushirikisha *SACCOS* hizo na Benki ili watu waweze kupata mitaji ya kulimia.

Sasa kwa Kilombero kwa nguvu za Mbunge na wapigakura tumeanzisha Vituo vya Kilimo na Kituo cha kwanza tulifungua mwisho wa mwezi Januari, 2004 tulifungua kwenye sehemu inaitwa Michenga na Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ndiye aliyekuja kukifungua. Jicho la Jimbo zima kwetu sisi ni kilimo.

Kwa hiyo, tunaomba kama alivyoainisha kwenye sehemu ya hotuba yake ibara ya 120 ya uwezeshaji ya mipango ya maendeleo kwenye Wilaya, basi atusaidie miundombinu ili tuweze kukamilisha Vituo vingine hususan vile vya Mofu, Chita, Chisano, Mlimba, Matema na Utengule. Uongozi wa Vituo hivi kidogo ni tofauti na kama vile Vituo vya hapo awali. Tumejaribu kuwashirikisha wananchi wenyewe wahusike na Kituo, lakini kwenye kuhodhi zana za kilimo watu binafsi waweze kuingiza ili tugawe majukumu ya wahodhi wa Kituo na wahodhi wa zana ili tuweze kukabiliana na ubadhirifu ambapo hapo awali kwenye Vituo vingine uliwahi kutokea.

Kama nilivyosema, hivyo inawezekana tu kama *SACCOS* za Vituo hivyo vitakavyoanzishwa zitawezesha kupata mikopo bila utata. Kupitia mpango wa maendeleo kama ilivyozungumzwa kwenye hotuba yako ya Wilaya pamoja na ile ya *PADEP* basi na kwa kuwa Morogoro imezungumziwa ni kati ya Mikoa iliyochaguliwa, basi na sisi Kilombero tuingizwe hapo.

Baada ya kusema hilo, niende tena kwenye sehemu ya XXII ambapo tunazungumzia umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri amesema umwagiliaji utaongezeka kufikia hekta 254,610 kutoka 227,486 na atafanya hivyo kwa kuhakikisha anakarabati mabwawa na kusimamia uvunaji wa maji ya mvua. Kwangu Kilombero hilo sio tatizo ndio maana nilisema hapo awali basi na sisi tuwezeshwe kwa umwagiliaji rahisi. Ninachohitaji ni Kilombero kwa Hazina zangu za mito pamoja na shehena kubwa ya maji tunaomba tu kupitia *SACCOS* tukopeshwe pampu za maji.

Mheshimiwa Spika, sehemu za kumwagilia Kilombero kama utakumbuka nilizungumzia mwanzoni kabisa kwenye hotuba yangu ya mwanzo kuwa takribani hekta 17,323 za kuweza kumwagilia na sehemu kubwa kati ya hizo ni pamoja na *Kilombero Sugar Company,* Lwipa, Mngeta, Ihanga na nyingine ndogo ndogo za Kisasawa, Mkula, Msolwa, Idete, *Msolwa Estate* na Ihanga. Sehemu hizi zote zinaweza kabisa zikatumika kuongeza pato la chakula na hasa kabisa kuitambua kuwa Kilombero hivi sasa kwa kilimo chake hakihitaji mbolea za viwandani. Mbolea namba moja ni maji na tunayo ya kutosha.

Kwa hiyo, nadhani kwa uwezo na taratibu iliyounganishwa kwenye hiyo sehemu ya 22 tukiwezeshwa kwa kuweza kupata fursa ya kuweza kuuza vyakula nje kwenye *AGOA, EBA* na sehemu nyingine tunaweza tukawa wazalishaji wakubwa wa *organic food.*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba tuangalie hapo kwa kutuwezesha sisi hasa kabisa kupitia hivyo Vituo na sisi tuingilie pia kwenye hiyo Sekta ya Umwagiliaji. Pamoja na hoja zote ambazo tumechangia wote za kuweza kukosoa Wizara hii, lakini ni lazima tutambue kwamba Wizara hii ni ngumu, kubwa na kuwa dhidi ya haya yote ndio sekta pekee inayochangia kipato kikubwa katika nchi. Kwa hiyo, inahitaji kabisa kila juhudi ya sisi sote kuweza kuisaidia Wizara hii kuipa moyo ili iweze kuendelea na mipango hii ambayo imeanzishwa.

Mheshimiwa Spika, nikipitia kitabu cha nne, Mpango wa Maendeleo, kitu ambacho kinajitokeza ni kuwa hela nyingi za maendeleo ni za Wahisani na kama ni hela za Wahisani sio rahisi kubadili mipango ambayo tumeambiwa tuitekeleze.

Kwa hiyo, nadhani jukumu hapa ni kwa Serikali yenyewe. Kama nilivyosema kwenye Hotuba ya Bajeti kuwa tujaribu kama tulivyoweza kwenye Sekta ya Barabara, tuongeze kipato kutoka mchango wa ndani kuipa Wizara hii ili tuweze kuzalisha zaidi na hatimaye tufikishe uwezo wa Sekta ya Kilimo kuchangia kwenye Bajeti ya nchi, naamini kabisa tutakapofikia kwenye takribani asilimia 70 ya mchango, basi hata ule utegemezi kwenye Bajeti utapungua.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyoelewa hivi sasa utegemezi kwenye misaada ya *HIPC* ni karibuni asilimia 40 lakini asilimia 23 ndio yenyewe hiyo mingine ni mikopo na kukopa ni utaratibu wa kote duniani, hakuna Serikali isiyokopa. Kwa hiyo, naamini tukiweza kuisaidia Wizara hii ikaongeza uzalishaji ikafikia wao kiwango cha kuongeza pato la nchi kwenye asilimia 70 basi tutabakia na jukumu tu la kukopa lakini sio la kuchangia Pato la nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naamini kuwa Wizara hii inafanya kazi nzuri, lakini tukizingatia kuwa tuna Sera ya Utawala Bora kwenye Wizara hii, lazima pia tuhimize hilo. Utawala bora na uwezeshaji wa mgao kama utakuwa kwenye Pato la nchi kwa Wizara hii, tunaweza hatimaye na sisi tukaweza kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, *Global Village* kwetu sisi tutakuwa ni watazamaji na sio kitu cha kutegemea hata kama tutasema dira yetu ya mwaka 2025 tutafikia lakini naamini kabisa sisi tutakuwa bado pembezoni lakini tusiwe pembezoni zaidi kwa sababu bila kukazana na bila kupeana nguvu ya uzalishaji tutatupwa nyuma na hatutapata nafasi ya kuogelea kwenye hilo bwawa la *global village.*

Mheshimiwa Spika, ni nguvu, ustadi, kuchukua teknolojia mpya, kuzijua kila wakati, hata kama tunaweza kuzitumia ili na sisi tubakie angalau pembezoni ya hicho Kijiji bila kutupwa mbali na hatimaye kama tutaweza kufanikiwa na sisi tutumbukie kwenye hilo gurudumu kwenye *excel* ya mzunguko. Vingine vyovyote vile kama hatutaweza kuwezesha kilimo kikakua na kupunguza ajira ya watu kutoka kwenye Sekta ya Kilimo kwenda Sekta nyingine, basi tutarudi tena kugeuka nyuma ambapo uchumi ulikuwa hauna Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja na kuiombea kila la kheri Bajeti hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie katika Wizara ya Kilimo na Chakula. Awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake, kwa jitihada wanazozifanya katika kuhakikisha kwamba wanawashughulikia wakulima na kuwawezesha.

Mheshimiwa Spika, inakuwa vigumu kwangu kuelewa kwamba jitihada za Wizara kushughulikia kilimo na kukiimarisha wanazipata namna gani, ule ujuzi wanaupata namna gani kama wanaelewa kile ambacho wanapaswa kukifanya. Kutokana na maswali na mijadala inayokuwa inaendelea sio hapa Bungeni tu, bali na nje ya Bunge kuhusu kilimo, ningependa nipendekeze kwa Mheshimiwa Waziri kama kuna uwezekano, basi ilikuwa ni wakati muafaka kwa Taifa kama Taifa kukaa chini likatunga Dira ya Maendeleo ya Kilimo. Dira peke yake kuondoa ile ya Dira ya Taifa ya mwaka 2000 - 2025 kwamba tuna Dira ya Maendeleo ya Kilimo na tukihusisha kilimo na suala zima la kufuta umasikini watu wakakaa waka-*brainstorm* wakajadiliana wakaona ni vitu gani viweze kufanyiwa kazi.

Lakini vinginevyo kutokana na ukubwa wa nchi hii na ukubwa wa shughuli yenyewe na jinsi mambo yanavyofanyika kwa sababu hapa tunavyoshughulika na kilimo unakuta kwamba Waziri Keenja sio yeye anayekwenda moja kwa moja kutoka Dar es Salaam mpaka Kijijini, ana-*interact* na Wizara nyingine. Kwa hiyo, anafanya kazi kwenye *system.* Sasa matumini ya yeye kufanikisha hiyo shughuli yake kwa kweli namsikitikia. Kama hatuwezi tukakaa tukapanga tukasema hii ni dira kwa ajili ya kilimo miaka 20, 25, 30, 40 huenda tukakwama. Kwa mfano, nilikuwa naangalia walivyogawa, wala hawaelezi hiki kilimo wamekigawa katika makundi mangapi kwa mujibu wa jiografia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama kuna nchi tajiri na watu ambao ni matajiri kuliko nadhani nyingine ni sisi kwa mujibu wa sera sahihi za Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kwa sababu kila Mtanzania, walio wengi wana ardhi na kila Mtanzania angependa ardhi, hawezi kukosa ardhi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sidhani kama kuna watu 10,000 wanaweza kusema sisi Serikali tunaomba ardhi tuko hapa, wakaikosa. Sasa kama hivyo ndivyo ilivyo tuambie Wizara imefanya namna gani kwa sababu iko mipango ya kujua kwamba tunawa-*target* kundi la mkulima mmoja mmoja. Tuna *target* mbili, kundi la watu ambao wamejiunda kwenye vikundi vikundi kama vya ushirika. Ni lazima muwe na *experience* kwamba ujamaa ulikufa na kule walikuwa wanalima kwenye vikundi. Kwa hiyo, kama wale wanaopenda na wanaweza basi mjue mnawasaidia namna gani. Yule anayetaka kulima peke yake mjue mnamsaidia namna gani.

Tatu, ujue kwamba kuna wakulima wa kati, hawa Waafrika wanaweza wakawekeza kama Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya nadhani, yeye tunamsaidia

namna gani? Nne, je, tunapaswa kuwa na kundi la wakulima wakubwa au wanasema wenye Makampuni wanaweza kuwekeza kama walivyowekeza kwenye miwa pale Kilombero? Kama ni suala la ardhi tunayo hapa hiyo mnayoisema, tufike mahali tukubaliane kwamba hii tunaitenga ardhi yenye ukubwa kama Mkoa wa Tabora tunatenga tunawaita watu, tutawawekea masharti walime hapa. Kwa sababu bahati nzuri madini mmewapa wamechokonoa yanakwisha. Lakini kwa ardhi, hata kama wakikaa miaka 300 tunaweza tukawanyang'anya kama Zimbabwe. Lakini waweze kulima, tuelewe hawa tunawasaidia namna gani na tunaweka *incentives* namna gani. Kama hamuwezi kugawa, hivi ninyi mnafika tu mnasema mtaendeleza kilimo, kwa kweli mnakabiliwa na hali ngumu.

Mheshimiwa Spika, kuna fedha hapa zimetengwa zinapelekwa Wilayani yaani hapa ndiyo kichekesho kilipo. Utakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa amesema wametenga bilioni tisa za kulipa pesa za Walimu na mimi nina uhakika kwamba hela zile zimetumwa kwa Halmashauri, wakatafuna hela zile zote. Wakatafuna kama wanakula mali ya Marehemu, maana Marehemu hawezi kulalamika. Sasa wewe kama unakula hela za Mwalimu anajulikana kwa jina, anajulikana alikohamishwa, anajulikana aliajiriwa pale na Serikali ikimtafuta inampata na anakulalamikia, ukazitafuna, je, hawa wakulima ambao huwajui unampelekea nani na wewe unamiliki hela, pale Wilayani hizi hawatazitafuna? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hela hizi zote wataziguguna na mwisho wa mwezi sijui zitaishia wapi. Ningekuwa mimi, hela hizi tungezizuia kwanza kwenye Benki za Serikali halafu tukajiandaa. Nasema hivi kwa sababu hao wanaowajibika kwanza hatujui nani tunamtumia hizo hela, mkulima mmoja mmoja, mtu amekaa hapo kijiweni anasema na mimi mnikopeshe hana shamba, hana ardhi, yule ambaye ana mali za kumtosha na anaweza kwenda kukopa Benki lakini kwa sababu ana uwezo wa kuzungumza na Mkurugenzi na Diwani mmoja ndio aje azichukue na yeye!

Mimi sielewi zitakuwa zinamlenga nani na hawa wasimamizi kwa sababu hawako chini ya wajibu wa Wizara ya Kilimo na Chakula, ndiyo maana hapa walitubabaisha sana. Unamwuliza Waziri wa Elimu na Utamaduni, anasema mimi nilizituma kule TAMISEMI, zile za walimu. Sasa hizi ambazo Mheshimiwa Charles Keenja, watu wanapokonya madaraka kule, utamkuta Mkurugenzi amepokonya madaraka yote, anamfukuza Afisa Kilimo pale, sijui anaziweka kwenye *account* gani na sijui kama *account* imefunguliwa. Sasa utaratibu huu haujulikani ni Wakala, ni huyu Mkurugenzi, bahati nzuri Hazina inapotuma hela inatangaza kwenye Gazeti la Serikali kwamba tumetuma hela Wilayani, Afya, Kilimo na Barabara. Wao ikifika kule Wilayani hakuna anayemwajibisha kwamba ninyi fedha zote mlizozipokea hebu andika kule kwenye mbao za matangazo. Wape Madiwani wote, peleka kwenye Kata zote, hakuna anayefanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa alikuwa na fedha nyingi sana. Amekusanya fedha nyingi sana, amepewa msaada mkubwa sana, lakini watu walioko katika Serikali wamekula fedha zile zote na watu wamebakia masikini. Wewe soma kile kitabu cha hela za *STABEX* sijui bilioni tatu, hivi mngekuwa

mnanunua matrekta si tungepona? Hebu chukua zile zote mabilioni mnazonunua pale halafu uangalie mnavyoliangusha Taifa. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba Wizara ifikirie hilo kwamba mrudie upya kabla hamjawatumia hizo fedha. Nani anazipokea, nani anajibu, kuna utaratibu gani na kuna uwezo gani?

Katika MMEM ambako mmeweka masharti na zikaenda kwa watu pale wanazingalia angalau kumekuwa na asilimia zaidi ya 60 ya *transparency* lakini vinginevyo mnakumbuka kuna wengine hawakujibu hapa, nadhani kuna Waziri mmoja alikuwa anapata taabu hapa. Walitaka hata kutafuna hata hizo ambazo wametangaza kwa uwazi wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la ruzuku. Unajua sisi Waafrika tuna matatizo, watu katika nchi za Ulaya wanakaa kupanga jinsi ya kuunda historia, sisi hapa tunakaa kupanga jinsi ya kuizungumzia historia na kuijadili. Kuna watu wengine nasikia wanakwenda kuandamana kupinga kwa nini Ulaya wanatoa ruzuku. Wanatoa ruzuku, sisi tunauza kwa bei ya chini. Sasa unataka wafanyeje? Yaani wewe Taifa kama Marekani na ukubwa wake lisitoe ruzuku watu waache kuzalisha waje kuomba chakula Tanzania! Wewe unadhani sio aibu? Nadhani ni aibu. Lakini ruzuku ile wanayoitoa inatumika kwa malengo kwamba Tanzania kwa sababu wao hatuwezi kwenda kuwapiga hawana silaha na tutapoteza muda wetu, tunawapa chakula, tukiwapa chakula wanakenua meno wanacheka wanatushangilia. Ndiyo maana wanatoa ruzuku. Kwanza wajilishe wao ndani kwa sababu wanaolima ni kidogo na vile vile wapate ziada ya kuuza nje na kuhakikisha hizi nchi ambazo zina uvivu, zinakamatwa, ndio madhumuni hayo! Lakini sio kwamba wao ni wendawazimu tu, wanatoa ruzuku na mnawalalamikia mnadhani wataacha. Sasa sisi tunajifunza nini? Tunajifunza kulalamika na kunung'unika na kulaumu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo lazima tuyaangalie ni ya msingi. Najua uongozi wa juu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukipenda, ukiamua kwamba leo tutahakikisha hizi sheria zote za madini tunazirekebisha, watu wote tunawawezesha, njia zote wanaamua wanafanya na wamefika huko. Lakini inapokuja kwenye kilimo *nobody is concerned.* Sijui kwa sababu wakulima hawawezi kutupiga! Sijui kwa sababu hawawezi kutuadhibu, sijui kwa sababu hawawezi kuja hapa, sijui kwa sababu hawawezi kuandamana!

Mheshimiwa Spika, nadhani wakati umefika maana tunasema hapa tufanye maamuzi ya busara kwa ustawi wa nchi yetu, ulipokuwa unatusomea dua. Hivi Ustawi utakuja wakati watu wengine wanamenyeka kule. Nenda Kijijini umkute mkulima anayeweza kununua shangingi, hamna! Yeye kila siku ni mtu anayetegemea pato lake kwa muda wa miezi mitano katika mwaka mzima. Bei ya mazao ikiteremka katika Soko la Dunia imemwangalia yeye, mpe *compensation,* hakuna! Ukame ukija umemwangalia yeye, lakini ukame hauwezi kuja kwenye mshahara wa Waziri, wala soko la mshahara wa Waziri, kama liko haliwezi kupungua kwamba siku hizi zimepungua kama linavyopungua pato la mkulima. Hapo ukishafikiria, tunafanya mambo ya mchezo mchezo. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa katika suala la ruzuku nadhani mnaogopa kwamba mtabanwa sijui na Mataifa gani. Kuna mambo tutaweza kufanya kama tulipoamua tunanunua *Radar,* mimi sikuwa naipinga kwa sababu nimekaa mpakani najua wanavyofanya Uganda nisingeweza kupinga. Mbona hatukuogopa? Sasa hapa tukisema katika kilimo tunataka kutoa ruzuku tusimame pale tuone inakuwaje, hakuna! Tunaogopa! Suala la utafiti nimekwishaeleza hapa, maana yake inategemea na anayepewa masharti, nataka unifanyie utafiti katika hili na hili.

Nakumbuka kule Uganda, Rais Yoweri Museveni, kahawa ilipoteremka akasema na nimnukuu sio maneno yangu. Akasema, "Najua viongozi wa Kiafrika na wale wengine wana matatizo kichwani. Kwa sababu bei ya kahawa imeteremka, mibuni yote wataifyeka. Sasa ni afadhali mimi nitachukua kila mtu namgawia mche wa kahawa halafu nampa na shilingi 100 akapande ili baada ya miaka kumi hawa kama za kwao walizikata mimi nitakuwa nazo nyingi. Kama sitapata faida kutokana na bei itakayokuwepo, nitapata faida kwa sababu ya kuwa na *volume* kubwa ya kahawa ya kupeleka. *Volume* kubwa atakayemwuzia magunia nitamkata kwenye kiwanda, atakayekuwa anasomba na magari nitamkata." Akahesabu zile zinazotokana na kahawa, akapiga hayo mahesabu.

Mheshimiwa Spika, akaenda hatua nyingine mbele. Nadhani Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, bahati nzuri anakumbuka. Akaja Bukoba akasema hivi Wazungu kwa nini mimi nawauzia kahawa? Kilo moja ya hii kahawa ya kukoboa Dola moja kwenye soko. Ukishakuifanya ikawa unga dola 15 na hivi sasa ninavyozungumza amewapa pale Uganda dola milioni 30 wakajenge kile kiwanda haraka haraka na amekwishachukua masoko kule. Anakwenda China na wafanyabiashara ili akawasaidie na anawa-*connect.* Lakini huku mtu anatoka hapa anakwenda pale China, sijui anakwenda wapi pale kuzungumza mambo ambayo hayapo, anakwenda peke yake. Sasa ukienda peke yako halafu inakuwaje? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tufike mahali tuone kwamba haya ni masuala ya kufa na kupona. Kwa sababu hawa wakulima *they can not move where they are.* Tunazungumzia utafiti, kwanza nimefurahi jana ametaja kwamba wanataka kutengeneza sijui pombe inayotokana na Mkonge. Hiyo ndiyo sasa uangalie maana hapa sisi tunaangalia ile *conventionally* kwamba tuwapelekee wataalam katika Chuo cha Kilimo cha Sokoine sijui Uyole, hapana.

Tufike mahali tuseme tunaweza kupata matumizi gani mbadala wa hiki? Sio za ogani mbadala, mbegu gani mbadala, hapana, matumizi gani mbadala. Katani ndiyo mnapata pombe, nilikuwa naona mnaweza kupata *material* ya kuezekea nyumba tuondokane na kuweka vumbi kule juu na nyasi. Kama ni ndizi tuweze kupata *wine,* kama ni mahindi tujenge kiwanda kikubwa cha kukoboa mahindi kama unga sijui wa Azam sijui wapi tuweze kupeleka Zambia kule, tusaidie kujenga *centre* kama hizo. Huo ni utafitia ambao Wizara ya Kilimo na Chakula, lazima kione, sio kung'ang'ana tu pale, tunataka mbegu bora inayohimili ukame, sijui na nini, ukame upi? *(Makofi)*

Sasa aina ya utafiti tunaoufanya tunataka kuwasaidia wananchi katika masoko, twende tuwaulize. Kuna mambo ambayo yana *sociological aspect* yanaweza kusaidia katika huo utaalam wa kilimo tunaoufanya badala ya yale yenye *scientific aspects.*

Nimalizie na suala la *STABEX.* Mimi sitaki kuwa kichekesho hapa, kila siku nasema *STABEX* na watu wengine wanaguna. Lakini nashukuru tangu niingie hapa Bungeni nilizungumza mara ya kwanza Serikali kupitia Vyama vya Ushirika ilikuwa imezoea vya Karagwe na Kagera, wakatupa, nikazungumzia suala la Masoko hapa nagombana na Mzee wangu Mheshimiwa *Sir* George Kahama, hapa watu wananichekelea, sasa walipotupa hayo masoko yetu tulikuwa tunauza kahawa kwa shilingi 40/=, sasa hivi ninavyozungumza ni Sshilingi 250/=. Tunaishukuru Serikali kwamba iliyasikia hayo. Sasa ninapozungumza *STABEX* hapa kuna watu wengine wanasitiri huku. Tunaomba, sio vizuri Serikali kuwanyonya watu maskini. Mlikwishawaambia hamuwezi kuwapa hata thumni mkononi, sasa hata barabara yenyewe mnawanyima? Ewe Mungu uliyeko juu hebu waangalie watu wabadilike hapa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* naomba anitajie hiyo Kampuni iliyokwenda, hivi na Kyerwa pale imepita? Naomba kabisa kabla sijajibwaga hapa chini aniambie na Kyerwa wamepata? Sasa kama watu mmewadhulumu hela zote hizo zimekuja shilingi bilioni 40 zote mkasema ninyi mliozalisha kahawa Wazungu wakainywa na pua zao, wakafurahi mpaka wakawazawadia hatuwezi kuwapa thumni, mkasema kitakachobaki tutawajengea barabara, hata barabara hamtaki. Hivi ukiwadhulumu watu wa Mungu unategemea yeye aliyewaumba akawapa nguvu wakulima inakuwaje? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nadhani ujumbe umefika. Tuitane hapa Mheshimiwa Charles Keenja, kama unatafuta fedha za Semina, tafuta Wabunge na watu mashuhuri siku tano mkae m-*brainstorm,* mwone mnafanyaje kuhusu kilimo. Haya mambo ya kufanya mzaha hapa hatutaondokana na njaa. Ni aibu kabisa mtu mzima unaweka tai nakuona unakwenda Ethiopia kuomba chakula. Mimi nasema mnacheka, nchi kubwa hivi Mwenyezi Mungu hatatuadhibu kweli na watu wengine wanakufa huko kwa kula mizizi? Sio kwa kula mizizi, mwingine anakufa kwa sababu ukame umeathiri mazao yake. Mazao yake yameteremka bei, hawezi kupeleka mke wake ana mimba wamemwambia Kituo cha afya hawawezi kumpasua wampeleke kwenye Hospitali. Hampeleki kwa sababu ya kumdhulumu. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwona Mheshimiwa Gwassa Sebabili, amerejea Bungeni, kwa kuwa tunao muda, tuna *pressure* kubwa, nampa nafasi atoe mchango wake kama Msemaji wa mwisho kwenye hoja hii.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula.

Kwanza nitangulize kwa kuwapa pole jamii na jamaa ya Mheshimiwa Marehemu Yete Mwalyego ambaye ametutoka siku chache zilizopita na pia nitoe rambirambi hizo

kwa jamaa na jamii ya wananchi wa Mkoa wa Tanga hususan Wabunge ambao wamepotelewa na kiongozi mwenzao, waliyekuwa wanashirikiana naye katika shughuli za kukijenga Chama cha Mapinduzi na kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watumishi wote wa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa maandalizi mazuri ya Hotuba hii.

Kwa vyovyote vile ni hotuba ambayo inalenga kutuondoa hapa tulipo na kutusogeza mbele katika mipango yetu ya maendeleo, kuondoa njaa na kupunguza kama sio kuondoa umaskini. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wakati wote kwa sababu kazi ya Bunge hili ni kuishauri Serikali namna bora ya kutawala na kujenga uchumi na amani na utulivu yako maeneo ambayo lazima tuzungumze kwa ushauri kwamba Wizara ya Kilimo na Chakula inapashwa ifanye kitu.

Mheshimiwa Spika, tumeshakubaliana kwamba kilimo kinalo pato kubwa katika Taifa letu kwa asilimia 45, kwa kupata fedha za kigeni tunazungumzia asilimia 70. Lakini zaidi zaidi ni tajiri mkubwa kwa ajira ya wananchi wa Tanzania ambao hawana mahali pa kugeuzia mbavu zao kujipatia mahitaji yao ya kila siku. Kwa hiyo, ni mwajiri mkubwa sana kwa asilimia 70 mpaka 85. Kwa hali hii ni lazima tukubali kwamba tunahitaji kuona kilimo kinaimarika nchini na tumeishasema kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Ni wajibu wetu sote katika Bunge hili na wale wenye mapenzi mema kwa Taifa letu kuusaidia uongozi wa Wizara ya Kilimo na Chakula kujaribu kuongeza kazi na kurekebisha utaratibu unaotumika hivi sasa kusudi waweze kusonga mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi ninavyofahamu nchi zote ambazo zimeendelea kiuchumi ambazo hasa ni nchi zenye viwanda vikubwa duniani, wengi wao wamepitia katika kazi hii ya kilimo na wengi wao wametumia njia za umwagiliaji maji. Ndiyo nchi hizi hizi ambazo zinajulikana kamba zilistaarabika mapema zaidi tangu karne ya 14 na zikaweza kufahamika na mpaka leo wakaweza kuzunguka ulimwengu na kuwatawala dunia tunayoiita ya tatu sasa hivi. Nchi kama Uholanzi ambayo ni mama wa Afrika Kusini, Marekani, China, Japan, Misri leo India, Korea, nchi zote hizi tunajua kwamba zimeendelea kwa sababu zinamwagilia. Kilimo chao hakitegemei mvua hata kidogo na pengine mvua hawatambui kwamba ipo.

Lakini kwa bahati nzuri tu Tanzania ina maji mengi, kuna maji ya Bahari ya Hindi. Kuna maziwa makubwa sana matatu. Tuna maziwa mengi sana ndani ya nchi. Tuna mito mingi yenye mabonde mapana, mito mirefu. Lakini yote haya hatuyatumii. Tunajua kwamba katika mikoa yetu 26 ya Taifa zima, ni mikoa kama mitano au sita iliyo na mvua kidogo. Lakini mikoa yote hiyo iliyobaki ina mvua nyingi kabisa kabisa. Hasa ukichukua ukanda wa Kaskazini kuja Mashariki. Kaskazini Magharibi kuteremka mpaka Magharibi kwenda Kusini. Mikoa yote hii ina mvua za hakika kuweza kutupa chakula.. Lakini hakuna tunachokifanya na wala haieleweki na wala haiwezi kueleweka kwa nini tuwe wahemeaji wa chakula miaka yote.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumzie Wilaya ya Ngara ina mito miwili mikubwa sana. Ina mto wa Kagera, chanzo cha Mto Nile na ina mto wa Ruvubu unaoingia katika Mto Kagera. Mito hii inapita katika Tarafa tano zote kwa pamoja. Mito hii inapitia katika Vijiji vinavyozidi 60 za Wilaya ya Ngara, Vitongoji ni vingi mno. Naomba niseme kwamba mwishoni mwaka wa 2002 Mheshimiwa Mbawala, Naibu Waziri wa Kilimo alikuwa Ngara, na tunamshukuru watu wa Ngara kwa sababu kwa kweli kazi aliyotuachia na hamasa aliyotuachia imetufikisha mahali pazuri na ninafikiri kwamba ataendelea kufuatilia kuona kama maelekezo yake yanafuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anakubali Wataalam wanasema kwamba mabonde yaliyoko katika mito hii miwili ni zaidi ya hekta 55,000 ni maji ya hakika. Mwaka 1974 Serikali ya Japan ilianzisha mradi wa kumwagilia, kwa wakajenga mifereji mingi katika bonde la Nyakabonde mjini Ngara, wakaweka vituo, wakatuonyesha namna ya kuchimba mabwawa, lakini kama ilivyo kawaida kwamba mara nyingi ya misaada hii wanaotuletea wanapotoka na sisi tunasahau miradi hii iliharibika.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba kwa kweli Wizara hii irudi na kuturudishia miradi hii Ngara tunaihitaji. Kilimo cha kumwagilia Ngara ni kilimo cha jadi na nataka kusema kwamba sisi Ngara hatujawahi kuomba chakula kutoka Serikalini na nafikiri kwa mkoa wa Kagera mzima. Tunayo mvua ya kutosha, sisi hatuhitaji mbolea hata kidogo. Tunachohitaji ni teknolojia. Tunachohitaji ni watumishi, tunachohitaji ni zana za kilimo.

Sasa badala ya kutuletea mbolea sisi watu wa Kagera na hasa hasa Wilaya ya Ngara tunaomba ufanywe utaratibu kama ni mtu mmoja mmoja na ni lazima tufanye mabadiliko katika maendeleo ikiwezekana Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na Wilaya zote nchini ziwekewe nafasi ya kuweza kukopeshwa matrekta kutoka katika mfuko huu wa pembejeo ili tuweze kulima na kujitolesha na kutosheleza Taifa kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mito hiyo kuna mabonde ambayo Mheshimiwa Mbawala aliyaona mabonde ya Mwiluzi, Mpanyula, Migombo, Nyakiziba, Mzaza, Chivu, Kirushya na mabonde mengine mingi sana, mapana na maji ya kudumu wakati wote. Tunahitaji sisi kumwagilia. Ujeuri wa Marekani leo ni kwa sababu wana chakula, si kwa sababu wana majeshi mengi, si kwa sababu wana fedha nyingi. Si kwa sababu wao ni watu wengi.

Lakini ujeuri wao ni kwa sababu wana chakula. Tanzania haiwezi kuendelea kuwa na aibu ya kuendelea kuomba omba chakula. Nakumbuka mwaka wa 1977 Waziri wetu mmoja, Marehemu Shekilango, alikufa kwa ndege kwa kuomba chakula kutoka huko Marekani na watu wote wanajua na ni historia na ni aibu.

Mheshimiwa Spika, sasa leo tunaendelea tena kuomba omba chakula. Tunafikia nafasi ya kutukanwa. Nchi tulizozikomboa kama Msumbiji, juzi Uganda tumeikomboa baada ya miaka mitatu tu wakatuletea chakula, tukaenda kuomba mahindi. Haifai

tukaendelea kuwa na hali kama hii. Tanzania lina sifa kubwa haiwezi kuwa ni nchi ya kuendelea kutajwa tajwa kwa vitu vidogo ambavyo tunaviweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe kabisa iwezekane Serikali iweke utaratibu wa kuona kwamba nguvu kazi inaimarishwa, kama Sheria hii haitoshi basi nguvu kazi iwekewe sheria. Vijana wengi hawana kazi. Vijana wengi wameingia katika masuala ya kuzurura, kula madawa ya kulevya. Ndiyo sasa wanafanya fujo za ujambazi ni kwa sababu hawakuandaliwa vizuri kuweza kujitegemea. Sasa kupitia kwenye Wizara hii na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo pia Ustawi wa Jamii. Nafikiri wakati umefika tuondokane na aibu hizi. Taifa hili haliwezi kusifiwa kwa mambo mengi lakini likabaki Taifa linaloombaomba kwa sababu lina njaa, kumbe nchi yetu inaweza kuzalisha chakula cha kutosha na kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii haina watumishi. Naomba Mheshimiwa Waziri akubali kabisa, Wizara hii haina watumishi. Waliokufa hawakurudishiwa, waliostaafu hawakurudishiwa, kulikuwa na *retrenchment* hakuna kitu kilichofanyika kama hicho cha kurudishia.

Sasa kwa babati mbaya mimi sijui kabisa utaratibu uliopo. Ni vigumu leo kwa mfano Wilayani Ngara hakuna watumishi kwenye Tarafa nne zilizopo pale. Vijiji vingi havina watumishi, Kata nyingi hazina watumishi. Sasa huwezi kutegemea kwamba utafanya kazi ya kilimo wakati huna utaalam na ni lazima tukubali kwamba utaalam unatokana na wataalam waliopita vyuoni, wataalam ambao wanaweza wakaonyesha mifano ambayo sasa kwa Tanzania nafikiri kwa jumla hawapo na hawatoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara inalazimika kuhakikisha kwamba ina watumishi. Kuna suala la utafiti. Utafiti katika Tanzania umekuwa ni wakuweka makabrasha makabatini. Utafiti hauwafikii wakulima. Utafiti unapatikana lakini hakuna vitabu vinavyooandikwa. Zamani matokeo ya utafiti yalikuwa yakipelekwa katika Mikoa.

Kulikuwa na Maktaba katika Ofisi za Mikoa. Kulikuwa na sehemu ndogo katika Ofisi za Wilaya ambako matokeo ya utafiti yaliyokuwa yanaweza kupatikana watu wakayafahamu. *Extension Officers* wakayafikisha kwa wananchi kusudi wakulima waweze kuyatumia. Lakini leo tunachokipata ni taarifa za kila wakati.

Sasa kasoro zinajitokeza kwamba hakuna fedha zinazotosha kufanya kazi katika vituo vya Utafiti. Na hakuna mahali popote ambako kazi yoyote inaweza ikafanyika ikawa nzuri. Sio Wizara ya Kilimo na Chakula peke yake, ni kila Wizara haiwezi kufanya nzuri kama haina utafiti wa kina. Na utafiti wa kina unaofaa ni ule wa kupeleka madodoso kwa wale wanaohusika kwa maana ya walengwa.

Mheshimiwa Spika, siamini kwamba kuna kitu kinachoweza kikafanyika vizuri, kama kilimo cha kisasa. Lakini hatujatofautisha kati ya vitu hivi vitatu. Kuna kilimo kama kilimo, kuna kilimo cha mboga mboga *hortculture.* Lakini kuna kilimo cha mchanganyiko *mixed farming.* Kwa wakati huu imefika wakati kwamba kufanyike mabadiliko ya namna kusudi aina hizi tatu za kilimo katika nchi yetu zifanye kazi.

Mazingira yanakubali kabisa. Mazingira yanakubali, wasomi leo tunao, Chuo Kikuu cha Sokoine kinatoa kiasi cha kutosha cha utaalam. Hapa tu ndipo panaweza pakatuponya, kupata mazao ya muda mrefu, kupata mazao ya muda mfupi katika long *plan terms.* Tunaweza tukafanikiwa kwa kutumia kilimo hiki.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo ya kusema narudia tena kuunga mkono hoja hii. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha kutegemea mvua za msimu hakiwezi kutuondoa katika umaskini na njaa. Wizara itafute fedha hata kwa mkopo nafuu kuanzisha *Scheme* kubwa za umwagiliaji maji katika mito mikubwa kama Rufiji ili maji ya mito hii yasipotee bure kuingia baharini bila manufaa. Kama hii haliwezekani basi Wizara itafiti mabonde ya mito yafaayo kwa umwagiliaji tutangaze duniani, tualike mabepari wakubwa walete zana za kilimo, mtaji na kadhalika Tanzania tuwaandalie miundo mbinu (mifereji ya umwagiliaji na barabara) wakizalisha mahindi, ngano na kadhalika waweze kuuza popote duniani na tukipata njaa nao watuuzie kwa unafuu kwa fedha za hapa nchini. Hawa watalipa kodi nafuu na kuwaajiri Watanzania wengi.

Pia tunaweza kuwaalika nchi rafiki kama China walime katika mabonde haya kibiashara tusiwaingilie mradi tu wazalishe wauze popote mradi nchi iwasaidie katika miundombinu. Watanzania watagawiwa *plots* ndogo ndogo katika *scheme* hizi wapewe mikopo nafuu kupata mtaji, mbegu na zana wakizalisha mazao hayo yalipie mikopo.

Mheshimiwa Spika, naelewa hii ni *ambition* kubwa lakini lazima tufanye kitu, ebu jaribu kuuza mawazo hayo kwa wengine tusaidiane aibu ya kuomba chakula nje ni kitu kisichovumilika. Tuombe chakula kwa mbinu nyingine isiyo ya aibu ila ya kutuondolea umaskini.

Mheshimiwa Spika, madawa ya kuua wadudu ni biashara kichaa isiyoweza kutunusuru anzisha utafiti wa madawa ya asili kama mbegu za muarobaini itengenezwe kwa wingi tuue wadudu wote. Naelewa kuua biashara ya wakubwa duniani ina gharama usijali mradi utaokoa chakula cha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, zana za kisasa za kilimo ni ukombozi mwingine wa Watanzania. Kuendelea kutegemea jembe la mkono ni ndoto itakayotuendelezea umaskini na njaa. Matrekta yanayoingizwa nchini ukilinganisha na magari yanayoagizwa na Serikali nchini ni aibu. Jenga hoja ili tuanze kutafuta mikopo ya nje tuingize matrekta 10,000 kwa mwaka yaende katika kilimo matokeo utayaona. Kilimo kinatueletea fedha za nje 70% lakini kukipalilia kiendelezwe 4%-10% tutafika lini kwenye maendeleo?

Mheshimiwa Spika, fedha za kuanzisha Mabenki ya kilimo na uvuvi zipelekwe kwenye Wilaya ili ziwafikie walengwa wenye shida usizipeleke tena *Exim* isiyo na mtandao wowote.

Wilaya ya Sumbawanga tunalima mahindi, hatuna zao la biashara hivyo bodi ya mazao ya nafaka (mahindi, mtama na ngao) iundwe ili nasi tuone jinsi tutakavyojiendeleza. Wizara ya Kilimo itusaidie pia fedha kwa ajili ya barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, mbolea ipatikane mapema katika Mkoa wa Rukwa hususani Wilaya ya Sumbawanga ambapo msimu huanza mwezi wa *September* na *October* ukichelewa hapo mbolea haina manufaa na bei ishuke na pia zana za kisasa zianze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, Scheme ya umwagiliaji ya Katuka haipati fedha za kutosha itachelewa kumalizika. Naomba fedha nyingi zitolewe ili mradi huu ukamilike wananchi wanufike na scheme hii. Yapo maeneo ya Msanzi na Singiwe yakipatiwa fedha yakajengewa miundombinu ya umwagiliaji tutavuna chakula mara tatu au mbili, tupatiwe fedha.

Mheshimiwa Waziri tafuta ushauri kwa Wabunge kuhusu uboreshaji wa kilimo Tanzania utafanya maajabu katika nchi hii utalisha hata nchi zote jirani kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH E. MASHELLE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Kilimo na Chakula na Naibu wake kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mapendekezo na ushauri wangu. Kutokana na hali iliyojitokeza mwaka 2003/2004 kutokana na janga la njaa, nashauri Serikali itenge fedha za chakula za kutosha kwa ajili ya mwaka 2004/2005 kwani hali iliyojitokeza mwaka 2003/2004 ilikuwa ni mbaya sana. Mikoa mingi ilikosa chakula. Hivyo, Serikali iandae fedha za kutosha kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la pembejeo za kilimo. Wananchi wengi hawana zana za kisasa za kilimo mfano jembe la mkono linatumika tangu enzi ya mababu mpaka sasa na ninatumaini mpaka miaka inayokuja. Serikali sielewi inafikiri maendeleo ya kilimo yatakuwaje. Ili kuepuka suala la njaa ni lazima tuzingatie suala la zana za kisasa. Zana hizo zisambazwe mijini na hasa vijijini kwa wananchi wa chini kwa sababu nchi yetu wananchi wengi ni wakulima. Hivyo ni lazima Serikali isambaze zana hizi mfano matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali isambaze wataalam wa kilimo na ipange mipango na mikakati thabiti ya kupeleka wananchi wengi kwenye Vyuo vya Kilimo hasa vijijini ili waweze kupeleka vijijini kilimo cha kisasa kwa kutumia wataalam hao kwani vijiji vingi mpaka sasa hawajapata elimu hiyo ya kilimo cha kisasa. Vile vile Serikali

ihakikishe kunakuwepo na mipango thabiti ya kuendeleza kilimo cha kitaalam kulingana na mabadiliko yanayotokea duniani hasa ya sayansi na teknolojia na kuwezesha uwezo wa kushindana katika soko la dunia ili pamoja na faida nyingine vijana wengi ambao hawana ajira wajihusishe na kilimo badala tu ya kukaa au kuwa wazururaji, vibaka kutokana na kilimo.

Hii itasaidia kuwahamasisha vijana na wazee ambao wamepunguzwa kazi na wengine wamestaafu lakini hawataki kurudi vijijini kwa kukosa kazi za kufanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Aidha, nimpongeze Waziri wa Kilimo na Chakula kwa hotuba ambayo imeandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula ni Wizara muhimu sana kwa Taifa letu. Ni Wizara ambayo inaajiri karibu 80% ya Watanzania na inachangia wastani wa 40% ya pato la Taifa. Sasa ni takribani miaka 43 tangu kupata uhuru lakini bado kilimo chetu hakijaweza kumkomboa Mtanzania mnyonge. Hali hii imetokana na sababu kubwa kwamba Serikali hazijaweka mkazo wa kutosha kuwapatia wakulima nyenzo na miundombinu ya kutosha kuwawezesha Watanzania kuleta maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linarejesha nyuma maendeleo ya kilimo ni kilimo cha kutegemea mvua. Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ulimwenguni mvua sasa hazinyeshi kwa wakati na kwa misimu iliyozoeleka. Hali hii imepelekea mavuno ya shambani kuwa machache. Ili kuleta mapinduzi ya kilimo hapana budi sasa Serikali itilie mkazo kilimo cha umwagiliaji. Tanzania ina raslimali nyingi ya maji ya mito, maziwa na maji ya ardhini. Ni wajibu wa Serikali sasa kuandaa miundo mbinu itakayowezesha kutumia maji hayo kwa ajili ya kumwagilia mashambani. Tukiweza kufanya hivyo matokeo ya njaa Tanzania itakuwa ni hadithi tu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nchi yetu ilikumbwa na tatizo la njaa tukalazimika kutumia hatua za ziada kukabiliana na janga hilo. Lakini mwaka huu tumeambiwa kwamba hali ya mavuno haitokuwa mbaya kutokana na kupatikana kwa mvua katika sehemu nyingi za nchi. Lakini kumejitokeza tatizo kubwa katika jamii na hasa hapa Dodoma kutumia mavuno waliyoyapata kupikia pombe baadhi ya sehemu huuza ili wapate fedha kwa ajili ya kucheza ngoma za jando, harusi na unyago.

Mheshimiwa Spika, hali hii ikiachwa kuendelea na wananchi wakashindwa kuweka akiba ya chakula njaa itakuwa haiondoki. Ninashauri Serikali kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba chakula kinachopatikana kinatumika kwa uangalifu. Kadhalika Serikali itenge fedha za kutosha kununua chakula cha ziada na kukihifadhi kwa matumizi ya baadaye *(SGR).*

Mheshimiwa Spika, hivi leo asubuhi Bungeni wakati Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula anajibu swali Na.131 la Mheshimiwa Masoud A. Salim alikiri kwamba uzalishaji wa sukari nchini umeongezeka baada ya viwanda vya sukari kubinafsishwa.

Pamoja na kuongeza kwa uzalishaji wa sukari inakuwaje leo bei ya sukari imepanda kufikia Sh.800-1,000 kwa kilo moja? Tunaiomba Serikali itupatie maelezo kuhusu tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo machache, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, natoa rambirambi kwa wananchi na wapiga kura wote waliompoteza Mbunge wao, Mheshimiwa Yete Sintemle Mwalyeto. Mungu ailaze pema roho ya marehemu, *amin.* Pia natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliofikwa na majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia yafuatayo lakini kwa kifupi kabisa:-

Mheshimiwa Spika, sheria zote zinazosimamiwa na Wizara hii zitafsiriwe katika lugha ya Kiswahili kama kweli tunalenga zitumiwe na wakulima wetu. Haja ya tasfiri hizo ni kubwa sana na ushahidi ni jinsi tasfiri (isiyo rasmi) niliyofanya kwa baadhi ya vifungu vya Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2001 ilivyopokelewa na kufanyiwa kazi kikamilifu kwani wakulima walielewa mara moja mahitaji/maelekezo ya sheria hiyo. Mafanikio makubwa ya kilimo cha tumbaku katika msimu huu ni ushahidi. Ubabaishaji au kubabaishwa kwa wakulima kulikokuwa kukifanywa na wateuzi na/au wawakilishi wa makampuni katika masoko sasa umepunguza kwa kiwango kikubwa sana na wakulima wanaridhika na bei wanazopata sokoni.

Napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa wakulima wa tumbaku katika Jimbo langu na Mkoa wa Tabora kwa ujumla kwa mafanikio makubwa sana waliyoyapata katika msimu huu. Hakika zao hili pekee ndilo linaloendelea kukua na kupanua vipato vya wanaojishulisha nalo na Taifa kwa ujumla. Kwa kuwa sasa Serikali imeanza kuwa na mipango ya upendeleo maalum katika maeneo na mazao yenye matumaini makubwa, napendekeza hilo pia lifanyike kwa zao la tumbaku. Tatizo kubwa hapa ni pembejeo zilizo aghali sana kiasi cha kudhoofisha mapato ya wakulima hasa wale wadogo wadogo. Jitihada hizi tuzione.

Lakini pia mbali ya kupunguziwa mzigo huo wa pembejeo ni vyema na ni busara wakulima hawa wadogo wakasaidiwa katika nyenzo ambazo zitawasaidia katika kupanua kilimo chao kwa kuondokana na nyenzo hafifu. Hapa napenda kuipongeza Serikali kwa kutoa sera ya uwezeshaji wa wananchi. Natumai wakulima wataingizwa kwa mstari wa mbele kabisa katika mkakati wa awali wa sera hii.

Mheshimiwa Spika, kuingizwa kwa Wilaya yangu ya Uyui katika Mpango wa *PADEP* ni ishara njema kwetu. Napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri kutupatia maelezo ya kina katika maandishi ili tupate nafasi ya kuelewa vilivyo mradi huu na jinsi tutakavyofaidika nao. Yawezekana nasi tukawasaidia katika kuuboresha na kuuelekeza zaidi katika kutatua matatizo *specific* katika maeneo yetu badala ya kuwa *genetic.*

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Spika, mimi sina pingamizi sana na hotuba hii ila nina mashaka na utekelezaji wa baadhi ya miradi iliyopangwa kutokana na fedha chache ambazo Wizara imepangiwa. Wizara ya Kilimo na Chakula ni moja kati ya Wizara muhimu na tegemeo la Tanzania. Kwa hiyo, Wizara kupewa Tsh.64,074,053,600 ambapo kati ya hizo Sh.29,097,441,500 ni kwa ajili ya Maendeleo, hakuna nchi kubwa duniani ambayo inapangiwa Sh.29,097,441,500 na ukasema hizo ni kwa ajili ya maendeleo na maendeleo yake yakaonekana na ya kuringia eneo hili linanipa mashaka kuona na kusema kuwa fedha hii ya maendeleo ni ndogo sana sana.

Ushauri wangu ili niondoe wasiwasi wangu Wizara iongezewe fedha ya dharura baada ya kupata fedha ambazo zimeombwa ili Wizara iweze kufanya kazi yake vizuri kama ambavyo Wizara inategemea. Wizara tayari imeshajipangia miradi yake (mipango) inayolenga kuboresha kilimo. Pia fedha zitolewe kwa wakati ambao umepangwa ili zisicheleweshe kutekeleza miradi iliyopangwa. Ukizungumzia kilimo ni sawa na kugusa uhai wa wananchi na wananchi wenyewe tupo na tunahitaji uhai huo. Kuongezewa fedha Wizara hii ni pamoja na kupambana na ukame ambao unaweza kutokea kama ambavyo unatokea.

Mheshimiwa Spika, vituo vya utafiti wa mbegu bora na hii ni sehemu muhimu sana ambayo pia ina gharama yake na gharama hizo lazima zionekane kama mafanikio badala ya kuona ni gharama. Gharama ni upotevu na faida ni kuongeza kwa hiyo basi utafiti wa mbegu bora uwepo na masomo kwa watafifi yatolewe

Mheshimiwa Spika, pia miundombinu ni sehemu ya maendeleo kama vile barabara. Kwa hiyo kule ambako wananchi wanakuwa na mazao au ni wakulima basi ni vizuri kuwe na barabara ili mazao hayo yaweze kutoka kwa ajili ya kuuzwa au wafanyabiashara waweze kufuatilia mazao hayo ili wakulima wapate soko bora. Kutokuwa na barabara basi hata ukiwa na mazao yako sehemu moja au nyingine basi mazao hayo hayatapatikana kirahisi kwa hiyo husababisha chakula kupanda bila ya sababu yoyote.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina nia nzuri, Waziri wake pamoja na Naibu wake wako makini wanachosubiri sasa ni fedha tu wapewe ili tuone kama yaliyopangwa hayatatekelezeka. Bila ya fedha hayo yote yatakuwa bure na lawama zitazidi kunawiri. Leo Tanzania kukimbilia Ethiopia kununua chakula pamoja na kuwa tumenunua bado kwa Tanzania nchi yenye ardhi ya kutosha na yenye rutuba ya kutosha na mvua za kutosha basi ni aibu na matusi ambayo hayatasahaulika ila uwezo wa kufuta aibu hiyo upo na ni huo ambao nimeshausema wa kuwa Wizara iongezewe fedha.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kuona umuhimu wa kuendeleza kupandisha vyeo watumishi wake. Uwanja kama huu wa kupandisha vyeo watumishi ji jambo jema sana kwa kuwa pia hupandisha maslahi ya watumishi wake.

Kuhusu mashamba ya mkonge ambayo hayaendelezwi kama Waheshimiwa Wabunge ambavyo huuliza maswali kama vile Tanga na kadhalika basi mashamba hayo wanyang'anywe wamiliki hao na wapewe watu ambao wana uwezo wa kuyaendeleza.

Mungu Ibariki Tanzania.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nianze na kutoa salamu zangu za rambirambi kwa jamaa na marafiki wa Mheshimiwa Mwalyego na niombe Mola aiweke mahali pema peponi roho ya Marehemu Mwalyego, amin.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia katika maeneo mawili. Kwanza ni Mfuko wa Pembejeo wa Taifa. Hapa nimpongeze Mama Mariam, Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko huu anafanya kazi makini na kwa uangalifu mkubwa sana na bila woga na kwa uhakika mkubwa, nampongeza sana aendelee na umahiri huo.

Lakini nishauri Wizara kuwa *Exim Bank* wakopaji wengi wanailalamikia sana hasa kwenye Jimbo langu hawana imani na benki hii kuwa inatoa huduma ipasavyo, wana upendeleo hasa kwa Wahindi, ukiwa Mhindi utakuwa na uhakika wa kupata mkopo kwa urahisi na Wahindi nao hawasambazi pembejeo mikopo hiyo ni kwa ajili ya shughuli zingine za biashara zao. Mfuko haubagui kama nilivyosema hapo juu lakini unapofika *bank* kwa kisingizio cha dhamana hapo *Exim Bank* hujikamatia hapo katika harakati zao za upendeleo mimi nasema Benki hii haifai itafutwe *Bank* nyingine kama *NMB, CRDB* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, juu ya Serikali kutenga fedha au kuweka utaratibu wa ku-*support* pembejeo aina ya salfa inayotumika katika mikorosho ili bei isiwe kubwa kama inavyosaidiwa mbolea za chumvichumvi katika maeneo ya kuzalisha mahindi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala la umwagiliaji Serikali isiishie katika makaratasi tu ianze mara moja na ianzie Kusini maana mmezoea kila kitu kuanza Kaskazini Jimbo langu lina mabonde mawili mazuri bole la Kitere na la mto Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo. Wananchi wa Mbinga kwa ujumla na hasa wakazi wa Kata ya Maguu wanaishukuru sana Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kuwawezesha kufanikisha Sherehe za Siku ya Chakula Duniani iliyofanyika tarehe 16 Oktoba, 2004. Mchango wa Wizara wa kutoa mabomba ya maji umeiwezesha mji mdogo wa Maguu kuwa na uhakika wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na viongozi wengine wa Serikali walitembelea maeneo mengi ya kilimo pamoja na kukagua mitambo ya kumenyea kahawa, maswali mengi ya wananchi yaliweza kupata majibu.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya elimu au teknolojia haijaleta mapinduzi ya kilimo. Hakuna mahusiano yenye tija kati ya wasomi wa fani ya kilimo na wazalishaji wanaozalisha ambao wengi ni watu wasioenda shule. Wananchi wanaolima na ambao hawana elimu huwalisha wasomi. Hii ni aibu kwa wasomi kama elimu inayotolewa ni kwa ajili ya kuajiriwa badala ya kujiajiri. Nashauri mkazo utiliwe katika kuwaelimisha na kuwawezesha wakulima kupitia Shamba Darasa. Wizara ianzishe utaratibu wa kutoa zawadi kwa wakulima wanaofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma) waliitikia sana mwito wa Serikali wa kupanua kilimo lakini walikatishwa tamaa, pale ambapo mbolea ilichelewa kuwafikia pamoja na mbolea kuwa ghali. Nashauri Serikali itoe kalenda ya kusambaza mbolea ili ifike kwa wakulima mapema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya pembejeo, wakulima wa Mbinga wamenituma fedha hizo zipelekwe kwenye Benki ya Wananchi ya Mbinga kuanzia msimu huu ili waweze kupata mkopo wa kununulia mazao badala ya kwenda Songea kufuatilia mikopo *CRDB.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji hapa nchini kwanza Serikali ianze kujenga tabia ya kuthubutu. Wakulima wa sehemu za milima tayari wanajadi ya kilimo cha kiangazi. Nashauri Serikali iwasaidie hasa pale ambapo wenyewe wanajitahidi. Wakulima wa kahawa watafaidika sana endapo Wizara itawachangia angalau maboma ya maji kwa kutumia *gravity* na *drip irrigation.*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri angalau vituo vyetu vya utafiti viwe vielelezo vya tija. Kwa mfano pale Ugano, taasisi hiyo bado inatumia mfereji wa asili na hivyo maji mengi kupotea. Hivi ni kweli Serikali inashindwa kuleta maji ya bomba na kumwagilia kwa kutumia *drip irrigation* hata katika kituo cha utafiti kinachosimamiwa na Serikali?

Mwisho, ningependa kufahamishwa kuhusu maombi ya Wilaya ya Mbinga ya fedha za kujenga mitambo ya kukoboa kahawa.

Mhimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SIJAMINI MOHAMMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa heshima na taadhima nianze kwa kutoa mkono wa Tahania kwa kifo cha ghafla cha Mbunge wetu wa Mbeya Vijijini ambacho kimeacha pengo kubwa huko Mbeya na hata humu Bungeni.

Baada ya salamu za pole na mimi niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake na Wasaidizi wao kwa ushirikiano mzuri na kutuletea hotuba hii nzuri sana iliyojaa ukweli ambo unalenga sera ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema kuwa, maskini hapendi mwema, kwani mimi siamini kuwa mfumo wetu wa kilimo utaweza kubadili uzalishaji wa kilimo chetu bila ya kuwa na mchango mzuri wa kutumia fedha ambazo hatunazo. Mimi kwa hakika huwa ninapatwa na mshangao kutoka kwa wenzetu wa Upinzani kwa kutoa *criticism* ambazo haziko *constructive* ila wao wanatumia *destructive suggestions* kwani siyo kweli kuwa Tanzania iwe inalingana na Misri au Marekani. Tanzania sasa ina umri wa miaka arobaini tu kinyume na hao tunaolinganishwa nao.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama Serikali yetu inapenda kuomba chakula wakati tunayo ardhi nzuri na kubwa sana ila kumbe tungefanya miujiza gani kuleta mvua ambayo hatunayo? Aidha, hizo fedha ambazo hatunazo tungezipata wapi kuanza kufanya *irrigation?* Nasema matatizo yetu ni matokeo ambayo yako juu ya uwezo wetu kwani yanatokana na Jaala ya Mungu. Mimi sijakata tamaa na mwenendo ambao tunakwenda nao katika kuelekea kwenye kumwagilia hasa kwa kuwa Wabunge wetu wote wanahimiza umwagiliaji hasa kwa kuwa Tanzania nayo ni nchi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, siyo sahihi kuiambia Wizara itafute fedha za kutosha kuhakikisha tunakuwa na kilimo cha umwagiliaji na ununuzi wa mbolea ya kutosha kwa watu wote. Hatuwezi kutegemea wahisani kutusaidia tupate fedha hizo za kutosha kwa mara moja kwani hawa wahisani hutoa misaada kutokana na matakwa yao wenyewe wala sio kulingana na shida zetu sisi.

Mheshimiwa Spika, njaa inapopatikana huku Tanzania Bara inakuwa tatizo kubwa kule Zanzibar kulingana na tatizo la ardhi kule Pemba na Unguja. Mazao ya kilimo huku Tanzania ndio mkombozi kwa wananchi pamoja na kuimarishwa kwa uchumi kule visiwani. Aidha, ninashauri kwa nguvu zaidi Wizara hizi ziwe karibu zaidi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara na wawe wanashauriana kwa juhudi kubwa kujua hizi ni Wizara muhimu kwa kuweza kusaidia Tanzania nzima. Hili wazo siyo geni kwani hapo zamani wakati wa utawala wa Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi (aliyekuwa Rais wa Zanzibar) alikuwa akihimiza sana wakulima wa milimani (NGORO) huku Tanzania Bara na watu wetu wengi kutoka Pemba walikuwa wakija kusoma Bara.

Mheshimiwa Spika, bado tunaamini kuwa kilimo ni uti wa mgongo kwa uchumi wa nchi hii kwa maisha ya wananchi siyo wakulima tu bali hata sisi walaji ambao hatulimi. Kwa umuhimu huu bado tunahitaji miundombinu mizuri inayoweza kuibua mbinu za kukuza kilimo nchini au nchi zetu mbili, Zanzibar na Tanzania Bara. Tusichoke kutembeleana na kuwapeleka wataalam wetu kwenda kuwaona wataalam wa nje kuona na kusoma na kupata taaluma ambayo wenzetu wanayo. Mfano mzuri ni ule Waheshimiwa Wabunge wetu kwenda kutembelea na pengine popote duniani wanakotegemea kilimo cha mvua na umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu ni la wakulima wazuri kule Unguja na wanategemea sana kilimo na uvuvi na kwa kuwa lazima tupate nguvu ya kulima, basi mimi kwa niaba ya wapinga kura wa Kitope tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Naomba tumpe Mheshimiwa Keenja fedha zote akafanye kazi kutuletea chakula na tuikimbie njaa.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam na wasaidizi wengine wote kwa hotuba nzuri. Hata hivyo, nina maombi yafuatayo kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ombi la kwanza linahusu kilimo cha umwagiliaji maji bonde la Lundo. Mbinga ina mabonde mengi kama Lundo, Lituhi, Luhekei, Chiulu, Chiwanda na mengineyo. Mnamo mwezi Machi, 2004 nilimuona Mheshimiwa Naibu Waziri pia Mkurugenzi wa Umwagiliaji Maji Mashamba kwa wakati tofauti na niliahidiwa kuwa walau bonde la Lundo litaingizwa katika mradi wa umwagiliaji maji mwaka 2004/2005 lakini ahadi hii yao kwangu nimechunguza ndani ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona mahali popote bali iko kimya. Mheshimiwa Waziri hili jambo halieleweki, wananchi wa Wilaya ya Mbinga kwa muda wa miaka minne wanakuwa watazamaji tu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri bonde la Lundo liingizwe katika miradi ya mwaka 2004/2005 kama nilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, la pili, Wilaya ya Mbinga vile vile tunaomba miradi ya majosho. Ni ukweli usiopingika kuwa Wilaya ya Mbinga inaongoza kwa kuwa na ng'ombe wengi kwa Mkoa wa Ruvuma. Ingawa Wilaya ina ng'ombe wengi hata hivyo mwaka 2003/2004 haikupata miradi ya majosho. Tunaomba sana tukifiriwe kupewa katika mwaka wa 2004/2005. Ingefaa miradi isambazwe sawa sawa ndani ya Mkoa badala ya kuijaza miradi sehemu moja. Hali hii ikiendelea haitaleta uwiano wa maendeleo ndani ya Mkoa na ndani ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mbinga tuna miti mingi mikubwa ya korosho na kwa bahati mbaya wakulima hawana uwezo kabisa wa kununua *sulphur.* Ingefaa sana Wizara ingewasaidia wakulima wa korosho Wilaya ya Mbinga kwa lengo la kuwajengea uwezo hivyo tunahitaji *sulphur.*

Mheshimiwa Spika, katika jedwali Na.4 inaonyesha Mabenki yaliyopewa fedha na Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, jumla ya shilingi bilioni 5.4 kuanzia msimu wa 2002/2003 hadi tarehe 31 mwezi wa Mei, 2004 lakini Benki ya Wananchi Mbinga haikupewa. Tunaomba kwa mwaka 2004/2005 Benki ya Wananchi Mbinga, nayo ipewe fedha kutoka Mfuko huo wa Pembejeo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana maombi yangu ya hapo juu Mheshimiwa Waziri ayape uzito wa kipekee na kuyakubali.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi na mimi mwenyewe binafsi naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. OMAR R. MAPURI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Wizara ya Kilimo na Chakula kwa jitihada zake inazofanya kumwendeleza mkulima katika mazingira magumu.

Eneo mahsusi ambalo napenda kuchangia ni lile la uvumbuzi wa mbegu mpya bora za mazao mbalimbali ya chakula na ya biashara. Kazi nzuri sana inafanyika katika eneo hili. Tatizo ambalo bado nahisi linahitaji kufanyiwa kazi kwa msukumo zaidi ni kuzifikisha mbegu hizo kwa wakulima na kuwathibitishia ubora wa mbegu hizo. Kazi hiyo inaweza kufanywa kwa ufanisi zaidi kwa kutumia mashamba ya mfano yaliyo karibu na wakulima, mashamba kama hayo yanaweza kutumika pia kuzalisha mbegu hizo na kuzisambaza kwa wakulima. Mashamba ya mfano ya Wizara pekee hayatoshi kwani ni machache na yako mbali na wakulima wengi.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri Wizara iwashawishi na kutoa utaalam wakulima wengi zaidi kuanzisha mashamba ya mifano yatakayotumia mbegu mpya zinazovumbuliwa. Pengine ingefaa pia Wizara ikawa na utaratibu mahsusi wa kuwatumia viongozi hasa Waheshimiwa Wabunge kwa sharti tu kwamba shamba la Mbunge ambalo litatumika kuendelezwa kama la mfano liwe ndani ya Jimbo lake. Kwa wasiokuwa na Majimbo yanaweza kuwekwa masharti mengine yatakayohakikisha kwamba mkulima kijijini anafaidika na utaalam kutokana na shamba hilo la mfano. Aidha mnaweza kuongeza ushirikiano na Jeshi la Magereza ili kuutumia vyema zaidi mtandao wao katika suala la mashamba ya mfano kwa mbegu mpya.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri aunde vikundi vya ushirika vya wataalamu kutoka wahitimu wa Vyuo vyetu nchini mfano Chuo cha Kilimo Sokoine, Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo cha Maji Dar es Salaam ambao wana utaalam kidogo wa umwagiliaji. Kisha Waziri awapatie vifaa kamili vya kilimo cha kisasa, Mbolea, dawa na mbegu bora. Baadaye wakabidhiwe moja kati ya mabonde yetu, kampuni hiyo iwe ni yao binafsi, nina hakika wataalam hawa watafanya kazi nzuri ambayo watapata fedha za kulipia vifaa ambavyo wamekopa na faida mbili Taifa litapata. Moja watakuwa wameumbiwa ajira. Pili chakula ambacho kitapatikana katika mradi huu kitasaidia kuongeza pato na chakula kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, vikampuni kama hivi viwe vingi kadri ya uwezo wa Taifa na hapa tutakuwa tumepiga hatua kiasi fulani na kwa zile sehemu ambazo hazina mabonde yenye maziwa na mito yenye maji ya kutosha mfano Mwanza, Shinyanga na Tabora basi Serikali ifanye mradi wa makusudi wa gharama ya kuyavuta maji ya Ziwa Victoria kwa wingi kwa ajili ya kumwagilia mashamba ya ushirika ya maeneo hayo. Kama ambavyo Serikali imeanza kujaribu kuyavuta maji ya Victoria kwa Mikoa hiyo kwa ajili ya matumizi ya binadamu, naipongeza sana Serikali kwa mradi huu pamoja na wafadhili pia tusichoke kuwaomba wafadhili wakuu wa dunia wale ambao walituambia ili uchumi wetu utengemae tubinafsishe kila kitu na kwa bahati nzuri kilichobaki katika kubinafisha ni wake zetu tu na uchumi bado kwa muono kwa kawaida unazidi kudumaa wanaweza kutusaidia kuvuta maji haya ya Victoria. Ingawa kuna mkataba wa pamoja wa kutumia maji ya Ziwa Victoria lakini tumuulize Waziri Lowassa huko Misri na Sudan Waarabu

wanaolima kwenye majangwa maji ya kumwagilia wanayatengeneza kwenye maabara gani tujue au ni haya haya yanayotiririka kwenye Mto Nile kutoka Victoria. Hili linawezekana naomba litimizwe na tutaona faida yake.

Mheshimiwa Spika, zaidi namwomba Waziri aangalie namna ya kutunza mazao ya wakulima na kuyatafutia soko. Kuhusu kuwa na viwanda vya kusindika baadhi ya mazao ambayo ni mengi na ni ya msimu ni la maana lakini ni gharama na Serikali haina uwezo. Huaje machungwa Muheza elfu kwa shilingi mia na Dodoma chungwa hilo hilo moja ni shilingi mia, Kibaha mananasi fungu shilingi mia tano Dodoma moja shilingi elfu. Huu ni mfano tu ambapo mazao eneo moja la nchi yanapotea na sehemu nyingine ni adimu na ghali, hebu Mheshimiwa Waziri tumia wataalam wako kuondoa dhiki hizi, usiwavunje moyo wazalishaji kwa bei na wengine wasiumie kwa bei.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Waziri kutoa taarifa kwamba ule mpango wa kugawa mazao mawili kwa Mkoa ameuondoa, mpango huu ungeturudisha nyuma sana.

Hatuna uhakika wa mvua na kila zao lina uwezo wake wa kukabili ukame yakiwa mazao mengi likiharibika hili, hili linamsaidia kama ni moja ndio basi tena. Wahenga wamesema: ‘mitego mingi harabu ya mnyama’ nampongeza tena Waziri kwa uamuzi huu.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki, naomba kuunga mkono hoja.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya, hasa kusimamia sera za CCM katika kilimo na chakula.

Tatizo langu ni katika Jimbo langu, sina mradi wowote wa umwagiliaji maji. Kuna bonde zuri, pana, kubwa, ambalo wananchi kwa kilimo chao cha kawaida kila mwaka wanavuna mpunga mwezi *May* na kuanza kilimo cha kiangazi *June* na huvuna mahindi, viazi, maharagwe kwa kiwango kikubwa lakini ni ulimaji wa kienyeji. Bonde hio linaitwa Bonde la Ruaha, yapo maji yanayoingia katika Bonde hilo kutoka Mito Tyka Kituti, Mgolo, Mbalaganga, Isyaga, Chirombola, Euga, Libenanga na kadhalika.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri, utume wataalam wako kuona ukubwa wa bonde hilo na uwezekano wa kuanzisha mradi mkubwa wa umwagiliaji. Sisitizo hili liko katika ukurasa wa 74 wa hotuba yako Kifungu 168. Naomba wataalam watakaotumwa wasikose kunishirikisha angalau kimawazo au kuona kwa pamoja eneo husika.

Mheshimiwa Spika. naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii kwa kuandaa Bajeti yenye ufafanuzi wa kina katika vipengele kadhaa.

Mheshimiwa Spika, pia natoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Mwalyego, kwa kuondokewa na mpendwa wao huyu. Niwatake kuwa na subira katika kipindi hiki cha majonzi na Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo. Ukurasa wa 24 na 72 kilimo cha umwagiliaji mashamba katika mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji maji nashauri kuwa kwa vile fedha zilizotengwa kwa Wizara bado ni ndogo ingefaa kwa mabonde yaliyoainishwa tufanye uamuzi makini wa makusudi wa kuendeleza mabonde mawili tu kama kianzio kwa fedha za mwaka huu ili ifikapo mwakani tuone dhahiri kilichofanyika. Hii ina maana tuendeleze miundombinu yote katika mabonde hayo ipasavyo.

Pili kuhusu suala la watumishi wa Wizara hii. Pamoja na kwamba watumishi hawatoshelezi hata hao wachache hasa wale waliopo vijijini wana matatizo ya vyombo vya usafiri kama pikipiki ili waweze kutekeleza shughuli za kilimo kwa wakulima.

Tatu ni vema sasa matokeo ya utafiti yote yasambazwe kwa wananchi hasa wakulima kwenye maeneo ambayo matokeo hayo yanafaa kutekelezwa/au kutumiwa.

Mheshimiwa Spika, ni kwa kipindi kirefu sasa tangu suala la uvunaji wa maji ya mvua kama teknolojia linazungumzwa humu Bungeni lakini teknolojia hii bado haijasambazwa kwa wananchi ingawa ni njia mojawapo ambayo ingesaidia sana kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji mashamba badala ya kutegemea mvua ambayo maji yake yanaweza kupotea bure.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri huo, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii, hata hivyo, ninao ushauri ufuatao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu skimu za kilimo cha umwagiliaji chini ya *PIDP.* Mpango wa *PIDP* ambao unalenga kueneza *scheme* za kilimo cha umwagiliaji unatekelezwa katika Wilaya nyingi pamoja na Wilaya yangu ya Manyoni. Mpango huu ni wa muhimu sana na nimetiwa moyo kwamba Bajeti hii inauendeleza. Kitu kinachokosekana katika mpango huu *(missing link)* hasa katika Wilaya ya Manyoni ni kukosekana kwa mabwawa *(dams)* kama vianzio vya maji ya umwagiliaji. Mpango jinsi ulivyo sasa unategemea maji ya mvua bila kuvuna na kuhifadhi maji ya ziada ili yatumiwe na wakulima kumwagilia mashamba nyakati mvua hakuna. Ushauri ni kwamba inafaa skimu zote za umwagiliaji ziwe na *component* ya bwawa moja kama mbinu ya kuongeza mavuno ya mkulima kupitia umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa uwezeshaji wakulima. Huu nao ni mpango mwingine wenye umuhimu mkubwa sana katika kuendeleza kilimo na wakulima nchini. Lakini mpango bado haujaenea katika Wilaya zote. Hii ni dosari kubwa. Mwakani iwekwe mikakati ya kueneza mpango huu katika Wilaya zetu zote. Wakulima wanahitaji

kuwezeshwa kupata pembejeo kwa bei nafuu na elimu juu ya kilimo bora *(extension services)* iwafuate huko huko waliko vijijini.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya watumishi. Wizara hii kwa miaka mingi imekuwa inalalamikiwa sana na watumishi wake kuhusu kupandishwa vyeo, kupata mafunzo, kurekebishiwa mishahara na kadhalika. Hivi sasa juhudi kubwa imefanywa kupunguza malalamiko haya, pongezi. Hata hivyo, bado malalamiko/manung'uniko hayajamalizika. Hivyo juhudi za sasa za kuwaendeleza watumishi wa Wizara hii ziendelezwe ili kujenga kada ya watumishi wenye ari na ufanisi wa kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na mipango mizuri ya utekelezaji iliyobainishwa. Hata hivyo, mchango wangu utajihusisha na uzoefu uliojitokeza katika utekelezaji.

Taarifa za mapungufu ya utekelezaji kwenye ruzuku ya usafirishaji wa mbolea uzingatiwe. Tatizo la mbolea ya ruzuku lisitazamwe kwa ujumla jumla tu, hapana, matatizo ya Wilaya ya Iringa Vijijini tofauti na mazingira yaliyopo katika Wilaya ya Ludewa hivyo kutoa ruzuku ya usafirishaji wa mbolea hadi Makambako kituo kilichopo km.220 hadi Ludewa hutawasaidia wakulima wa Ludewa hadi mwisho wa dunia hii gharama za usafirishaji zitaendelea kupandisha bei ya Mbolea. Kama mwaka 2003 wakulima wa Makambako waliuziwa mbolea kwa bei ya Sh.14,500 lakini wale wakulima wa Ludewa bei zilikuwa kati ya Tsh.20,000 hadi 25,0000 kwa mfuko moja. Nashauri Wilaya ya Ludewa ipewa unafuu maalum wa kufikishiwa ruzuku ya mbolea hadi Wilayani Ludewa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuliongezea Shirika la Hifadhi ya Chakula *(SGR)* fedha za kununua mahindi. Tunashauri Shirika hili kuanza kununua mahindi mapema inavyowezekana halikadhalika kwa Wilaya kama Ludewa kuongeza *buying post* katika maeneo ya Malangali, Lugarawa, Mavanga, Maweregi, Luana na Ludewa Mjini. Maeneo hayo yote yana maghala mazuri ya kutosha kwa ajili ya kuhifadhi mazao.

Mheshimiwa Spika, maelezo mengine nilikwishayatoa wakati nachangia katika hotuba ya Waziri wa Fedha, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia japo kwa maandishi, hotuba hii ya bajeti ya Wizara hii ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, tunalima ili tupate chakula na chakula ni uhai. Tulime tulimavyo lakini kama Maafisa Kilimo/Mabwana Shamba hawaendi vijijini kuelimisha wakulima kilimo bora, Wizara itakuwa inafanya kazi bure, ni lawama tupu.

Mheshimiwa Spika, kwa kilimo cha kahawa kalamu ya Bwana Shamba ni mkasi wa kuchambulia matawi ya kahawa ili kahawa izae kahawa bora. Mabwana Shamba kalamu hii mkasi hawana kabisa. Hawatembelii wakulima wa kahawa. Wakulima wanakatia matawi kwa utashi wao tu. Mabwana Shamba hawana daftari/*counter book* ya kuweka record ya hata mkulima mmoja waliomfundisha uchambuaji matawi ya kahawa. Toka Januari hadi Desemba hawafanyi lolote. Wako Mkoani, Wilayani na kwenye Kata. Wanapata mshahara kila mwisho wa mwezi na wanapandishwa vyeo kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa kilimo na Chakula ukurasa wa 49(xvi)-114-5.

Mheshimiwa Spika, rejea ukurasa wa 58(135) kuhusu fedha za *STABEX.* Hizi fedha ni kidogo sana Sh.42bl toka *European Union* zimetapanywa mno kama inavyoonekana katika kifungu 135(c) (i-viii) (d) na (e) swali:-

(1) *Euro 6,308,693* zitapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya?

(2) Uboreshaji wa kahawa *Euro 2,500,000 Central pulparies* za Serikali, watu binafsi au Ushirika? Watakopeshwa au watepewa bure? Halafu iweje kama si ulaji tu?

(3) *Euro 2,661,307* - sensa ya kilimo. Huu ni ulaghai mtupu. Bajeti 2004/2005 ifanye nini?

(4) *Euro 450,000* - kurekebisha mifumo ya bodi. Acha hiyo peleka fedha hizo *TANROAD.* nchi yetu. Sikio la kufa halisikii dawa. Waziri afanye atakavyo, IMEKITHIRI.

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote kwa pamoja kwa jinsi walivyoonyesha umahiri wao mkubwa na wa pekee kwa namna walivyoiandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kilimo kama ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu Serikali haina budi kukipa umuhimu mkubwa zaidi na wa pekee katika Bajeti yake kuliko Wizara nyingine yoyote. Kwa kweli Serikali bado haijatoa umuhimu unaostahili kwa sekta kubwa kama hii inayowagusa 80% ya Watanzania katika maisha yao ya kila siku. Bajeti ya Sh.64,074,053,600 kwa sekta kubwa kama hii ni dhahiri kwamba fedha hizi ni kidogo mno na haziwezi kuleta mabadiliko yanayostahili kwa wakulima wadogo wadogo walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, baya zaidi na la kusikitisha ni kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo Sh. 29,097,441,500 ni kidogo sana na miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa kipindi hiki cha 2004/2005 itakuwa haitekelezeki. Zaidi Sh.6,436,433,200 ndio fedha za ndani sawa na 22.12% na Sh.22,661,008,300 ni fedha za nje sawa na 77.88% je ni kweli miradi hiyo 12 ya maendeleo itatekelezeka chini ya utegemezi huu mkubwa?

Hiki ni kiini macho na ni ndoto ya mchana kwani wahisani/wafadhili hawatoi fedha mnazoziomba kwa wakati unaostahili kulingana na matakwa ya Serikali. Hii ni kasoro na dosari kubwa. Ninaishauri Serikali itafute namna yoyote ya kitaalam kuweza kupunguza japo kwa 50% utegemezi wa fedha za nje kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kukipa umuhimu wa pekee kilimo cha umwagiliaji maji ili kuweza kupambana na umaskini kwa vitendo kwani nchi yetu ina mabonde mengi yenye maji ya kutosha na rutuba. Kwa mfano Mkoa wa Morogoro una mito 175 isiyokauka hivyo kwa wastani chini 10% ya mabonde ya Tanzania nzima ndio hutumika kwa kilimo cha umwagiliaji maji, dosari hii inapaswa iondolewe.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kupanga mikakati madhubuti ya kupambana na watu wanaopelekea kutoweka kwa vyanzo vya maji. Kuna watu wengi vijijini wanakata miti hovyo bila kufuata taratibu na hasa wale wanaokata miti kwa uchomaji wa mkaa. Lakini la kushangaza Watendaji wa Vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya wanashuhudia uovu huo lakini hawakemei kulikoni?

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuwachukulia hatua wale wote wanaosababisha ukame na jangwa kwa makusudi kwa tamaa binafsi wachukuliwe hatua za kisheria mara moja na pia ninaishauri Serikali kuwafukuza kazi mara moja watendaji wote kuanzia vijiji hadi Mkoa ambao hawakemei ukataji miti ovyo hasa katika vyanzo vya maji kwani maji yanaendelea kutoweka kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali itilie mkazo juu ya namna bora ya uvunaji wa maji ya mvua ili yasipotee ovyo kwani elimu ikitolewa vizuri kwa wakulima ni dhahiri kwamba maji hayo yataleta mabadiliko makubwa katika kilimo na wananchi kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kwa nguvu moja wakapeleke kwa haraka mbolea katika Wilaya ambazo mwaka 2003/2004 hawakupata.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kupitia *TOSCA* kuweza kudhibiti mbegu mbovu zinazoingizwa nchini isivyo halali kwani mbegu hizo zinazorotesha maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuruhusu kulimwa kwa zao la pamba Mikoa ya Kusini mwa nchi yetu katika hali ya kupambana na umaskini kwani kama tangu 1942 alipoonekana funza mwekundu *(red bollworm)* na hatimaye kilimo hicho kupigwa marufuku katika miaka ya 1990 je, kuna utafiti wowote uliofanywa katika kipindi hiki ukaonyesha kuwa mdudu huyo bado yupo au la?

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kwani mdudu huyo katika nchi alikotokea kama vile Msumbiji, Malawi, Zambia, Zimbabwe na Afrika Kusini wanalima pamba licha ya kuwepo kwa mdudu huyo funza mwekundu na badala yake wanatumia viuatilifu kumdhibiti funza huyo. Hivyo ni vema Serikali ikafanya utafiti wa kina na

kusaidiana na *TPRI,* Arusha kuangalia namna bora ya kuruhusu pamba kulimwa Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo cha maua ni biashara muhimu sana katika Mataifa yaliyoendelea na kwa vile kilimo hiki kinaingizia fedha za kigeni Serikali kama kule Arusha, *Tengeru Flowers* hivyo ninaishauri Serikali ikaandaa mkakati maalum wa kuboresha kilimo hiki cha biashara kwa Mikoa mbalimbali na hasa Dodoma katika kasi ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, imebainika kutokea kwa vifo vingi miongoni mwa wataalam wa Wizara hii jambo ambalo ni pengo kubwa kwa Taifa. Hivyo kwa vile imedhihirika wataalam hufariki kwa ugonjwa wa UKIMWI na mara nyingi huambukizwa virusi wanapokuwa safari nje ya maeneo yao ya kazi na wana ndoa wao hivyo ninaishauri Serikali kuwaruhusu na kuwagharamia wataalam kuchukua wana ndoa wao pale Serikali inapowapangia majukumu ya kazi nje ya mahali pa kawaida pa kazi zao. Hii itasaidia kupunguza maambukizo na vifo vya wataalam wetu kwa gonjwa la UKIMWI.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na kukupa pole wewe mwenyewe, familia ya Hayati Mheshimiwa Mwalyego, pamoja na wananchi wa Mbeya Vijiji, kwa kumpoteza Mbunge wao. Namwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, pili naomba niunge mkono hoja hii mia kwa mia kabla sijasahau kuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba naishauri Serikali ni vipi iboreshe kilimo ili wananchi wanufaike na kilimo cha uhakika.

(1) Serikali isijitoe kabisa katika suala la kununua matrekta na kuyapeleka kwenye Halmashauri ili yaweze kukodiwa na wananchi ili walimie. Hii itasaidia kupanua kilimo na kupata mavuno ya kutosha.

(2) Pamoja na uwezo na kazi nzuri iliyofanywa ya kutoa fedha za kutengeneza miradi ya umwagiliaji ambayo baadhi ya mingine itakuwa imekamilika na mingine haijakamilika hata iliyokamilika bado haikidhi mahitaji ya maeneo hayo. Naishauri Serikali iwe na miradi michache ya kila mwaka ili fedha nyingi zitumike kutengeneza miradi mikubwa kwa zamu kuliko ilivyo sasa. Vile vile watendaji watumie fedha za uendeshaji vizuri ili zizae matunda badala ya kulipana posho na miradi haiishi. Ni vizuri uzalendo uonekane katika suala la kudhibiti fedha.

(3) Naishauri Serikali kuweka mpango wa kuboresha kilimo kwa kundi maalum la wanawake kwa kuzingatia umuhimu wao katika kazi kubwa wanayofanya ya kushiriki

katika kilimo. Ni vizuri kuchimba mabwawa hasa katika maeneo ya Mbabala, Mpunguzi, Ihumwa, Pahi, Haubi, Nzali, Chalinze, Bahi na kadhalika na sio mabwawa tu bali hata visima vifupi.

(4) Serikali ingetoa maelekezo kila Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji kujiwekea akiba ya chakula hasa kwa kuanzisha Benki Kata. Utaratibu wa kuweka akiba ya chakula cha Taifa unachelewesha kugawa chakula kwa kigezo cha kukosa takwimu sahihi na huo sio utaratibu mzuri kwani wakiweka akiba wenyewe watakuwa na uhakika wa chakula na kila mtu atakitumia kwa uangalifu badala ya kutegemea akiba ya Taifa. Nashauri mpango wa akiba ya Taifa ufutwe na fedha zigawiwe kila Wilaya au Mikoa wanunue chakula cha akiba wenyewe na Taifa libaki kama Mdhibiti Mkuu badala ya Ofisi ya Waziri Mkuu kulaumiwa kwa suala la chakula. Ofisi ya Waziri Mkuu ipelekewe malalamiko ili iyasuluhishe badala ya hiyo ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri inayoleta matumaini, lakini kweli tutapatra hayo matumaini! Mbona Mabwana Shamba hawapo vijijini? Mbona wananchi wanaendelea kulima kama walivyozoea miaka nenda miaka rudi kwa jembe la mkono bila kutumia mbolea na sasa ardhi katika maeneo mengi imechoka?

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao mbadala. Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia (kuwafundisha) kilimo cha vanilla, zao ambalo lina bei kubwa kuliko kahawa, ingawa tunaambiwa imepanda kidogo sana baada ya Brazil na nchi nyingine kupigwa na barafu kali *(frost)?* Je, Wataalam wa Kilimo cha vanilla wapo? Nashauri mikakati ya wazi ielekezwe katika Wilaya maskini kama Ngara, ili waweze kupata zao la biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umwagiliaji. Kila mara tuna tunaambiwa kuwa kuna mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji. Mpango huo ni wa kusikika, kufikirika au kusadikika? Kwangu mimi ningepata imani kama miradi ya umwagiliaji ingeanzishwa katika mabonde ya Mto Ngono, kama vile Kajunguti, Nkenge, Kyaka, Kera na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja za Wabunge waliozungumza kwa uchungu kwamba wananchi hawapati manufaa kutokana na bajeti kubwa inayotengwa kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo natamka kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. TATU M. NZIMIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Natoa angalizo juu ya Mabwana Shamba wa Kata, Vijiji na Tarafa:-

(a) Utambulisho wa kazi zao, warudishiwe sare ili watambulike wawapo kazini na kuweza kudhibitiwa.

(b) Hawaendi kwa wakulima kutoa elimu ya kilimo kwa kudai hawana usafiri wa kuwafikia wananchi kwenye maeneo yao.

(c) Kama wao wanashindwa kuwatembelea kwenye maeneo, je, hata kuwaita kuwapa elimu katika vituo vyao vya kazi?

(d) Kwa uhakika Mabwana/Bibi Shamba hawa sidhani kama wana hadidu za rejea za kufanyia kazi, wanaonekana wapo wapo tu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara walione hilo litatuliwe ili wananchi watakapowaona Watendaji hao, wapewe heshima wanayostahili. Vinginevyo, wanaonekana kama ni wakazi tu wa vijijini badala ya kuwaWatendaji.*Output* na *inputs,* haviendi sawa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. GEPRGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji ni ukombozi na muhimu sana hasa katika kuondoa/kupunguza tatizo la njaa katika nchi yetu, ipo haja kubwa kwa Serikali kuwekeza/kuhakikisha mabonde yote iyanalipwa, yakiwemo mabonde ya Matomondo, Inzomvu, Lumuma, Malolo, Lufusi, Mbuga za Msagali (kilimo cha mpunga - upo mradi wa *PIDP*, Kijiji cha Msagala, Wilayani Mpwapwa.- Naishukuru sana Serikali). Mabonde haya yakilimwa, tutapata chakula cha kutosha na kuondoa njaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya chakula. Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kwamba maeneo yote yenye ukame na hawatapata mavuno ya kutosha, wapewe msaada wa chakula; na tathmini ifanyike katika maeneo yote ya Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazao ya biashara. Mkoa wa Dodoma, ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa, wanalima sana mazao ya biashara kama vile karanga, ufuta, alizeti na kadhalika, tatizo kubwa hakujna soko la kuuza mazao hayo. Pia ipo haja kubwa kwa Serikali kuunda Bodi ya Mazao mchanganyiko ili Bodi hiyo iweze kuboresha kilimo cha mazao hayo, hasa katika Wilaya ya Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma na maeneo yote yanayolima mazao hayo ya karanga, ufuta, alizeti, na kadhalika. Pia ipo haja kwa Serikali kuanzisha viwanda vya kukamua mafuta ya kula kwa kuwa tuna karanga, ufuta, alizeti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wananchi wanatumia mafuta ya kula yaliyoagizwa kutoka nje ya nchi. Nchi yetu ina uwezo wa kuanzisha viwanda vya kukamua mafuta ya kula hapa hapa nchini kwa kuwa mbegu za mafuta tunazo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia 100%.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake ambayo ina mipango mizuri sana kama timu yake itakuwa makini katika kufuatilia na kuona kama yaliyolengwa yanatekelezwa biola ya kuyaacha katika makaratasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, niungane na Watanzania wote wapenda maendeleo, kuishauri Wizaara ione umuhimu wa Wataalam wa Kilimo wanakuwepo angalau ngazi ya Kata ili wawe karibu na wakulima walioko vijijini, kuwapatia elimu. Sababu kilimo cha karne hii kinahitaji utaalam, kwani kwa sasa wakulima wanalima kilimo cha zamani ambacho kimepitwa na wakati. Pia ngazi za juu, Wataalam wasikae tu maofisini, waende mikoani hadi wilayani na ikiwezekana hadi kuangalia mashamba yanavyolimwa. Tukifanya hivyo, nina imani tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha trekta kipewe kipaumbe kwa Mtwara. Kilimo cha bondeni katika maeneo ya Mto Ruvuma, kinahitaji trekta, na kilimo hicho kikisimamiwa vizuri, uzalishaji wa hali ya juu utakuwepo.

Mheshimiwa Spika, utaalam wa kilimo cha umwagiliaji maji kianze Mkoa wa Mtwara kwa maeneo ya Mto Ruvuma. sawa na mikoa mingine. Matumaini yangu ni makubwa sana kwamba tukianzisha kilimo cha umwagiliaji maji Tanzania, tutajitosheleza kwa chakula na tutaondokana na aibu ya omba omba nchi za nje. Kila jambo linawezekana, timiza wajibu wako.

Mheshimiwa Spika, katika mkoa kuna upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo kutokana na jua kali. Mihogo ambayo ilipandwa ilikauka na jua. Hivyo wakati wa kuangalia mikoa yenye upungufu wa chakula, na Mkoa huu uangaliwe.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa jinsi ilivyojitahidi kugawa chakula mikoa iliyokubwa na njaa, ikiwemo na Mtwara. Ila wanavijiji ambao wameathirika kwa kula ugali wa mihogo yenye sumu, ilitokana na ukosefu wa mvua za kutosha. Serikali haijachukua hatua za kuwasaidia, kwani wamedumaa na tuseme wamelemaa, na ni hatua zipi kwa sasa Serimali inachukua kunusuru maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kabla ya msimu, iwe imeandaa kujua mambo muhimu kama malengo, pembeje - ikiwemo wataalam na mbolea zipi na ziwafikie wakulima kwa wakati. Mbegu zinazofaa kulimwa na Mtwara, mihogo inapandwa kuanzia mwezi Oktoba. Wapatiwe mbegu bora ili kuepuka tatizo la msimu huu kula mihogo ya sumu. Kama hawatapatiwa mbegu bora, tatizo litaendelea.

Mheshimiwa Spika, nguvukazi - vijana ambao ni tegemeo la Taifa, miongoni mwao wamehamia mijini. Lakini mipango ikiandaliwa vizuri, watarudi na kuungana na wenzao katika kilimo. Niipongeze Wizara kuwa na mipango ya kuwakopesha wakulima. Nashauri uzoefu utumike wa kuikubali NMN, sababu imeonyesha kuendesha kazi zake vizuri, na imekuwa na matawi hadi vijijini, na wanavijiji ndiyo Benki wanayoijua. Ikae nao na kuwapatia maelekezo nini wafanye. Kulingana na hali ya miji kuwa ngumu, vijana wengine wameanza kurudi kwa maelezo niliyoyatoa hapo juu. Nina imani kuwa wengi zaidi watarudi na kuungana na wenzao katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kuna viwanda 12 vya ubanguaji korosho. Serikali ijitahidi kuweka vivutio ili wawekezaji wavichukue mara, kwani kutofanya kazi viwanda, kunaathiri mambo mengi - kuchakaa kwa viwanda, kukosa ajira kwa vijana na wanawake. Hivyo, kwa vile vya Mtwara, ningeshauri Wizara kuvipa kipaumbele. Ukiangalia na kudumaa kwa maendeleo ya muda mrefu, kufufuliwa kwa viwanda hivyo kutachochea maendeleo ikiwemo uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuanza kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Pia nashukuru Wizara ya Kilimo kukubali kuingiza bwawa la Malolo na Nkinizwa kwenye bajeti ya 2004/2005. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ipo katika kilimo kwenye mabonde, kama vile Ziwa Victoria umetenga hekta zipatazo 200 tu. Hivi eneo halitoshi ama fedha ndizo hazitoshi? Mimi nashauri eneo liongezwe, na siyo bonde hilo tu, hata Manonga, Mto Ruaha, Mto Ruvu na hata Mto Rufiji. Ili tuondokane na njaa, lazima tuwekeze kwa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, Wizara irejeshe utaratibu wa mafunzo kwa wakulima kwa kuwalenga kuonekana na kilimo cha jembe la mkono. Mafunzo yalenge katika umwagiliaji, matumizi ya mbolea na mbegu bora. Wakati wa miaka ya 80 na 90, kulikuwa na mradi wa *NARLEP* ambao ulifanyika nchi nzima. Rejesheni mafunzo hapo pote nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na jembe la mkono, Serikali iweke mpango wa makusudi kuwa na jembe la ng'ombe na matgrekta madogo madogo.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, ondoa ukiritimba wa *Exim Bank.* Toa kwa faida ya wakulima wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakutakia kazi njema.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya Wizara ni nzuri sana, inagusa kila eneo la Wizara. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa umwagiliaji. Naomba jibu la kuridhisha kabla sijatoa Shilingi juu ya mradi huu. Inaonyesha mradi huu unawachanganya wanavijiji wa Diguzi, Lulongwe na Matuli. Waziri aliwaahidi wananchi pale kijijini. Naomba maelezo na idadi ya miradi ya aina hii ambayo imekwama. Wananchi, viongozi wa Kijiji,. Kata na Tarafa ya Ngerengere wanasubiri kauli yako.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa matrekta. Tunayo ardhi ya rutuba, wakulima wenye moyo na viongozi wanaojituma katika Wilaya zote za mkoa wetu. Tunaomba zana za kisasa za kilimo. Matrekta Ngerengere, Kiroka, Turiani, Mvuha, Bwakira, Mkulazi, Tununguo, Mikese, Mkuyuni, Kilombero, na kadhalika.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Aidha, naipongeza Wizara kwa kazi ngumu wanayofanya ya kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara/Waziri atoe ufafanuzi wa kina kuhusu taratibu zitazotumika kuaamua kutengeneza barabara kwa fedha za *STABEX* ya kahawa. Je, *Consultant* wa kutambua barabara zitakazotengenezwa kwa fedha *STABEX* alipewa hadidu zipi za rejea?

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana katika harakati za kupambana na umaskini na kujitosheleza kwa chakula. Aidha, hivi karibuni Wizara ilijibu swali langu Bungeni na kunieleza kwamba ilitoa Shs. 20,000,000/= kusaidia kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Nkenge *(Ngono Project).* Hata hivyo, uchunguzi wangu umebaini kuwa fedha hizo hazikufika kwa walengwa. Je, Wizara ilimkabidhi nani fedha hizo? Je, Wizara imefuatilia kuhakikisha fedha hizo zinafanya kazi iliyokusudiwa? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iwe inatoa taarifa kwa Wabunge na kwenye Vyombo vya Habari, zinazoonyesha fedha zinazotolewa Wilayani na kwenye miradi ya kilimo, ili Wabunge tuweze kufuatilia mapema matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kilimo hayawezi kupatikana iwapo mkazo haukuwekwa katika shughuli za utafiti.

Mheshimiwa Spika, utafiti ni jambo la msingi na la muhimu hasa ukizingatia mabadiliko ya hali ya hewa ulimwenguni, ukuaji wa teknolojia ya uzalishaji wa mazao ya kilimo,d lakini pia mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini tunavyo vituo vingi vinavyoendesha utafiti kuhusu masuala ya kilimo. Kamati ya Kilimo na Ardhi, ambnayo mimi ni Mjumbe, tulipata nafasi ya kutembelea baadhi ya Vituo vya Utafiti wa Kilimo. Tulijifunza mengi

mazuri, lakini tumeona mengi ambayo yanahitaji kurekebishwa ili kukuza ufanisi katika tafiti za kilimo.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa matatizo tuliyoyaona au kuelezwa ni pamoja na:-

(a) Uchache wa fedha kuendeshea tafiti.
(b) Ukosefu wa vifaa vya kisasa.
(c) Uchache wa Wataalam.
(d) Majengo yaliyochakaa.
(e) Uchache wa fursa za mafunzo ya ziada.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bajeti ya Wizara inayoelekezwa kwenye utafiti, kamwe haitatufikisha mbali, na kwa hivyo bado shughuli za utafiti zitaendelea kusuasua, na kwa hivyo mchango wake kwa maendeleo ya kilimo utakuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kufikiria upya kuona namna ambavyo shughuli za utafiti zinavyoweza kuboreshwa dna kutoa mchango mkubwa utakaoweza kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ili utafiti uwafikie wakulima, ni lazima huduma za ughani nazo ziboreshwe kwa wahusika kupewa elimu ya kutosha na vifaa vinavyostahili. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa utaratibu wa kufanya baadhi ya tafiti moja kwa moja kwa wakulima wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo inasaidia zana kukuza uwezo wa wakulima kutokana na kushirikishwa katika tafiti hizo. Napenda kuishauri Serikali kutilia mkazo suala hili la *on farm trials,* kwani zimeleta mafanikio makubwa katika Mapinduzi ya kilimo.

**MHE. OMARI S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nataka kumpongeza Mheshimiwa Keenja kwa juhudi zake ambazo anazionyesha katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pongezi zimfikie Mheshimiwa Prof. Mbawala na Katibu Mkuu - Bwana Ngirwa, kwa ushirikiano wao ambao wametoa kila unapofika ofisini kwao.

Mheshimiwa Spika, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri na timu yake wawatume Maafisa wao Kilwa ili wakaone Bonde la Nkoma ambalo liko Tarafa ya Njinjo, Kata ya Mitole. Bonde hili lilikuwa linalimwa na Kanisa la *Roman Catholic* la Kipatimu, ambalo walikuwa wanavuna zaidi ya tani 50,000.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ombi hili nililitoa mwaka 2002 na hadi sasa sijapata majibu, hivyo naomba baada ya Bunge, Mheshimiwa Naibu Waziri na Mkurugenzi wake wa Kitengo cha Kilimo cha Umwagiliaji, wafike Kilwa ili kufanya maandalizi ya kuliendeleza bonde hilo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi kinachotakiwa hapa ni matrekta angalau matano ili yatumike katika kuliendeleza bonde hili. Tuwasiliane kwa Simu Na. 0748-597397 - Dar es Salaam na Kilwa na 0744-839068 - Dar es Salaam tu.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mmheshsimiwa Spika, kwanza ninatoa shukrani kwa kupata nafasi ya kuchangia angalau machache katika Wizara hii ya Kilimo. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa maandalizi ya taarifa nzuri iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, ningeomba kutoa pole zangu za dhati kwa familia na ndugu wa Mahemu pamoja na wananchi wotge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kumpoteza Mbunge wao Marehemu Yete Sintemule Mwalyego. Mungu ailaze pema roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nianzie kwenye kilimo. Watanzania wote wanawawanaelewa na kukubali kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu. Kilimo ni mkombozi pekee wa uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningeshauri mambo yafuatayo:-

(a) Wataalam wetu waendane na kisayansi ya hali ya juu.

(b) Hali ya zana za kilimo, ziwe safi na za kileo zinazoendana na kilimo cha kitaalam.

(c) Mbegu zetu ziwe nzuri, zilizotunzwa kitaalam, zitumike katika maeneo ya ardhi yanayokubaliana na vipando hivyo.

(d) Mbolea ipatikane ya kutosha na isambazwe kwa wakati muafaka na bei iwe nafuu ya kuimudu mwananchi.

(e) Tuondokane na kilimo cha kutegememea mvua, lazima juhudi kubwa ichukuliwe katika kilimo cha umwagiliaji, lakini kiambatane na utaala wa hali ya juu. Suala la jembe la mkono, ninaomba kwa sasa tuliache kabisa.

(f) Pamoja na juhudi zote hizo, ili kuondoa njaa nchini pamoja na kuimarisha uchumi wa nchi yetu, basi suala la mabarabara na miundombinu mingine, iangaliwe na ishughulikiwe kithabiti.

Mheshimiwa Spika, mifugo ni sehemu muhimu dkatika uchumi wa nchi yetu. Lazima utaalam uelekezwe kwenye mifugo. Bado mifugo mingi inaendelezwa kienyeji. Naomba sana Wizara yetu sasa itilie mkazo na ifuatilie kwa dhati mifsugo yote. Majosho yaimarishwe, madawa yapatikane, Wataalam (Madaktari) wawe na vyombo vya kufuatilia mifugo na kutoa taaluma kwa mifugo yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho nashauri masoko ya ndani yaimarishwe vizuri, na masoko ya nje yatafutwe kwa kupeleka bidhaa zilizo bora kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba sana kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga kwa ushindi mzuri aliopata kwa kurejea Bungeni na kukipa heshima ya hali ya juu Chama chetu cha CCM.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa heshima ninaunga mkono mia kwa mia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie fursa hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba, kutoa rambirambi kwako wewe binafsi, Bunge lako Tukufu na kwa familia ya Marehemu kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote katika Wizara hii, kwa hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri. Ni hotuba nzuri katika hali, mazingira na uwezo wa Serikali ilio nao kuhusu hifadhi ya chakula.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Kitengo hiki, uongezwe na upatikane mapema. Kwa vile yapo maeneo yanayopata chakula kila mwaka na bado njaa inapatikana hata katika maeneo ambayo awali yalikua na chakula cha kutosha na ziada, nashauri:-

(a) Elimu kwa familia ya kujiwekea chakula cha kutosha, iendelee kutolewa. Ujulikane kuwa kuuza chakula kabla ya kuweka akiba ya kutosha ni uhujumu.

(b) Kanuni zitungwe angalau kwa kila familia ya watu watano, ijiwekee akiba ya magunia 12 kila mwisho wa mavuno kabla ya kuanza kuuza chakula chochote. Ni vizuri Serikali ya Kijiji ikapewa uwezo wa kisheria wa kulifuatilia hili, kwa vile usalama wa raia ni pamoja na kuhakikisha ya kuwa familia wakati wote ina chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, nimeipitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Nilitarajia katika baadhi ya miradi/mipango ya Wizara hii, Wilaya yangu nayo ingalitajwa. Kwa bahati mbaya Kwimba haionekani mahali popote. Nilitegemea ingalitajwa kwenye orodha ya Wilaya chini ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani *(PIDP).* Kwimba haimo (uk. 74). Hata hivyo, nashukuru kwa kutambuliwa Kwimba kama moja ya Wilaya zinazotarajiwa kuwa na njaa. Nilitegemea katika juhudi ya Wizara kuinasua Wilaya hii ambayo ndiyo pekee katika Mkoa wa Mwanza, isiyopakana na Ziwa Victoria, ingalipewa kipaumbele ili nayo iweze kujinasua.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. GEDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa jitihada zao za kuendelea kuboresha huduma katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, wakulima bado wana matatizo mengi. Bajeti ya Serikali na Wizara, inatoa matumaini ya kupunguza baadhi ya matatizo hayo. Changamoto kubwa kwa Wizara ni kutafsiri kwa vitendo matumaini hayo ili hatimaye yakafikie walengwa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa mipango yake ya *DADPS* na *DADS* ambayo imetuwezesha kupata nyenzo, zikiwemo fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Kukoboa Kahawa, kukarabati Kituo cha Maksai, kuanza kujenga intake kupitia *Zonal Iriigation Unit* kwa ajili ya umwagiliaji eneo la Mbebe.

Aidha, Mheshimiwa Spika, watumishi wa kilimo wameendelea kupata mafunzo, hivyo kuboresha uwezo na ufanisi wa utendaji kazi. Mwaka wa fedha 2003/2004, Wilaya yetu imepatiwa gari moja jipya *(pick-up) double cabin* kwa ajili ya shughuli za ugavi. Tunashukuru sana kwa miaada yote hii.

Mheshimiwa Spika, kiu ya maendeleo katika sekta ya kilimo ni kubwa sana. Wilaya yangu imedhamiria kuendelea kujitosheleza kwa chakula na kutoa ziada. Kwa mantiki hiyo, tunaomba Wizara iendelee kutoa misaada kadri itakavyoweza. Ombi maalum kwa Wizara ni kuendelea kusaidia kukamilisha Mradi wa Umwagiliaji Mbebe. Huu ni mradi mkubwa na wa matumaini kwa Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingine midogo katika maeneo ya Ikumbilo/Chitete, Mapogoro na Ilulu. Tukisaidiwa katika maeneo hayo, tuna hakika tutazalisha chakula cha ziada kitakachopelekwa katika maeneo yenye upungufu ndani ya nchi yetu.

Aidha, Mheshimiwa Spika, tunaomba msaada wa kukarabati Kituo cha Kutengeneza Matrekta. Tunayo matrekta mawili tu ambayo yanahitaji matengenezo. Uwezo wetu bado ni mdogo kugharamia shughuli hizi. Tunaomba msaada ili tuboreshe kilimo chetu na tuendelee kupambana na adui umaskini kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba suala la pembejeo kwa wakulima, lisimamiwe kwa makini zaidi. Pembejeo zipatikane kwa wakati na kuwafikia walengwa mapema. Nafuu iliyokusudiwa iwanufaishe wakulima badala ya kumezwa na wafanya biashara tu. Nashukuru kwa fursa hii. Nawatakia mafanikio mema, inawezekana, tupangane vizuri na tuchape kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kutoa pole kwa Mheshimiwa Dk. Aidha Kigoda na Mheshimiwa Dk. Abdallah Kigoda, kwa kuondokewa na mzazi wao. Pia nampa pole Mheshimiwa Anne Kilango Malecela

kwa kuvamiwa na majambazi. Vile ninampa pole Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kupata ajali. Pole nyingi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, Mwenyezi Mungu awape subira.

Mmheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha katika Bunge la kwanza la Afrika. Kwa namna ya pekee, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongela kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wake, na namwambia karibu Bungeni tena *(welcome).* CCM oyee.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi siyo mkulima, lakini mababu zangu walikuwa wakulima. Napenda kushauri yafuatayo:-

(a) Tuipige vita njaa kwa staili mbalimbali, ikiwemo mkazo juu ya kilimo, hasa wakulima wadogo wadogo wasaidiwe ili wazalishe zaidi. Tusifikirie kuwapa matajiri, lakini wazalishaji *(producers).*

(b) Wizara ibuni mipango mizuri ya kilimo cha kisasa *(modern agriculture),* kilimo ambacho kinawahusisha wote - vijana, watoto, wazee, hata akina mama, pamoja na wasomi na hata wataalam. Kuna wakulima wengine wamekuwa Marais wa mataifa makubwa *(the tools to him who has the ability to handle them).*

(c) *Modern agriculture needs modern technology.* Upatikanaji wa matrekta uwe nzuri. Kodi za aina zote ziondoshwe juuya matrekta.

(d) *Emphasize Irrigation Farming,* mwone siyo kitu cha kutegemewa sana, lakini umwagiliaji ndiyo mkombozi wetu.

(e) *We should take advantage i.e. geographical advantage and the availability of plenty of water resources in our country to boost Irrigation Farming, as a result of which will be producing plenty of crops and no more buying of food from outside instead selling to outside markets.*

(f) *We should not sit down and complain of being poor, and ask for help from donor countries, our poverty should be the parent of revolution, Agricultural Revolution is a must now and hardwork is the only sounded investment we should have to overcome our difficulties.*

(g) *Get what you can and keep what you have, fight idleness.* Kuna umuhimu wa kuwa na Benki ya Wakulima, ambayo itasaidia wakulima wadogo wadogo kupata mikopo, pamoja na kupata uwezo wa kuanzia viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda ambayo mengi yanaishia kuoza. Kwa mfano, kule *Thailand,* kuna Benki iitwayo *Thai Farmers Bank* na kadhalika. Hata sekta nyingine za uzalishaji zitafaidika na Benki za aina hizi.

(h) Wizara ifanye utafiti *(Research)* kwa mazao yetu. Kwa nini zabibu za Dodoma haziboreki kama zile kutoka Afrika Kusini au pengine kama Calfornia? *The Best Insurance PMolicy for the future of an industry is Research.*

(i) *Prioritize the building of infrastructure. Better roads, easy access to markets, better communication, availability of plenty cheap power (electric), etc.*

Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru sana Waziri wa Kilimo - Mheshimiwa Charles Keenja (Mb.) na Naibu wake - Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala (Mb.), na nawapongeza kwa hotuba nzuri na subira waliyokuwa nayo hata baada ya kuona kuwa bajheti yao haina tofauti na ya mwaka 2003/2004, na kujwa wanatarajiwa kufanya mengi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja 100%.

**MHE. MIZENGO K. P. PINDA:** Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 109 wa hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, unaonyesha mambo yafuatayo kuhusu kilimo cha umwagiliaji Wilayani Mpanda:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | Umwagiliaji | - Uruira | | Shs. 25,250,000/= |
| (b) | Majosho | - Yuseria ) | - nyonga )<br>- Mahumbi) | Shs. 15,150,000/= |
| (c) | *SACCOS*- Katavi) | | | Shs. 5.050,000/= |

Mheshimiwa Spika, kuhusu (b), Wilayani Mpanda hatuna Vijiji vya Useria wala Mahumbi. Ninahisi vijiji hivi vimekosewa kuandikwa . Naomba kujua vijiji hivi viko wapi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu (c), *SACCOS* hii iko katika Kijiji/Kata/Tarafa gani? Katavi ni jina la Mbuga ya Taifa iliyoko Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa hatua hii. Wilaya ya Mpanda ina mabonde mengi sana yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa sababu sehemu kubwa ya Wilaya hii iko katika Bonde la Ufa, Uruira ikiwa ni mojawapo. Mabonde haya yako katika Tarafa za Mpimbwe, Nsimbo, Mweze, Kabungu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majosho, ninaomba kueleza kwamba eneo hilo la Bonde la Ufa ambamo Ziwa Rukwa limo, linayo mifugo mingi sana ambayo inafuata malisho. Mifugo hii inahitaji majosho mengi kwa kuwa sasa hayapo. Inakadiriwa kwamba mifugo iliyopo katika bonde hilo ni zaidi ya 300,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maombi yafuatayo:-

(a) Wizara itume Wataalam wake ili waje kufanya uchunguzi kuhusu mabonde na mifugo iliyopo katika eneo hilo.

(b) Fedha zaidi itolewe kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na ujenzi wa majosho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, nami ninaungana na wenzangu kutoa mkono wa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego - Mbunge mwenzetu ambaye amefariki hapa Dodoma mwishoni mwa wiki iliyopita. Mwnyezi Mungu ailaze pema roho ya marehemu peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya kilimo. Wananchi wake asilimia 80% wanaishi vijijini na wanategemea kilimo kwa maisha yao. Ili wananchi na nchi yao watembee kifua mbele na wawe na kauli ya kusikilizwa na jamii nyingine au nchi nyingi yoyote na kuonekana kuwa wa maana, ni kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, ni kitendo cha aibu na kujidhalilisha kwa nchi kama Tanzania iliyobarikiwa kuwa na ardhi kubwa yenye kila sifa za kuzalisha chakula cha kutosha kwa wananchi wake na kupata ziada ya kuuza nje, kuwa ombaomba wa chakula. Tanzania ina maji ya kutosha ya juu na chini ya ardhi, ina ardhi yenye rutuba, inayo hali ya hewa inayoruhusu kilimo cha mazao mbalimbali na kadhalika. Inakuwaje watu wake wateseke na njaa? Hali hiik inaonyesha kuwa bado hatujajiweka sawa katika utekelezaji wa mipango yetu na hata katika kuweka vipaumbele kwa manufaa ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, ili tujitoe katika kashfa hii ya ombaomba chakula, ni lazima sasa tujikite katika kilimo cha umwagiliaji kwa vitendo,, siyo kwa mipango mizuri ya kwenye karatasi tu. Wananchi washirikishwe kikamilifu katika mipango hii ili waweze kupata au kuwa na sense ya ownership ya mpango mzima na kusaidiana na Serikali, wakiwa na uchungu wa jambo zima. Hivyo ningeshauri kwa upande wa kilimo, kipaumbele namba moja iwe ni kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Misri kwa asilimia kubwa ni jangwa, na kianzio chao kikubwa cha maji ni mimoja tu Mto Nile. Lakini wameweka kipaumbele juu ya kilimo cha umwagiliaji, kitendo ambacho kimewawezesha kulibadili janwa lenye mchanga milima kwa milima na joto la ajabu kuwa ardhi inayozalisha mazao mbalimbali yanayotosheleza soko la ndani na hata kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, nasi tufuate mfano huyo. Wamisri wapo tayari kusaidia kwa maelezo ya viongozi wa huko. Hivyo ninashauri wizara zetu mbili - Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, ziandae programu ya pamoja na kupeleka ombi la msaada huko haraka iwezekanavyo kabla hawajasahau kauli yao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuchangia ni kuunganisha mazao ya matunda na mboga mboga na viwanda vya kilimo *(agro-based industries).* Matunda

mengi na mboga nyingi zinapotea. Tujitahidi kushajiisha wawekezaji katika maeneo haya, kwanza ajira itaongezeka na kipato kwa mkulima kitaongezeka kutokana na soko la uhakika. Mbona nchi nyingi inawezekana, kwa nini hapa Tanzania imekuwa vigumu kupata hivi viwanda? Kwa hili, Mheshimiwa Waziri atueleze hatua alizochukua na amekwama wapi na ana mpango gani wa kujikwamua?

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la utafiti juu ya mambo mbalimbali ya kilimo na matumizi ya matukio *(research findings)* ya tafiti hizo. Hapa ninapenda kuwapongeza Wataalam kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli ukitembelea Vituo vya Utafiti, utaona jitihada za hawa Wataalam. La kusikitisha ni kwamba matokeo ya tafiti hayawafikii kikamilifu walengwa hasa wa vijiji vya mbali na vituo. Mara nyingi yanaishia kwenye maabara. Mabwana Shamba ambao wangesaidia kusambaza matokeo haya, wanashindwa kutokana na kutokuwa na vipando vya kuwafikisha huko. Aidha, hakuna mpango wa makusudi wa kutoa semina kwa Mabwana Shamba kuwaelimisha juu ya tafiti hizo.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri alirekebishe tatizo hili mara moja ili wananchi walio wengi wafaidi matunda yha tafiti za kilimo. Aidha, vituo vya tafiti vipatiwe fedha za kutosha kuendeshea kazi zao na wataalam wapatiwe maslahi mazuri ili wasihame na kwenda kutafuta maslahi mazuri kwingineko. Vile vile matokeo ya tafiti yalindwe ili wageni wasiyapate kiholela na kuyageuza ya kwao. Kwani teknolojia ya *tissue culture,* anaweza mgeni akabeba jani dogo tu la mbuni *(coffee leaves)* akaweka kwenye mfuko wa *plastic* na kupulizia *oxygen*, akafika nalo umbali wowote na kuzalisha miche mingi tu kutokana na jani lile, badala yake akaweza kuuza kana kwamba ina asili ya kwao.

Mheshimiwa Spika, ulimwengu hivi sasa umeanza kukataa kutumia mazao ya kilimo yanayooteshwa kwa kutumwa mbolea za chumvi chumvi. Hivyo Serikali iendelee kuwaelimisha wakulima juu ya utumiaji wa mbolea ya samadi na mboji ambazo zinapatikana katika mazingira yetu bila ya gharama kubwa. Misri kule jangwani, kwa kiasi kikubwa wanatumia mbolea ya mboji, na utashangaa mazao mengi yanayopatipatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iandae mpango na utaratibu mzuri wa kuwapatia wakulima mikopo na itoe mafunzo juu ya utumiaji bora wa mikopo hiyo. Aidha, mpango kabambe uandaliwe wa kuwafanya vijana wapende kulima, na hii itawezekana tu kwa kuandaa vikundi vya vijana (kwanza kama *pilot)* na kuwapatia mazingira mazuri ya kilimo. Mfano, wapate maeneo mazuri, zana bora, pembejeo na mikopo itakayosaidia kununulia mahitaji mengine muhimu kwa kilimo. Ninaamini manufaa yatakayopatikana ni makubwa, na wengine watafuata kwani watakuwa wamejifunza kwa wenzao.

Mheshimiwa Spika, tatizo la masoko ya mazao ya kilimo hasa matunda na mboga mboga, litafutiwe ufumbuzi. Aidha, wananchi waelimishwe namna ya kuzalisha kwa matakwa ya soko hasa la nje, kitu ambacho kinakosekana kwa wakulima wengi wadogo wadogo ambao wanashindwa kutunza vyema mazao na uhifadhi unakuwa hafifu sana kiasi kwamba *quality* ya mazao yao haifikii kiwango kinachohitajika kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza hoja hii ya Wizara ya Kilimo na kuunga mkono, naomba nichangie machache katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchangia kuhusu utafiti. Ili kilimo chetu kiwe cha kisasa, ni lazima tujali utafiti katika nchi yetu. Katika mabadiliko ya kiuchumi na hasa Serikali ilipojitoa kwenye biashara, tukatekeleza pia taasisi zetu za utafiti. Kilimo hakiwezi kuendelea bila kuwa na utafiti wa mbegu zinazostahili katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Vituo vingi vya utafiti vimejaa Wataalam waliokata tamaa kwa sababu ya kutopata fedha za kuwawezesha kufanya kazi za utafiti.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hatuna mbegu za aina yoyote - si ya mazao ya chakula au ya biashara. Wakulima wanahangaika kupata mbegu e.g. mahindi toka Malawi, Kenya na sehemu zingine za dunia. Mahindi haya yamefanyiwa utafiti katika nchi zao kulingana na hali ya hewa ya huko pamoja na hali ya udongo na wadudu waliopo. Kwa kweli hatutaendelea katika hali hii, kufikisha matokeo ya utafiti kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kufikisha matokeo yetu ya utafiti kwa wakulima. Utafiti wa mazao mbalimbali ulishafanyika e.g. mahindi, mitende, mazao ya biashara katika vituo vyetu mbalimbali miaka ya nyuma, lakini matokeo hayo bado yapo kwenye vituo vya utafiti tu. Kuna sababu gani ya kupoteza fedha nyingi bila kupeleka utafiti huo kwa walengwa? Baada ya utafiti, tutumie fedha maradufu ili kupeleka utafiti huo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, tafadhali pia tutumie mbegu zilizofanyiwa utafiti katika nchi yetu, na wala siyo kupata mbegu toka nchi nyingi. Tufufue vituo vyetu vya utafiti na kuvijali, ili vitusaidie katika mMapinduzi yetu ya kilimo.

**MHE. PROF DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa matumaini makubwa.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa pato la taifa kunategemea kwa kiasi kikubwa ukuaji katika sekta ya kilimo. Kilimo ambacho kinategemea mvua isiyo ya uhakika. Kilimo ambacho kinategemea jembe la mkono. Kilimo ambacho kwa kiasi kikubwa ni kilimo cha kujikimu, na siyo kilimo cha biashara. Kilimo ambacho kinategemea pembejeo ambazo zinapatikana kwa bei ya juu, hata kama zimepewa unafuu wa kodi kwa sababu ya hali mbaya ya usafiri, na hivyo kusababisha zisifike kwa wakati. Kilimo ambacho sehemu kubwa ya mazao yake hayaongezewi thamani, bali kuuzwa yakiwa ghafi. Kilimo ambacho kwa miaka zaidi ya 40 ya kujitawala, bado hakijabadilika. Kilimo ambacho ni duni, lakini kinategemewa kibebe uchumi wa kisasa wa karne ya sayansi na teknolojia wakati chenyewe kinatumia sayansi na teknolojia duni. Kilimo

ambacho mwaka 2002 kilikua kwa asilimia 5.0%, wakati mwaka 2003 kilikua kwa asilimia 4.0%.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Taifa hili upo njia panda, na lazima kuamua njia ya kwenda. Ziko njia mbili. Njia ya kwanza ni kuondokana na sekta hii ya kilimo na kuwekeza zaidi katika sekta ambazo zitakuza pato la Taifa. Zipo sekta zinazoonyhesha kukua:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Madini** | - | 2002 | - | 15.0% |
| | | 2003 | - | 17.0% |
| **Viwanda** | - | 2002 | - | 8.0% |
| | | 2003 | - | 8.6% |

Mheshimiwa Spika, vile vile wakati umefika kuzungumza kwa makini nafasi ya nchi hii kijiografia na namna ya kukuza uchumi wa Taifa kwa kuvuna uchumi wa jiografia ya nchi hii. Nchi yetu inazungukwa na nchi takriban nane ambazo zinategemea Bandari ya Dar es Salaam. Wataalkam wafungue mjadala wa mtazamo huu.

Mheshimiwa Spika, njia ya pili ni kufanya uwekezaji wa makusudi wa kuleta Mapinduzi ya kilimo ya kweli, na siyo kama tulivyokuwa tukifanya miaka ya nyuma. Kusema kwamba kilimo ni uti wa mgongo au sekta kiongozi wa uchumi wetu bila ya kuwekeza katika kilimo, bila ya kuleta Mapinduzi ya kweli ya kilimo kwa maana ya kuwa na kilimo cha kitaalam na chenye kutumia zana bora za kisasa kama vile plau na matrekta; kilimo hakiwezi kikawa sekta kiongozi bila ya kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua na kuingia katika kilimo cha umwagiliaji maji - kumwagilia hekta milioni 29.4 zinazofaa badala ya hekta 200,895 za sasa. Kutoridhika na ongezeko la asilimia 44.89% kwa miaka mitano iliyopita, hili ni ongezeko dogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo kinanyang'anyana maji na umeme, lazima kuondokana na umeme wa maji ili maji yote yatumike kwenye kilimo. Mpango kamambe wa kilimo cha umwagiliaji, ambao ukifika mwaka 2017, hekta 405,400 zitakuwa zinamwagiliwa. Huu huwezi ukauita ni mpango kamambe wakati eneo linalofaa kuwagilia ni hekta milioni 29.4. Si lolote wala si chochote kuwa na mpango kama huo wenye lengo dogo kama hilo, tena kumwagilia zao moja la mpunga!!

Mheshimiwa Spika, kilimo hakiwezi kikawa sekta kiongozi bila ya kuwekeza katika kilimo kwa kufufua vituo vya maksai, kuongeza uingizaji wa matrekta zaidi kuliko hayo 170 ya mwaka jana. Kilimo kitakuwa na maana kama thamani ya mazao ya kilimo kwa kuyasindika na kuanzisha viwanda vya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kubadilisha mtazamo wa kilimo ili kifanane na nafasi inayotakiwa kuchukua katika uchumi.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mmheshimiwa Waziri na Wataalam wa Wizara hii. Napongeza juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara hii katika kuboresha huduma za kilimo.

Mheshimiwa Spika, wakulima wengi wanaozalisha chakula ni wanawake walioko vijijini. Lakini huduma nyingi za ugavi hazijawagusa. Waathirika wakubwa wa huduma za kilimo ni wanawake. Sasa mikakati ilenge kumkomboa mwanamke kwa kuwapa pembejeo na utaalam wa kilimo. Wataalam wa ugavi watumie vikundi vya wanawake vijijini ili kuwafikia. Familia duni zenye upungufu wa chakula, zifikiriwe kupewa pembejeo kwa njia ya kukopeshwa kupitia kwenye vikundi vyao vya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala ya UKIMWI. Naipongeza Wizara ya Kilimo kufikiria kuingiza suala la UKIMWI katika mpango wa bajeti ya mwaka huu. Lakini elimu ya UKIMWI katika Wizara hii, ni lazima iendane na elimu ya lishe bora. Lakini katika hotuba hii sijaona elimu ya lishe ikizungumzwa. Wizara ni lazima iwe na mikakati ya makusudi kuimarisha kitengo cha lishe ili kiweze kutoa elimu kwa jamii kuhusu lishe bora.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha mboga na matunda ni muhimu sana katika Kaya. Utaalam uendelee kutolewa kwa wananchi. Kilimo cha maksai pia kitiliwe umuhimu ili kuepukana na jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

**MHE.ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, Serikali iandae mipango kabambe ya kukabiliana na janga la njaa nchini ili mara nyingine lisiathiri kwa kiasi kikubwa wananchi wetu kama ilivyokuwa katika kipindi hichi. Katika kulikabili janga hili Serikali Kuu itenge fedha za ziada ambazo zitabaki kwa dharura kama hii tu, na si kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, iandae mipango endelevu ya miundombinu katika mipango ya umwagiliaji ili chakula cha kutosha kiweze kuzalishwa nchini, na kuondoa upungufu wa mara kwa mara wa chakula. Kwa kuwa Watanzania wengi na maskini, ni vyema kwa Serikali - kwa chakula kitakachouzwa ndani ya nchi toka *SGR,* kiuzwe kwa bei ya kununulia bila kuongeza faida.

Mheshimiwa Spika, katika kila kijiji itolewe semina kila msimu wa kuvuna unapokaribia juu ya namna bora ya kuvuna na kutunza nafaka ili zisiharibiwa na wadudu. Maafisa wa Wizara wahakikishe wanafundisha wananchi wa vijijini namna nzuri ya kutunza akiba yao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, katika kutilia mkazo suala la *irrigation,* nashauri Serikali Kuu kufikiria kuanzisha Wizara pekee itakayoshughulikia suala zima la umwagiliaji nchini ili kupambana na balaa la njaa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifikirie uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo katika maeneo husika ili kuongeza bei ya mazao ya wakulima, na pia kuongeza ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, vituo vya utafiti vifanyiwe ukarabati wa hali ya juu ili viendane na hali halisi ya karne ya 21 ya sayansi na ufundi.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napeleka salamu zangu za rambirambi kutokana na kifo cha mwenzetu Mbunge wa Mbeya Vijijini - Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyefariki dunia hivi majuzi.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa kuandaa hotuba ya bajeti safi ya Wizara yenu.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja ya Kilimo, ningependa kukumbusha tu kuwa kumekuwa na *negative publicity* kutoka kwa Wabunge na baadhi ya vyombo vya habari. Malengo ya criticism hizi ni kutaka Wizara ijirekebishe katika mambo muhimu yaliyozungumziwa, na kamwe Wizara isijione kuwa viongozi wake wanalengwa binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umwagiliaji, tafadhalini Wizara mliwekee maanani. Angalieni vyanzo vikubwa hasa vya Rufiji, Malagarasi, Bonde la Matandu, Ruvuma na Lukuledi. Haya ni maeneo ya uhakika. Kama ni masta plani, basi lazima ianze katika maeneo hayao ambayo yanaweza kulisha nchi nzima. Tusipoteze fedha nyingi kuhudumia vijisehemu vidogo vidogo, lazima sasa tuende kwa wigo mpana. Tuone katika bajeti hii dhamira hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kukarabati matrekta, umekwenda wapi? Wilaya ya Masasi walijaza fomu za kukarabati matrekta mengi, lakin cha ajabu ni kuwa hata mtu mmoja hakupata mkopo huu ambao ungesaidia kufufua zana muhimu za kulimia. Sasa mpango huu upo bado ama nini kifanyike ili matrekta ya Wilaya ya Masasi yakarabatiwe mzumu huu?

Mheshimiwa Spika, nawatakia kheri katika utekelezaji wa Bajeti hii na ninaunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula, na nampongeza sana Mheshimiwa Keenja kwa kazi ngumu anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi za Serikali kukuza kilimo kwa kuondoa kodi zote katika kilimo, na pia kwa kujaribu kuvutia wawekezaji katika kilimo. Kwa hiyo, nashauri yafuatayo kwa nia ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, mikopo inayolenga wakulima wadogo wadogo, iwafikie. Naomba sana wananchi wa Kongwa walioomba mikopo ya ukarabati wa matrekta yao,

wapate japo kumi kiwilaya. Tutashukuru kwa vile ni dogo, lakini mwaka huu mmeliongeza kwa Shs. 3bn./=

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati ya kununua magari kwa Idara za Kilimo Wilayani, naomba kuikumbusha Wizara kuwa Kongwa hatukupewa mgao wa yale magari 52 ya mwaka jana. Ningependa kushauri ununuzi wa pikipiki badala ya magari, na zigawiwe kwenye Kata ili wataalam wa Extension waweze kuwafikia wakulima huko waliko.

Mheshimiwa Spika, Kongwa tunao uwezo wa kuboresha kilimo cha karanga, lakini soko lake si la uhakioka. Tusaidieni tupate soko ili nasi tujinasue na umaskin. Bodi ya Mazao mchanganyiko huko Ushirika na Masoko, inaanza lini? Ianze haraka tafadhali na ikiwezekana iwe chini ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kongwa, bado ina upungufu wa chakula hasa katika maeneo ya Tarafa ya Kongwa Vijijini vya Manungu, Vilundilo, Mbande, Sejeli, Nkurani, Banyibanyi na Nsunjilile. Tafadhali hawa wafikiriwe kupata chakula cha msaada kuanzia Oktoba/Novemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, tunataka wilayani kwetu kuimarisha kilimo cha mtama. Tunaomba uhakika wa soko na aina ya mtama wenye soko. Mtama ni ukombozi mkubwa kwetu kwa kilimo cha chakula na biashara. Tuonyesheni soko.

Mheshimiwa Spika, tunayo katika Wilaya ya Kongwa, maeneo mazuri sana kwa kilimo cha umwagiliaji katika Vijiji vya Suguta, Chamkoroma, Manghweta, Tubugwe na Msta. Ni maeneo yenye maji mwaka mzima. Kinachohitajika ni mradi wa kuboresha mifereji kwa vile maji mengi yanaingia ardhini kwenye mchanga *(sand).* Kwa hiyo, hafiki ya kutosha *downstream.*

Mheshimiwa Spika, tunawaomba *SGR* wajenge ma-*godown* mapya pale Kibaigwa ili nao wanunue mahindi kuyahifadhi pale pale tayari kupeleka kokote nchini penye upungufu.

Mheshimiwa Spika, ningelishauri Mheshimiwa Waziri atafute *tractors* za bei nafuu na *used* kokote kule duniani. *Let us know.* Tutafanya kila liwezekanalo kuagiza sisi wenyewe kutoka huko ziliko na kuzileta Tanzania. Isiwe ni jukumu la Waziri peke yake ku-*import tractors.* Tunachokosa ni *reliable information.*

Mheshimiwa Spika, mwisho nina mwaliko rasmi Mheshimiwa Waziri kwamba utembelee vijiji viwili au vitatu tu Wilayani Kongwa uone namna wakulima wanavyo-*progress* kinyuma na imani ya wengi kuwa hakuna jema katika kilimo. Karibu Kongwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALHAJI SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nilisahau hoja yangu kwa Mheshimiwa Charles N. Keenja (Mb.) - Waziri wa Kilimo na Chakula, katika mchango wangu kwa kusema.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake, anipatie msimamo wake. Hoja ni kwamba Wiozara ya Kilimo na Chakula ishirikiane na Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iwe na mpango wa kupeleka wakulima *undergraduates* wanapokuwa likizoni.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo itakuwa inawezesha wakulima kupata mbinu mpya za *farm management.* Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kuna jambo dogo ambalo litahitaji uamzi wa Bunge hivi punde. Halikuwa kwenye *Order Paper* kwa sababu linahusu uendeshaji wa shughuli zetu hapa ndani. Kwa kuwa haikuwa kwenye *Order Paper* basi Waheshimiwa Wabunge waliokwenda kunywa chai na hivi hawakujua kwamba litakuwepo.

Kwa ajili hiyo kabla halijawekwa Mezani namwomba *Serjeant-at-arms* kengele ili Waheshimiwa Wabunge walioko nje waweze kurudi ndani ambao hawapo kwenye Kamati ili tufanye uamzi huo mdogo.

*(Hapa kengele ilipigwa kwa ajili ya Wabunge walioko nje ya ukumbi waingie ndani ya ukumbi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni Na. 23 Kifungu kidogo cha (vii) kinasema kwamba Serikali itakuwa na haki ya kuagiza shughuli zake ziwekwe katika orodha ya shughuli za kila siku kwa mpangilio ambao Serikali yenyewe itaona unafaa. Serikali imepewa fursa hiyo.

Nimearifiwa na Msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni, kwamba lipo jambo la dharura ambalo linahitaji uamuzi wa Bunge hili si zaidi ya kesho. Kwa sababu kesho ndiyo mwisho wa hilo ambalo wanataka kulifanyia uamzi. Uamuzi usipofanyika kesho mambo yataharibika.

Lakini litalielezwa na Mwakilishi wa Serikali. Sasa uamuzi mdogo ninaousema unahitajika kufanyika leo ni kutokana na Kanuni nyingine ya Bunge ambayo ni Kanuni ya 79 Kifungu kidogo cha (ii). Kanuni hiyo inataka kwamba tukishaanza shughuli za Bajeti lazima ziendelee mfululizo bila kuwekwa kitu kingine mpaka zimalizike.

Kwa ajili hiyo, lakini Kanuni hiyo inasema, isipokuwa kama Bunge litaamua vinginevyo. Iko ruksa kwa Bunge kuamua kubadilisha Kanuni hiyo, kwamba tukishaanza shughuli za Bajeti basi hakuna kuweka kitu kingine mpaka vikamilike. Isipokuwa Bunge likiamua vinginevyo.

Sasa kwa kuwa Serikali ina shughuli za dharura inataka zifanyike kesho tunahitaji hoja ya kuliomba Bunge likubali kwamba kesho tusifanye shughuli za Bajeti tufanye

hizo shughuli nyingine. Kwa ajili hiyo namwomba Mheshimiwa *Chief Whip* wa Serikali atoe hiyo hoja.

## KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

## HOJA YA KULIOMBA BUNGE LIKUBALI KUFANYIWA SHUGHULI NYINGINE NJE YA BAJETI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 79(ii) inasema kama ifuatavyo: "Isipokuwa kama Bunge litaamua vinginevyo, shughuli za Bajeti ya Serikali zitapewa nafasi ya kwanza kabla ya shughuli nyingine yoyote na zitawekwa kwanza kwenye orodha ya shughuli za kila siku mpaka zitakapokuwa zimemalizika." mwisho wa kunukuu.

Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, Mheshimiwa Spika, na maelezo hayo ya Kanuni naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kesho tarehe 30 Juni, 2004 tufanye shughuli nyingine ambayo haihusiani na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Lakini shughuli hiyo nyingine si bora Bunge lijulishwe? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Narudia tena Mheshimiwa Spika, kwamba naomba Bunge lako Tukufu likubali kwamba kesho tarehe 30 mwezi wa sita, tufanye shughuli ya Kujadili na Kupitisha Azimio la Kuongeza Uhai wa *LART* ambao mwisho wake ni tarehe ya kesho, suala ambalo halihusiani na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Hii ni kuomba ruksa ya Bunge tu kwamba Kanuni hiyo isitumike kwa kesho. Hii Kanuni ya kwamba lazima tufanye Bajeti mpaka imalizike. Kwa hiyo, tupate uamzi wa Bunge.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

*Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge ilipitishwa na Bunge*

*(Bunge liliridhia uamzi uliofanywa ili kazi ya dharura iliyopitishwa ifanyike)*

**SPIKA:** Kwa hiyo hoja imeafikiwa. Kwa ajili hiyo, *Order Paper* ya kesho itasema kuwa kutakuwa na maswali kama kawaida. Kabla ya maswali ile Hotuba ya Waziri pamoja Taarifa ya Kamati, zitawekwa Mezani kama kawaida. Halafu baada ya

Maswali na Majibu kutakuwa na hilo Azimio la Kuliomba Bunge liongeze muda wa *LART* ambao unakwisha kesho tarehe 30 Juni, 2004.

Sasa hatujui itajadiliwa kwa kipindi gani hilo Azimio. Lakini tunadhani litakwisha kabla ya mwisho wa Kikao cha kesho yaani kabla siku haijaisha, tutakuwa tumeshamaliza kuliamua hilo Azimio. Kwa hiyo, ili siku hiyo isipotee bure au sehemu ya siku itakayokuwa imebaki isipotee bure, tumeamua kuweka Semina. Semina kuhusu Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. *(Makofi)*

Tutapata maelezo kutoka Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili tuelewe vizuri hiyo shughuli ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Sasa baada ya maelezo hayo ili tuwape watoa hoja nafasi ya kuwasiliana na Wataalam wao kabla hawajaanza kujibu hoja leo jioni, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni.

*(Saa 05.48 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge asubuhi tulikuwa tumemaliza orodha ya wazungumzaji, kwa hiyo sasa tutamwita Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo na Chakula aanze kufanya majumuisho.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ninazungumza kwa mara ya kwanza tangu Bunge hili la bajeti lianze, tafadhali uniruhusu nami nijiunge na Wabunge wenzangu katika kutoa maneno machache ya utangulizi yafuatayo: Kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Namtumbo na mimi mwenyewe binafsi, naomba kwanza nianze na kutoa rambirambi kwa familia ya wapiga kura wa Mbeya Vijijini na familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyefariki ghafla majuzi hapa Dodoma. Namwomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mapema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, natoa pole kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa kuvamiwa na majambazi njiani na Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kupata ajali barabarani. Namtakia Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere apone mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuweka historia kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Hongera sana Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa CCM na kumbwaga mpinzani wake, Mwenyekiti wa *UDP* Kitaifa. Hongera sana *Comrade* Makanga kwa ushindi huo wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya ya utangulizi, sasa napenda kutamka rasmi kuwa, naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia Hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu pia nianze kusaidia kutoa maelezo ya ufafanuzi wa baadhi ya michango mizuri sana ya ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge yenye lengo la kutuelekeza jinsi ya kufanikisha huduma za Wizara hii ya Kilimo katika mwaka wa shughuli unaoanza kesho kutwa. Tumewasikia Wabunge, tumewaelewa fika na tunakubaliana nanyi sana kwa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, siyo rahisi kutoa maelezo au kujibu kila hoja katika hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya ufinyu wa muda jioni hii ya leo. Lakini hata hivyo, tunaahidi kwa dhati kabisa tutayazingatia yote katika utekelezaji kwa umakini na ubunifu. Mengine mengi atachangia mtoa hoja mwenyewe, Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja iliyochangiwa na Wabunge wengi sana, inayohusu umwagiliaji wa maji mashambani. Mwaka huu wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula, imedhamiria kulenga kuendelea kuongeza eneo la uzalishaji kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani kwa jumla ya hekta 27,124 likiwa ongezeko kubwa kwa shughuli zilizofanyika kuanzia mwaka 2002 hadi mwaka huu wa 2004, nikijumuisha yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilibidi nifuatilie kuona nini tumefanya, kadri takwimu tulizonazo mwaka 2001/2002, tulianza na hekta 4,806 katika Wilaya nne na *scheme* tano. Huo ni mwaka ule wa mwanzo. Uliofuata 2002/2003, hekta 11,242 katika Wilaya 37, *scheme* 21, ni ongezeko mara mbili. Mwenyewe niliburudika kuona vile vile kumbe hatukulala sana kama tulivyosemwa. Mwaka wa tatu ambao ndiyo huu unaoishia leo au kesho, yaani 2003/2004, zimelimwa hekta 23,970 katika Wilaya 75, *scheme* 51. Sasa baada ya kuona hayo yote, tunaomba tuwapongeze sana *Irrigation Engineers* wetu wamejitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya kipindi hicho hicho ndiyo imetengenezwa *Irrigation Master Plan* ya kuainisha, sasa sio tu wanaongeza lakini wakaona tufanye kitu kinachoeleweka zaidi, sasa ni hekta milioni 29 zimeainishwa na kwa hiyo sasa hata tukisema tunataka kufanya kitu kinachoeleweka, inaeleweka tunaanzia wapi. Kwa hiyo, napenda tena kuwapongeza sana *Irrigation Engineers* wetu kwa jitihada hizo kufanya hayo yote mawili kwa pamoja ndani ya miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huu wa ujumla, sasa naomba nigusie hoja zingine moja moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitawataja Waheshimiwa Wabunge waliochangia, jukumu hilo ni la mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Kulikuwepo na hoja ambayo ilihusu fedha za mipango ya maendeleo ya kilimo zinazotolewa Wilayani zitangazwe kwenye vyombo vya habari na Wabunge wajulishwe ili wafuatilie utekelezaji wa mipango yake. Sasa jibu ni kwamba, fedha zilizotolewa kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya kilimo kwa mwaka 2003/2004, zilitangazwa katika magazeti ya Uhuru na *Daily News.* Ushauri huu utazidi kuzingatiwa katika kipindi hiki cha 2004/2005. Kwa hiyo, tunakubaliana na hoja hiyo ya Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa Wilaya ya Kwimba haipo kwenye mipango ya Wilaya ya Kilimo. Baada ya kupeleleza tumegundua kwamba, mipango kama ile ya *DADPs* lazima iibuke huko, iletwe Wizarani tutaishirikisha. Hata hivyo, ipo miradi ya *irrigation* katika Wilaya ya Kwimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni malalamiko ya kutokuwa na imani na Benki ya *Exim* kwa kuwa ina upendeleo na haitoi huduma ipasavyo hasa kwa wasio Wahindi. Hilo baada ya kupeleleza imegundulika kuwa lilihusu zaidi matatizo ya Mfuko wa Pembejeo. Baada ya kupeleleza sana tukagundua kwamba, vigezo vile havikuwa Uhindi wala Uafrika, lakini vigezo vilikuwa hivi, lazima kuwa na hati miliki ya mali isiyohamishika, kwa mfano, nyumba na kadhalika. Lakini kama huna nyumba au shamba lenye hati miliki hata kiapo cha Mahakama bado kinafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu inawezekana kabisa mwingine asipendelee sana kwenda Benki hii ya Biashara na naona Mheshimiwa Waziri mtoa hoja ataelezea zaidi, bado unaweza kutumia kama unatoka maeneo ya Mufindi kuna *Mufindi Community Bank,* ambayo haina utata huu wa *Exim* na vile vile kama unatokea Mbinga kuna *Community Bank,* huna haja ya kupambana na *Exim.* Lakini tumegundua vile vile nchini kote kuna Vyama vya Kuweka na Kukopa chini ya Shirikisho la *SCCULT* havina matatizo haya. Kwa hiyo, tunaomba kama kuna utata mwingi uliojitokeza basi tuelekee hasa kutumia Vyama vya Kuweka na Kukopa na zaidi tunaomba Waheshimiwa Wabunge, mtusaidie kueneza shughuli hizi za kupanua Vyama vya Kuweka na Kukopa kwa sababu havina masharti ya hati miliki. Tukitumia Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS),* itatusaidia sana kukwepa kukwamishwa na shughuli zetu za kilimo katika kuutumia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna *Kilimanjaro Cooperative Bank* na vile vile kuna *Kagera Cooperative Bank.* Zote zinafanya kazi hiyo na hazina utata kama *Exim* ilivyojitokeza katika muda wa siku mbili tulizosikiliza majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo kulikuwa na suala la Mfuko wa Pembejeo wa Kilimo kuwa una wadaiwa sugu wa kiasi cha Sh. 4,432,432,000/= na hao

siyo kama taarifa zao hazipo na sio wakulima walalahoi, ni watu wenye uwezo lakini wanaachiwa tu. Hatua gani zinachukuliwa hasa dhidi ya wadaiwa hawa sugu. Tumepeleleza, tukagundua kuwa ni kweli wapo wadaiwa sugu lakini Mfuko umefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadaiwa 171 ambao walikuwa wanadaiwa kiasi cha shilingi bilioni nne *plus* kama nilivyotaja hapo juu, walifikishwa Mahakamani. Hadi tarehe 15 Juni, 2004 wadaiwa 90 ambao wanadaiwa kiasi cha Sh. 1,807,635,000/= kesi zao zimehukumiwa. Hukumu zake ni pamoja na kuuza mali zilizowekwa dhamana na wakopaji. Kwa hiyo, dhamana zao zimeuzwa. Dhamana hamsini na saba zimeuzwa na kuweza kurejesha kiasi cha Sh. 343,000,000/=. Kesi 81 zenye thamani ya Sh. 2,600,000,000/= bado zinaendelea Mahakamani. Kwa hiyo, tunafuatilia, tunataka fedha hizi zirudi kusudi ziweze kupanua shughuli za Mfuko wa Pembejeo wa Taifa. Kwa hiyo, kwa niaba ya Wizara naupongeza uongozi wa Mfuko kwa jitihada hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilenge masharti ya mikopo ya kukarabati matrekta ili wakulima waweze kukopa. Sasa jibu ni hili, ili kutopata tatizo la kuweka rehani kwenye Benki ya Biashara, mkopaji anashauriwa alete maombi yake kwa kupitia Vyama vya Ushirika kama nilivyosema Benki mbili za Ushirika hizo. Lakini kama yupo mbali na benki hizo, basi atafute Vyama vya Kuweka na Kukopa au *SCCULT*, awasilishe maombi haya kusudi tuweze kuanzisha huduma hizo. Huduma hizo hazitaendeshwa na Serikali yenyewe, zinaendeshwa na sekta binafsi na kwa hiyo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, mtusaidie kupiga debe ili wajitokeze watu na *NGOs* zozote wanazoweza kuanzisha, sio kununua trekta moja moja lakini vile vile kuanzisha vituo vya kukodishia matrekta ikiwezekana. Lakini isipowezekana kupata trekta basi bado tuzingatie kutumia majembe yanayokokotwa na wanyama kazi hasa maeneo ya wafugaji kama vile ilivyo katika ukanda mwingi wa Magharibi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilisema Serikali iwasaidie wakulima milimani kwa kuwawekea mifumo ya umwagiliaji maji kwa njia ya matone. Ni kweli tumelitambua hilo na tunalizingatia. Hivi sasa kuna aina nyingi tu za umwagiliaji, ipo ya kumwagilia kwa juu, lakini sasa hivi umeanza utaalam mwingine ambao ni bora zaidi nao ni ule wa kumwagilia kwa matone na umwagiliaji huo tumeanza kuufanyia majaribio kule katika Chuo chetu cha Ukiriguru, Mwanza ambapo tunashirikiana na Kampuni inayoitwa *Burton Tanzania* katika kufanya haya mawili. Kwa nini tumekiweka kule? Kwanza, tunafikiri kwa kuweka karibu na Kituo kile cha Chuo itakuwa rahisi kwa wataalam wetu nao kuifahamu hii dhana ya *drip irrigation* au umwagiliaji wa matone. Lakini vile vile kufanya utafiti kujua jinsi maji tukiyatumia katika *drip irrigation* yanavyofanya kazi yake katika maeneo mbalimbali na kwa hiyo, kupata kile tunachotaka kukipata kwa manufaa ya kukieneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa ukitumia umwagiliaji wa kawaida wa *flat* una athari kidogo. Mbali ya kuwa unatoa maji hata kwa magugu yaweze kutumia maji hayo hayo lakini kwa *flat* vile vile inasaidia sana kueneza chumvi chumvi na hivyo kuleta athari na baadaye *flat irrigation* inaweza hata kuathiri ardhi yenyewe ikafa. Ipo pale lakini itakuwa haina uhai. Lakini *drip* ni tone linalokwenda kwenye mmea na

inahitaji maji kidogo tu na kwa njia hiyo unanufaika zaidi kuliko ukitumia *flat* ambayo inahitaji maji mengi sana. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge hasa wale wa Ukanda wa Ziwa, ambako kule tunafanya mazoezi au tuseme maonyesho, waweze kutembelea ile na tunaomba kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge, kujaribu kueneza hii dhana ya *drip irrigation* iweze kutufaa kwa kilimo kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametoa hoja kuwa Serikali itenge eneo dogo la umwagiliaji maji kwenye mabonde hususan Ziwa Victoria kwa Mito ya Manonga, Ruaha, Ruvu na Rufiji. Ni sahihi kwamba maeneo ya mabonde yanayoendelezwa ni madogo kama ilivyoainishwa na Mheshimiwa Mbunge lakini ni azma ya Serikali kuwa na maeneo makubwa kadri fedha zitakavyoruhusu. Bajeti ikiruhusu tutajitahidi kueneza maeneo makubwa zaidi ya miradi midogo midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge mwingine ameshauri kuwa ipo haja ya Serikali kuwekeza na kuhakikisha mabonde yote yanalimwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji kama vile mabonde ya Matomondo, Nzovu, Lumuma, Malolo, Lufusi, Msagali na anasisitiza kwamba, mabonde haya yakilimwa chakula cha kutosha kitapatikana na kuondoa njaa. Nasema ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, unakubalika hata hivyo Serikali imeshaanza sehemu za utekelezaji katika mabonde ya Lumuma na Msagali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba, kuwe na Wizara ya Umwagiliaji ili umwagiliaji uwe na shughuli kubwa nchini. Jibu ni kuwa Serikali imetambua umuhimu wa umwagiliaji maji mashambani na ndiyo maana kuanzia mwaka 2001 au 2002, Mheshimiwa Rais aliunda Kurugenzi Maalum ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi ndani ya Wizara ya Kilimo ili kuonyesha uzito wa shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu miradi kutofanyiwa utafiti wakati inaanzishwa na hivyo kusababisha miradi hiyo kufa mfano wa *COTACO* na *Lower Moshi*. Jibu ni kuwa hatuamini kuwa kila mara inatokea hivyo kwa sababu ukishafanya upembuzi yakinifu matatizo mengi unayakwepa. Kilichotokea kwenye Mradi wa *COTACO* ni kuwa wawekezaji walikuwa na matatizo huko huko walikotoka nchini kwao, kwa hiyo, walijitoa na walipojitoa mradi ule ukakwama lakini haikuwa azma yetu kufanya hivyo. Kwa *Lower Moshi* kilichotokea ni kuwa mradi ulipoanza ulikuwa na wakulima wachache lakini shughuli zilivyoongezeka na watu kutambua kuna faida kubwa wengi wamejiingiza huko na kuchukua maji kwa wingi kwa hiyo, *Lower Moshi* ina matatizo ya maji kwa sababu watu walishabikia mradi na sio kuwa haukufanywa kufuatana na taratibu za *feasibility study* kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine inayosema tuige mfano wa Misri katika matumizi ya maji kwa ajili ya umwagiliaji maji. Sisi tayari tumeanza na tulianza kabla ya kwenda Misri. Tulianza kabla ya Waheshimiwa Wabunge, mtupe hata hongera, haya yote tuliyoyataja huku ndani, ahaa, Misri si watu wamekwenda mwezi huu uliopita jamani. Sisi tumefika maeneo yote haya jamani, tunaomba mtupongeze jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, aliipongeza Wizara kwa kazi nzuri na matatizo yanatokana na ufinyu wa bajeti. Tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu nchi hii inahitaji fedha katika sekta mbalimbali ambazo zote ni muhimu bado, kwa hiyo, tulichogawiwa ndicho hicho kimetufikisha hapo. Uchumi ukiboreka tutaongeza shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge mwingine ameshauri kuwa Vijana wengi wanafanya kazi ya Umachinga. Hivyo kuwe na programu ya kuendeleza mabonde ya kilimo cha umwagiliaji maji ili nguvu kazi itumike. Tunasema hivi Wizara inajitahidi katika kilimo cha mazao yenye bei nzuri na hivyo kuvutia vijana kwenye umwagiliaji maji. Mfano, mbogamboga zina bei nzuri sana kama nyanya na kama ukiwa Kagera zao la *vanilla.* Mara ya mwisho tulipotembelea pale maonyesho ya wataalam wakulima wa *vanilla* wakati wa kikao cha *SADC* tuliambiwa au mimi mwenyewe niliambiwa kuwa kilo moja ya *vanilla* mbichi ni Sh. 60,000/= na kilo hiyo moja ukiuza *vanilla* kavu ni Sh. 300,000/=. Niliambiwa na wataalam waliohusika kule. Sasa hiyo sisi ndiyo maana tumeanza kulishughulikia zao hili ingawa halitakuwa na bei hii tunayosema kwa sababu inasadikiwa sasa hivi bei hii ni nzuri sana kwa sababu wazalishaji wakuu walipata majanga ya tufani. Kwa hiyo, zao liliharibika, kwa hiyo, kuna *shortage* ya zao hili. Lakini hata hivyo bei ya *vanilla* kila mara imekuwa juu zaidi kuliko mazao mengi sana ya mbogamboga. Kwa hiyo, wanaoweza kutoka Kilimanjaro na Kagera na kwingine, tujaribu kuona uwezekano wa kusukuma hili na kwenye Kitabu cha Mheshimiwa Waziri zao hili amelitaja ni namna moja ya kuvutia vijana wetu kushiriki kilimo chenye faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anashauri tuondokane na kilimo cha kutegemea mvua. Juhudi kubwa zichukuliwe katika kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Ushauri wa Mbunge unazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge mwingine amesema kukamilisha mradi wa umwagiliaji wa Mbebe na miradi mingine midogo ya Kikumbiro, Chitete, Mapogoro na Ilulu. Sasa kutokana na ukubwa wa Mradi wa Mbebe, Serikali Kuu imefanya ujenzi wa miundombinu ya shamba inayojumuisha mifereji na vigawa maji ili kuwawezesha wananchi kupata maji ya umwagiliaji. Hata hivyo, miundombinu mingine kama vile banuo itaendelea kujengwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Utekelezaji wa miradi mingine unaendelea chini ya utaratibu wa *DADPs.* Tunaomba Waheshimiwa Wabunge, hii miradi mingi ya *irrigation* msingoje tu mpaka inabuniwa juu kuletwa chini, tunapendekeza mtusaidie kwa kuhamasisha Halmashauri waiwasilishe miradi ya umwagiliaji katika kila Wilaya kutumia fedha za *DADPs* na fedha hizi zipo. Kwa mwaka huu kuna shilingi bilioni nne kwa shughuli hiyo. Kwa hiyo, tunawaomba wenzetu mwende kule muanze huko huko Wilayani kuiibua hii miradi tuweze kuihusisha na miradi mikubwa ya *Master Plan* ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge mwingine pia amesema kuongeza upatikanaji wa matrekta na kuanzisha *Tractor Hire Service Centres.* Ndiyo wazo hili ni zuri, tunakubaliana na hoja lakini tunasema hivi, *Tractor Hire Service* au Vituo vya Kukodisha Matrekta vinaanzishwa na sekta binafsi sio na Serikali. Kwa hiyo,

tunachoomba tutimize yale masharti ya mikopo. Si lazima uende *Exim,* kama tulivyosema kuna *SACCOS* na *SCCULT* wanaweza kusaidia suala hili. Ukishatimiza yale basi mkopo utatolewa na kwa kutumia mkopo kutoka pembejeo hapo tunaweza kununua na kuanzisha hizo *Tractor Hire Service.* Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge karibuni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine, Mheshimiwa Mbunge ameomba Mheshimiwa Waziri na timu yake awatume Mafisa Kilimo Kilwa ili wakaone Bonde la Mkoma ambalo lipo Tarafa ya Njinjo, Kata ya Mitole. Bonde hili lilikuwa linalimwa na Kanisa la *Roman Catholic* la Kipatimo ambalo limekuwa linavuna zaidi ya tani kadhaa za mazao. Tumesikia, tutatuma wataalam na tukiona kama tumezidiwa usisahau kutukumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge mmoja amezungumzia kuhusu Mradi wa Matuli. Mradi wa Matuli tunachotoa ushauri ni kuwa, mradi huo upitishwe katika Halmashauri ya Morogoro kama *DADP.* Halafu kuna matreketa, narudia yale yale kusema suala la matrekta mkiona hayamo kwenye Wilaya ni kwa sababu moja tu, hatujawahamasisha wananchi kupitisha kwa Vyama vya Ushirika. Tafadhali sana matrekta yasikosekane eti kwa sababu ya Benki fulani fulani. Tunapendekeza tujitahidi tunavyoweza ingawa kweli patakuwa kidogo na ufinyu wa bajeti kwa sababu maombi yakitoka Wilaya zote hizi kwa mara moja haitakuwa rahisi kutekeleza maombi hayo. Lakini tutajitahidi kadri tutakavyoweza suala la kutumia wanyamakazi na suala la kutumia matrekta katika kilimo ndio njia itakayosaidia ikijumuisha na umwagiliaji maji katika kupanua kilimo na tija nchini. Waheshimiwa Wabunge tunaomba mtuunge mkono. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nijaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa hapa Bungeni na namshukuru sana Naibu Waziri kwa kunisaidia kujibu nyingi sana kati ya hizo. Hoja hii kwa kuwa sisi wote tuliopo humu ndani tunahusika na kilimo kwa karibu sana, imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 24 kwa kusema hapa Bungeni na 41 kwa kuandika. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea hapa Bungeni ni Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Khamis Awesu Abood, Mheshimiwa George Francis Mlawa, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Dr. Chegeni Raphael Masunga, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Philip

Magani, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa Gwassa Sebabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Sijamini Mohammed Shaame, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Alhaj Abdallah Shaweji, Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Janet Mashelle, Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri na Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Hamisi Jumanne Nguli, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Stanley Kolimba na Mheshimiwa Diana Chilolo. Waheshimiwa Wabunge mliochangia nawashukuru kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna yeyote ambaye amechangia kwa kusema au kwa maandishi ambaye sikumtaja, naomba anileteе karatasi hapa nita-*interrupt* mazungumzo yangu ili niweze kumtaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yaliyoelezwa hapa Bungeni ndiyo *concerns* za Serikali karibu yote. Serikali ingependa iweke fedha nyingi inavyowezekana katika kilimo kama tungekuwa nazo. Mimi naomba niseme kwa dhati kabisa, Serikali imekuwa ikijitahidi sana kukipa kilimo umuhimu katika ku-*allocate resources* lakini tatizo ambalo tunalipata ni kwamba, mambo yanayohitaji hizo fedha kidogo ni mengi. Kwa mfano, kilimo kinasaidiwa na barabara. Mheshimiwa John Magufuli, akijenga barabara basi mimi nitahamisha mazao. Mwaka huu tunategemea kwamba, uzalishaji wa pamba utakuwa mara mbili ya mwaka2003, kama hatuna reli, kama Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya hana mabehewa ya kubeba hiyo pamba kutoka Mwanza na Shinyanga kuipeleka Dar es Salaam, tutakwama. Kwa hiyo, haya mambo yote kwa pamoja ndiyo yanayochangia katika Sekta ya Kilimo. Barabara ziwe nzuri na reli ifanye kazi sawasawa, watu wawe na afya na wawe na elimu, ukinipa haya yote kwa pamoja *then* kilimo kinakwenda vizuri, sasa hata kukua huko kutaonekana kwa urahisi zaidi. Lakini haya mengine yakiwa kikwazo, basi hata kilimo nacho kinakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naishukuru sana Serikali kwa jitihada zinazofanyika lakini ninaungana nanyi kuomba kwamba, kadri itakavyowezekana *resources* ziongezwe katika kilimo ili tuweze kuwekeza kwa ukubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme moja linalotuhusu sisi wenyewe maana sisi ndiyo viongozi tuliochaguliwa na wananchi na kupewa dhamana ya kuwasimamia. Linalotuhusu sisi na viongozi wetu walioko kule Mikoani pamoja na *Extension Officers,* ni udhaifu mkubwa sana upo katika usimamizi wa kilimo sasa hivi. Kumetokea ugonjwa wa kukaa ofisini badala ya kwenda kwa wananchi kuhimiza na kusimamia kilimo. Ninataka niseme kwa dhati kabisa, maofisi mengi wanayokaa watu hata kazi za kufanya hazipo. Kwa mfano, Afisa Kilimo wa Wilaya ukiniambia ana kazi za kumshindisha ofisini kwa siku nzima mimi nakataa. Niliwahi kuwa Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya na nilikaa sana Kigoma kwa Waha wenzangu na ilikuwa saa nne ikifika tunatoka tunakwenda vijijini kwa sababu kazi za karatasi zinakuwa zimekwisha, ukipata barua moja, mbili, umepata barua nyingi sana siku hiyo. Sasa naomba turudie utaratibu wa kwenda kwa wananchi kuhimiza maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote hapa tumelalamika sana juu ya Maafisa wa Kilimo kutokwenda vijijini. Lakini Afisa Kilimo angejua kwamba, Mkuu wake atakuja kumtembelea angehakikisha kwamba, yuko kijijini anafanya kazi. Lakini anakaa mwaka mzima hamwoni anajua kwamba *actually* yupo katika utawala binafsi na yeye anafanya anavyoona inamfaa. Naomba tuondoe huu udhaifu kwa sababu hauhitaji fedha za kigeni, hauhitaji hata juhudi maalum, magari tunayo na mafuta siku hizi Serikali inatupa kwa wingi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye baadhi ya hoja na tumekubaliana na Mheshimiwa Pius Mbawala kwamba, mimi nitashughulikia masuala ambayo yanagusiagusia sera zaidi. Naomba nirudie tena kumtambua Mheshimiwa Mizengo Pinda kwamba, alichangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mawili yalitokea hapa wengine walisema *speech* yenyewe imekaa ovyo ovyo, inalalamika lalamika badala ya kujibu hoja. Sehemu moja inaeleza kazi tulizofanya na mafanikio tuliyopata na matatizo tuliyopata. Sasa ukiangukia kusoma yale matatizo utaona tunalalamika. Lakini ukisoma zile kazi tulizofanya utaona kwamba, kuna mafanikio kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri hapa. Hilo sitaki kulizungumzia kwa sababu inategemea. Kwanza, vitabu vyenyewe viligawiwa wakati nasoma *speech* hapa Bungeni watu hawakupata nafasi ya kuvisoma. Naomba mwendelee kuvisoma kwa sababu vina maelezo mengi sana kuhusiana na sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lilisemwa vilevile kwamba, hatuna mpango wa kilimo na mimi naomba niwakumbushe kwamba hapa Bungeni tulifanya semina ya kujadili *Agricultural Sector Development Strategy* na ilikuwa tarehe 28 Juni, 2003, ilikuwa wakati wa Kikao cha Bajeti, tukapitia ule mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo, tukakubaliana kwamba, unafaa na mkakati huo unazungumzia matatizo yote tunayoyazungumzia hapa. Ukuaji mdogo wa kilimo, kilimo cha kutegemea jembe la

mkono hakitupeleki mbali, umuhimu wa umwagiliaji maji mashambani na kadhalika. Sasa unaweza ukasema ule ni mkakati siyo *modernization*, lakini ule mkakati kazi yake ni *modernization* labda ucheze tu na Kiingereza, huyu aite mkakati na huyu aite Programu ya *modernization.* Kwa hiyo, tunayo *strategy* ya kilimo na baada ya *strategy* sasa tuna programu za kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi napenda niwakumbushe kwamba, hotuba yangu nilipoiwasilisha hapa nilimwambia kwamba, mipango yote sasa ni lazima iibuke kutoka kijijini ipande mpaka ifike kwenye Wilaya ndiyo itengeneze *DADPs* ukianza kwa utaratibu mwingine wowote umepotea njia. Katika programu hizi tunazozingumzia zinakisiwa kwamba, zitahitajika shilingi bilioni 617, asilimia 75 inatakiwa iende moja kwa moja kijijini, asilimia 20 ibaki katika ngazi ya Taifa kushughulikia masuala ya sera, masuala ya kisheria, masuala ya kiutawala na asilimia 5 ishughulikie masuala yanayojulikana kama masuala mtambuka ambayo ni masuala ya mazingira na masuala ya UKIMWI, masuala ya *gender* na masuala kama hayo. Kwa hiyo, kwa kweli mipango tunayoiandaa sasa hivi ni mipango ya kuendeleza kilimo kwenye Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PADEP* imebadilishwa nataka nimhakikishie mwenzangu, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, ambaye naona bahati mbaya hayupo hapa kwamba, Wilaya yake ya Mwanga itaingizwa katika *PADEP* mwaka huu. *PADEP* inabadilishwa kufuata mfumo huu kwamba itatekelezwa kutokana na mipango itakayoibuka kutoka kwa wananchi. Halafu tuna ule mwingine tunakopa kutoka *ADB dollar* za Kimarekani 57 milioni nao umefuata mfumo huo huo. Halafu Wahisani wote sasa wanarekebisha mipango yao kufuata mfumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema lazima tuwe maskini jasiri. Katika mipango hii kama nilivyoeleza jana, moja ya *component* ni kutoa ruzuku za mbolea kwa asilimia 50 pamoja na madawa na vifaa vya kulimia, vifaa ambavyo ni *capital goods* asilimia 80. Kwa hiyo, mkulima anatakiwa achangie asilimia 20 tu kwa nguvu zake, kwa fedha kidogo wakati mwingine na kwa kutumia *materials* ambazo zinapatikana katika eneo lake. Ndiyo maana tuko *confident* kwamba, tukienda hivi tunavyokwenda mwaka 2005 na mwaka kesho 2006, tukaendelea hivyo hivyo katika miaka michache ijayo tutaanza kuona mabadiliko makubwa kabisa. Sasa ninataka niwahakikishie kwamba, mpango upo. Lakini lazima tuelewe kwamba, mpango upo ndiyo tuuone maana kama hatukubali kwamba upo tutautafuta wakati *actually* na vile vitabu tuligawa na kama kuna aliyepoteza aseme nimpe kingine. Hii ndiyo *strategy* ya kilimo na sasa tunatakiwa tuandae *programmes* kutoka Wilayani na Wilaya zimekwishakutana na zimeandaa programu zao na ndizo zitakazogawiwa fedha alizozungumza Naibu Waziri shilingi bilioni 4 mwaka huu. Tuko *confident* kwamba, mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililojitokeza hapa ni suala la *STABEX* lakini *component* ya *STABEX* inayozungumzwa ni *component* ya barabara tu. Sasa mimi ningependa niombe kwamba, hii *component* ya barabara izungumzwe wakati Wizara ya Ujenzi itakapowasilisha hotuba yao hapa na mimi nitasimama kusaidia kujibu. Kwa

sababu sasa tunazungumza kilimo na tunataka tuzungumzie na ujenzi wa barabara hapo hapo, nafikiri tunataka tu kupotosha mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya asipozungumzia *STABEX* kule nyumbani hawamsikii. Kwa hiyo, anajitahidi kweli kuizungumzia *STABEX*. Sasa wakati watakapowasilisha bajeti ya Wizara ya Ujenzi hapa, mimi nitaomba nafasi nichangie ili nitoe maelezo kikamilifu kabisa kwamba, nini tunachofanya na hii *road component* katika *STABEX*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niwambie kwamba, hili suala la kuteua mtaalamu wa kuandaa huu mpango ni suala ambalo liko katika makubaliano kati ya Serikali na *EU* na kifungu chenyewe kinasema hivi na kimeandikwa kwa Kiingereza: *"A consultancy to be funded under this FMO is to assist the identification and privatization of Regional Roads to be included in the Project."*

Kwa hiyo, hili suala la kumteua huyu mtaalamu ni suala la lazima. Lakini naomba tukubaliane barabara siyo kusema tu ni barabara kutoka Dodoma mpaka Manyoni ni lazima uonyeshe vilevile kwamba ni nini kitachofanyika kwenye hiyo barabara na gharama gani zitakazohitajika. Sasa ukimwachia Mkurugenzi wa Wilaya ambaye pengine hata *Engineer* hana, afanye kazi hiyo, kazi atakayoileta haitawezekana ku-*fund* na haitaweza kutoa *contract* za kujenga. Ndiyo sababu anatafutwa mtaalamu wa kusaidia ili hiyo kazi iweze kufanyika kwa ufanisi zaidi. Barabara zitakazohusika ni barabara za kwenye maeneo ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Waheshimiwa Wabunge wapige simu kule nyumbani kuuliza kama huyu mtaalamu ameshafika ili kama ameshafika basi aonyeshwe hizo barabara ambazo wanafikiri zingepewa kipaumbele. Lakini fedha zipo na tumegawa makabrasha ya kuonyesha kwamba hizi fedha bado zipo. Huyu mtaalam aliteuliwa kwa utaratibu wa kawaida kabisa wa *tender* na kwa hiyo hakuna wasiwasi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nigusie kidogo hili suala la umwagiliaji maji. Kuna hoja zinazopingana zilitolewa hapa. Waheshimiwa Wabunge wengi sana hata wale waliosema kwamba hakuna lililofanyika, wanarudi nyuma wanasema tunashukuru sana kwa mradi wangu fulani uliotekelezwa. Lakini wengine wamesema hizi fedha kidogo tunazopata twende kwenye mradi mmoja kama ule Mradi wa Ngono, nasikia wamebadilisha jina wanaita Nkenge siku hizi tukautekeleze huo ili uonekane. *(Makofi)*

Sasa mimi nataka kusema hapa kila mtu anakula nyumbani kwake. Kwa hiyo, lazima mradi uwe karibu na pale walipo watu, hii miradi inatusaidia kusimamisha maji ili wananchi wapate maji ya kunywa. Kwa hiyo, huwezi kwenda kufanya mradi mmoja ukatatua tatizo hilo. Huu mradi unatusaidia kuzalisha chakula watakachokula watu kijijini kwao ku-*improve food security* pale kijijini. Kwa hiyo, haiwezekani ukatekeleza mradi mmoja ukawa umetatua tatizo la Watanzania, utakuwa umetatua tatizo la kundi fulani tu katika kijiji fulani pengine ama katika Kata fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, ameniambia kule kwake hakuna mradi nimemwahidi nitamtafutia mradi mmoja. Sasa hivi ukisikiliza na ukazungumza na Waheshimiwa Wabunge walioko hapa kila mmoja atakwambia ana mradi uliotekelezwa kule kwake na ukatatua tatizo la msingi la maisha ya wananchi na ndilo tulilotaka. Nimetembelea Ismani na Mheshimiwa William Lukuvi nikakuta miradi miwili, mitatu, iliyojengwa ambayo ime-*transform* kabisa maisha ya watu sasa hivi mambo ya njaa hakuna, mambo ya matatizo ya maji hakuna wale wananchi wanaishi kama raia huru wa Tanzania sasa hivi. Sasa mimi nafikiri tukubaliane hilo kwamba, tujaribu kujenga miradi hii kila mahali panapowezekana ili wananchi wengi iwezekanavyo wafaidike na hii miradi.

Baada ya kujenga *Lower Moshi* moja kwa shilingi bilioni 6 halafu Mwenga pale kwa ndugu yangu, Mheshimiwa Christopher Wegga, ambako nako kuna mradi wa shilingi bilioni 6. Sasa zile shilingi bilioni 6 tungeweza kujenga miradi midogo pengine 60 ambayo ingetusaidia kuhudumia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile nisahihishe *concept* moja hapa ambayo ina matatizo kwamba kilimo kitakachotuokoa ni cha umwagiliaji ukiongeza pekee yake umefeli mtihani. Kwa sababu kilimo kitakachotuokoa ni kilimo cha mvua tunachotumia pembejeo vizuri, tunachotumia mashine vizuri halafu kikiwa *supplemented* na kilimo kikubwa cha umwagiliaji. Katika mpango wa mwaka kesho, tumeomba na tunaomba mtuidhinishie, jioni hii, shilingi bilioni 7.244 kwa ajili ya kazi hii ya kusambaza pembejeo za kuongeza tija katika kilimo. Ile Mikoa mnayosema kwamba, mvua zinapatikana bila kusita tunataka ipate mbolea nyingi kabisa, wazalishe kwa wingi kabisa, tuache kununua kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema wakati ule *South Africa* ikiwa imepamba moto akasema: “Hakubaliani na wale Makaburu wa *South Africa* lakini akiwaambia watu wake wanakufa kwa njaa atafunga safari kwenda *South Africa* kununua chakula.” Sasa tusijifikishe hapo, tujaribu kutumia *resources* tulizonazo kwa kuhakikisha kwamba, tuna chakula cha kutosha na hakuna matatizo hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mariam Mfaki na Mheshimiwa Lucas Selelii na wengine waliozungumzia juu ya tatizo la jembe la mkono. Kinachotukwamisha ni jembe la mkono, kwa hiyo, mashamba madogo tunayolima kwa familia ni *zero point two hectares* mpaka *two hectares*. Kama alivyoomba Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba na mimi niombe mtupe *credit* kwa kuanzisha utaratibu hata wa kununua matrekta japokuwa siyo mengi sana kwa mwaka. Kwa sababu ni *recognition of the fact* kwamba, jembe la mkono halitupeleki mahali. Kuna matrekta 6,000 mabovu katika nchi hii ambayo yangetengenezwa tungekuwa na matrekta 6,000 yanayolima na baadhi ya matrekta tunaambiwa yana matatizo madogo na mengine yamekwisha matairi na mengine ni *injector pump* imekufa, ndiyo maana tukaanzisha hii miradi tujaribu kufufua hayo matrekta yaliyopo na bahati nzuri yanafufuka kwa wingi kidogo na wakati

huo huo kununua matrekta mapya ili yatusaidie kuondokana na jembe la mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungekuwa na uwezo tungetaka katika muda mfupi uwezekenao, tuachane kabisa na kulima ardhi kwa kutumia jembe la mkono, lakini inahitaji *resources* ambazo hatuna. Tumeomba sana *Private Sector* zitununulie matrekta zilete ziyasambaze kwa sababu wananchi wako tayari kuyanunua na kuna vyombo ambavyo viko tayari kutoa mikopo kwa ajili hiyo. Kwa hiyo, tunaomba sasa hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limejitokeza hapa ambalo ningependa kuligusia kidogo ni hii mbolea ya ruzuku. Mwaka 2003 kwa mara ya kwanza katika zaidi ya miaka kumi Serikali iliamua kutoa ruzuku na niseme kwa dhati ruzuku kidogo kwenye mbolea ili kufanya mbolea isiwe na bei kubwa kiasi ambacho mkulima hangeweza kuinunua, ndiyo hicho alichokiita Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, maskini jeuri. Serikali ikasema tutatoa ruzuku na kama kuna mtu anataka kutuuliza tutamjibu. Bahati nzuri hakuna mtu aliyetuuliza kwa sababu tulitumia fedha zetu tukatoa ruzuku katika mbolea. Matokeo yalikuwa mazuri sana, wananchi waliongeza sana utumiaji wa mbolea. Lakini ni mara ya kwanza tulifanya jambo hili kabla ya hapo tulikuwa hatuna utaratibu wa kutoa ruzuku na kwa hiyo tulikuwa hatuna utaratibu wa kufuatilia upelekaji wa mbolea mikoani, kwa hiyo, yakatokea matatizo kidogo, ilipofika mwezi Machi ile mbolea ya ruzuku ikawa imekwisha, wajanja wakaenda huku nyuma kupandisha bei ya mbolea wakaanza kuuza mfuko mmoja kwa Sh. 20,000/= mpaka Sh. 25,000/=.

Lakini kama ni ku-*score a point, we scored a point* kwamba, tukipunguza bei za mbolea wananchi wataongeza matumizi ya mbolea na wataongeza uzalishaji. Ndiyo sababu mwaka huu Serikali itakatenga shilingi zaidi ya bilioni 7 kwa ajili hiyo ili tuweze kutoa mbolea kwa wingi zaidi na tujaribu kutoa mbolea katika Mikoa yote ambayo inapata mvua za uhakika. Sasa mimi nafikiri haya ni maendeleo mazuri. Ni maendeleo mazuri kwanza kwa sababu tumerudia utaratibu mzuri na pili kwa kuwa utaratibu huo sasa utapanuliwa kuwafikia wakulima wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeulizwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba, je, hii mbolea ni kwa mahindi tu, nikasema hapana, kwanza ni vigumu sana kwenda kusimamia na kuhakikisha imetumika kwenye zao gani. Kwa hiyo, hii ni mbolea inatakiwa itumiwe kwenye kilimo kama unalima mahindi weka mbolea, kama unalima pamba wekea mbolea, kama unalima zao lolote litilie mbolea ili kuongeza uzalishaji ili uweze kupata mazao mengine zaidi na uweze kupata mapato makubwa zaidi. Kwa hiyo, hakuna *restriction* juu ya hilo.

Lakini kuna dhana inajitokeza hapa kwamba, tunaweza kutumia samadi badala ya mbolea za chumvichumvi. Mimi nataka kuwaambia samadi ni nzuri sana, ina-*improve* sana hali ya udongo, inafanya udongo unakuwa mzuri na unashika maji na wadudu wanaishi ndani yake ambao wana manufaa kwa mimea. Lakini hebu niambie hiyo samadi nyingi namna hiyo tutaipata wapi ya kutosha kuweka kwenye mashamba

makubwa. Kwanza, kule Mwanza ile samadi wanaichoma moto na ndiyo wanatumia kama kuni kwa hiyo, kuna *problem.* Kuna taarifa nilikuwa nasoma hapa, imeandikwa na *President* wa *Sasakawa Global 2000,* anasifu sana matumizi ya mbolea lakini anaendelea kusema kwamba, kuna udongo ambao kama hukutia *phosphate,* hukutia *potassium,* huvuni kitu, anasema hata magugu hayaoti. Kwa hiyo, lazima tutumie mbolea za chumvichumvi na kama tuna samadi tuongeze samadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanasema kule Ulaya kuna watu wasiokula vyakula vilivyopandwa kwa kutumia mbolea, hawa ni watu walioshiba. Nataka niwaambie kuna *scientists* wengi sana humu ndani, aniambie *scientist* mmoja kwamba, nimpe mhindi uliotiwa mbolea na ambao haukutiwa mbolea aonyeshe tofauti yake. Ile mbolea haiingii kule ndani kama *Urea* wala haiingii kama *TSP*, ikishaingia kwenye ule mmea inakwenda kubadilishwa, inafungamana na *chemicals* nyingine za mmea inakuwa ni sehemu ya mmea na wewe ukila unapta kutoka kwenye ule mmea na kusaidia na wewe kujenga mwili wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu kubwa sana tunatumia mbolea kidogo mno, tunatumia kilo sita tu kwa hekta. India wanatumia kilo 103 na huyu mtaalam anasema kabla hatujafikia matumizi ya mbolea ya India tutakuwa na njaa miaka yote. Anasema, kama unatumia chini ya kilo 103 kwa hekta za mbolea, siyo ule mfuko wa *Urea* una *only forty six percent Urea,* kwa hiyo, mifuko miwili inakupa *forty sixy kilograms*, sasa anazungumzia kilogramu 103 za *Urea* siyo kilogramu 103 za mfuko na anakwambia bila kufikisha hapo nchi yako itaendelea kukabiliwa na matatizo ya njaa. Karibu nchi zote za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara pamoja na *South Africa* tunatumia chini ya kiwango hicho. Ukienda Ulaya wanatumia zaidi ya kilogramu 250, ukienda katika hizi nchi mpya na akina China wanatumia karibu kilogramu 300 na zaidi ambapo zamani walikuwa wanategemea sana *organic fertilizers.* Jitihada zetu lazima ziendelee kupata mbolea kwa wingi zaidi na kuitumia kwa ukamilifu zaidi. Mtu anayesema tutumie mbolea kwa chini zaidi hapana, anatudanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kidogo suala la *Exim Bank,* ambalo limezungumzwa sana hapa hata tukaulizwa *Exim Bank* ni ya nani? Mimi kwa kweli sijui *Exim Bank* ni ya nani? Lakini najua Mkurugenzi Mkuu wa *Exim Bank* anaitwa Mwambenja, ni mama mmoja wa Kinyakyusa, hodari sana. Hii ndiyo Benki pekee inayowekeza katika kilimo sasa hivi. Pamoja na matatizo yake mengine yote, *it is the only bank* ambayo inawekeza katika kilimo, benki nyingine zote haziwekezi katika kilimo. Tulipokuwa tunatafuta mabenki ya kukopesha hizi fedha tulikwenda kwenye mabenki yote *NMB, NBC, CRDB,* Akiba Benki na Benki ya Posta, hakuna aliyekubali. Hawa *Exim Bank* walikubali kwa sababu walikuwa na uzoefu wa kupitisha mikopo iliyokuwa inatumika wakati ule kwenye korosho na kwenye shughuli nyingine, wakasema wana uzoefu, hii kazi wataifanya. Kwa hiyo, kwa kuwa hatukuwa na *option* tukawachukua *Exim Bank* na tukawachukua *Kilimanjaro Cooperative Bank,* ambao walikubali lakini wanasuasua sana sasa hivi kwa kweli katika fedha walizopewa ndiyo walikopesha kidogo kuliko wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni na nje ya Bunge, kutokana na matatizo ambayo wamesema wanayapata kupitia huku, tukapanua wigo ili tupate watu wengi zaidi wa kuwashughulikia hizi fedha. *SCCULT* mwaka 2003 waliongoza kwa kutoa mikopo kwa vikundi vya *SACCOS* 83. Mheshimiwa Abu Kiwanga, alikuja akaniambia amekwenda kule wamemkwamisha nikamwambia rudi kwenye *SACCOS* yako, pitisha mikopo yako kule achana na hawa. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba, yale matrekta aliyoyazungumzia atayatengeneza kwa mkopo atakaochukua kutoka kwenye *SACCOS* yake na siyo kupitia mahali ambapo anaona anaendelea kukwama. Benki ya Mufindi tumeiomba ihudumie Iringa, ihudumie Mbeya, ihudumie Ruvuma, ihudumie Rukwa mpaka tutakapopata chombo kingine cha kuhudumia maeneo hayo. Kwa hiyo, hamna haja ya kufunga safari kwenda mpaka Dar es Salaam. Mheshimiwa Maria Watondoha, ameniandikia hapa akaniambia kule wanataka nyumba za Dar es Salaam na Arusha, sasa kila mmoja ataende kujenga Dar es Salaam na Arusha, si ile Miji itajaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba kwa dhati kabisa kwamba, kama mnataka kukopa pitieni kwenye Vyama vyenu vya Kuweka na Kukopa, pitieni kwenye Vyama vyenu vya Ushirika, pia kwenye *Community Banks* zilizo karibu nanyi na mtapata mkopo kwa masharti mtakayoelewana na hao wakopeshaji. Mradi tukubaliane tu kwamba, kila utakapokwenda kuna masharti yatatofautiana labda kwa utaratibu wa kuyasimamia. Lakini masharti yatakuwepo maana moja ya sharti lazima urudishe huo mkopo katika kipindi mtakachokubaliana. Lakini hii ya kulalamika juu ya *Exim Bank,* naomba tuachane nayo na sisi tutakwenda hatua kwa hatua baadaye tuta-*withdraw*. Kwanza, tuna mpango wa kuanzisha benki yetu ya kilimo, ikishaanza mifuko yote hii itakwenda kwenye Benki ya Kilimo na hakutakuwepo na matatizo ambayo yanatusumbua sasa hivi. Hili ni jambo moja ambalo limetusumbua kwa muda mrefu sana na ningeomba tulifikishe mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, aliniandikia juu ya tatizo la kilimo cha pamba kwenye Mikoa ya Kusini hususan Mkoa wa Mbeya. Nimekusanya kumbukumbu nyingi sana na nilichelewa kumjibu kwa sababu nilikuwa nakusanya kumbukumbu zinazohusiana na tatizo hili tunazo zimekamilika. Tumetafuta wataalam wanaohusika, tumetafuta nini tulichokuwa tumefanya maana mwaka 2003, kipindi kama hiki tulifanya kikao hapa tukaagiza kwamba, tutume ujumbe kwenda kwenye nchi nyingine Kusini mwa Afrika zikaangalie hali ilivyo halafu watuletee ripoti. Tumeshatuma ile Tume akiwemo Mheshimiwa Njelu Kasaka, akiwemo Mheshimiwa Dr. James Wanyancha na wataalam, wakaenda Afika Kusini wametembelea kule wamerudi wanajua sasa kilimo cha pamba ya kawaida na *BT Cotton,* tutafanya semina ya wadau wa pamba wakati huu tukiwa Bungeni, tutamwomba Mheshimiwa Spika, atutengee muda tupitie masuala yote yanayohusiana na tatizo hili la kilimo cha pamba. Halafu tukubaliane ni njia gani tufuate kwenda mbele kutoka hapo. Tukiwa tumeelewa wote kwa usawa juu ya tatizo hili na madhara yake kwa uchumi unaotegemea pamba. Kwa hiyo, naomba tukubaliane hivyo kwamba, tutaandaa hiyo *workshop,* tutakaa wote tutazungumza, tutakubaliana.

Ninasema hivi kwa sababu hii nchi inayoitwa Tanzania ni nchi yetu sote. Mimi nina hakika sisi sote tuna *interest* zinazofanana na nchi yetu tungetaka iendelee, isonge mbele, iwe *middle income country,* baadaye iwe nchi ambayo imeendelea na watu wa kufanya hayo ni sisi ambao itabidi tukae hapa tufanye maamuzi ya kutuwezesha kuelekea huko. Kwa hiyo, hilo tutafanya halafu tukishafanya kama ikibidi tutarudi hapa Bungeni kuja kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu.

Kuna mambo mengi ambayo tungeweza kuyazungumzia lakini napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, ushauri wote walioutoa tumeuzingatia na tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba, unatekelezwa. Lakini ninaomba niwaahidi kitu kingine kwamba, hoja zote mlizouliza hapa tutaleta majibu kwa maandishi ambayo yatafafanua kwa undani kila *issue* inatokana na nini, ni nini kinachofanyika na ni *resources* gani tunazohitaji. Tutawajibu kikamilifu kadri itakavyowezekana ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuelewa kwamba, ni kitu gani ambacho tunajaribu kufanya katika Serakali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimebakisha kama dakika mbili, tatu hivi, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liniidhinishie fedha ili niweze kwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. Ahsante. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**Matumizi ya Kawaida**

**Fungu 43 - Wizara ya Kilimo na Chakula**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ...Sh. 1,181,844,200/=

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kushika kifungu 1001 - Mshahara wa Waziri. Ningependa nipate ufafanuzi kuhusu ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji kule Same ambaye Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati akijibu swali Na. 106 aliahidi kwamba, ingekuwepo katika bajeti. Sasa ningependa kufahamu kama ipo katika bajeti au vipi?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijibu swali hapa Bungeni juzi, tukaeleza kwamba, iwapo litaletwa kupitia kwenye mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya tutalishughulikia. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa John Singo kwamba, tutatuma wataalamu kwenda kushirikiana na wataalamu wake kuandaa makisio hayo, tutafuta fedha za kutekeleza. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri wakati akijibu swali alishakiri kwamba, ilishaletwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2004/2005. Sasa ninashangaa Mheshimiwa Waziri analirudisha tena huko lilikotoka!

**MWENYEKITI:** Wanakwambia zipo fedha, anachotaka Mheshimiwa Waziri ni ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Endapo kama makisio haya ya gharama za kufanya hiyo kazi yameshaletwa tutayatumia hayo hayo kushughulikia hiyo kazi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwamba atatumia makisio hayo hayo yaliyoletwa.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashika kifungu 1001 - Mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa hoja ya *Exim Bank* imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na hoja niliyompelekea mimi sasa hivi imesema wenzetu hawa wanataka hati za nyumba au kitu chochote kisichohamishika kwa Dar es Salaam au Arusha. Swali langu kwake lilikuwa, je, wakulima wa nchi hii wako Dar es Salaam na Arusha tu, wakulima wa sehemu nyingine ya nchi hawana haki ya kupewa mkopo? *(Makofi)*

La pili, nilisema katika mchango wangu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba, tuambiwe fedha tulizotenga mwaka wa fedha uliopita zimebaki kiasi gani na zimeweza kukopeshwa kwa watu wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikihitimisha hoja yangu hapa, nilizungumzia na nikagusia hii hoja aliyonitetea Mheshimiwa Watondoha. Ni kweli kwamba, wakulima wa nchi hii hawako Dar es Salaam na Arusha peke yake. Lakini naomba nikumbushe kwamba, huu mfuko unakopesha *stockiest* wa *input* na sio moja kwa moja wakulima. Hata hivyo, tumeweka vyombo vingine vingi vya kukopesha ili kuondoa hili tatizo lililopo wakati tukifuata sasa utaratibu wa kisheria kuona nini tufanye na hii Benki ambayo haitakiwi kukubalika kwa wakulima.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nifahamu *stockiest* wa Mkoa wa Lindi hao watakaonunua pembejeo, mimi nilidhani hata matrekta yako kwenye Mfuko huo huo na wananchi wa Mkoa wa Lindi watapata kutoka Benki gani?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwishakueleza kwamba, mikopo hii inaweza kupitia kwenye Vyama vya Kuweka na Kukopa, inaweza ikapitia kwenye Vyama vya Ushirika, inaweza kupitia kwenye vikundi vyote ambavyo vina *registration.* Nilieleza hapa kwamba, *SCCULT* imepitisha mikopo

83 ambayo ni mingi kuliko iliyopitishwa na chombo kingine chochote. Lakini haya matatizo yaliyopo nitayashughulikia na kuhakikisha yanaondoka ili tutakapokutana hapo mwaka 2005 yawe hayapo tena.

**MHE MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Lakini ndugu zangu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara mpaka sasa hawajui wapi pa kwenda?

**MWENYEKITI:** Ndiyo fedha tunapitisha sasa watajua pa kwenda.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize maswali machache ili na mimi nihoji hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula nikizingatia kifungu Na. 1001 - Mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika kujumuisha hapa sasa hivi alisema kwamba, anawaomba maafisa ugani waende vijijini kufundisha na kuelimisha wakulima. Namwuliza kama Waziri anawaomba ama anawapa amri waende. Hilo ni moja. *(Makofi)*

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi alitumia mfano hapa kwa kuwapa Wakuu wa Mikoa amri waende wamletee ripoti tarehe 30 jinsi fedha za pensheni zilivyokuwa zinatumika. Sasa yeye anawaomba au anawapa amri na hilo liwe ni changamoto kwa Mawaziri wote watoe amri wasiombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili katika hotuba yake ukurasa wa 59 na 119 ili mshahara wake nimpe kwa kazi hii nzuri ananiambia ya kwamba, tuangalie kifungu (c)(i) - Mipango ya Maendeleo ya kilimo ya Wilaya ni *Euro* 6,308, 693. Lakini pia chini yake kabisa amesema mchanganuo wa fedha hizo imeonyeshwa kwenye kiambatanisho Na. 8, tuangalie kiambatisho Na. 8 Mheshimiwa Mwenyekiti. Kinasema ni *FMO STABEX Coffee 1994/99*. Hapa angalia chini *District Based Programmes, allocation* ni 4,308,693, kinyume na jinsi alivyosema kwenye Wilaya. Lakini pia kwenye matumizi yake anasema *total euro*, anasema *committed zero, no commitment for this money.* Anasema *Disbursed* ni *zero.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fedha zote hizi hazina mwelekeo na amezi-*allocate,* amezi-*allocate* kwa nani na zifanye kazi gani. Naomba majibu.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nilikuwa nazungumzia viongozi na watumishi kwenda vijijini kuhimiza kilimo. Sasa watumishi ninaweza nikawaagiza, lakini sina uwezo wa kumwagiza Mkuu wa Mkoa. Kwa hiyo, nilikuwa nawahimiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Makatibu Tarafa, Maafisa Watendaji wa Kata na *Extension Officers* tuondoke kwenye maofisi yetu twende tukahimize kilimo vijijini. *(Makofi)*

Hili la *STABEX* alilouliza Mheshimiwa Mstaafu Major Jesse Makundi, nafikiri anafahamu jibu. Kwa sababu hizi fedha, *allocated* maana yake zimetengwa kwamba zipo, *committed* kwamba hakuna kiasi ambacho kimeshapangiwa kazi. Zilizotumika hakuna kwa sababu hazijatumika. Kwa hiyo, hizi fedha zipo zinasubiri kutumiwa na *DADPs* kugharamia Mipango ya Maendeleo ya Wilaya ya Kilimo.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo sikatai. Lakini amesema kuwa, Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani ni 6,308,693 huku kwenye jedwali anatuambia 4,000,000. Hizo 2,000,000 zimepelekwa wapi? Potelea mbali. Sawa huku mipango bado lakini 2,000,000 ziko wapi, *where is the money? (Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nadhani unamwelewa?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Nilikuwa namwomba anisaidie tena hii *paragraph* inayoleta utata ni *paragraph* gani?

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu angalia ukurasa wa 59(c) pale juu na (i). Imeandikiwa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *Euro* 6,308,693. Akasema hapa chini kabisa hebu angalia pale chini sentensi yake amesema mchanganuo wa fedha hizo umeonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. 8 na Kiambatisho na. 8 namwambia aangalie ukurasa 119 kama alivyoweka hapa, *District Based Programmes* ni *Euro* 4,308,633 hizi 2,000,000 nyingine ziko wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge basi tumeelewa. Mheshimiwa Waziri nadhani umeipata hoja yake?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda nitafute habari za kuweza kuelezea hii tofauti.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea tutarudi baadaye. Si ameomba muda tunampa.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi sina haja ya kushika mshahara wa Waziri. Nahitaji ufafanuzi tu, *Vote 43,* programu hiyo ya 10 *Subvote 1001* - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka tu ufafanuzi juu ya Bonde la Lundo, Mradi wa Umwagiliaji Maji. Mradi huu mimi nilikwenda kwa Mheshimiwa Waziri, nimekwenda kwa Mkurugenzi wa *Irrigation* Wizarani nikazungumza nao juu ya Mradi wa Umwagiliaji Maji Bonde la Lundo. Katika mazungumzo wote walikuwa na nia ya kuingiza mradi huu kwa mwaka 2004/2005. Bahati nzuri hata Mheshimiwa Waziri wakati alipokuwa *RDD* Ruvuma, Mkoa wetu wa Ruvuma alianza lakini bahati mbaya mradi haukukamilika. Kwa hivi alikuwa na nia nzuri tu ya kufanikisha huu mradi ili kuendeleza nia aliyoianza ili mradi uweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mshangao mkubwa, nimepekua kwenye kitabu sijaona Mradi huo wa Lundo. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala hili linashughulikiwa sasa hivi kwa sababu mradi huu ulitakiwa uingie kwenye *DADP* uje juu. Maelezo ya *DADPs* tulikuwa hatujayapata. Lakini linashughulikiwa wakati wa kuandaa *DADPs* zote kwa sababu *allocation* bado haijafanyika kwa nchi nzima na huo wako upo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani zimepatikana, Mheshimwa Mbunge ameridhika na mradi upo, kwa hiyo, tunakuja kwa Mheshimiwa Christopher Wegga.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mshahara wa Waziri - *Subvote 1001,* ninataka tu nipate ufafanuzi kuhusu suala la pamba Kilosa. Dawa iliyopigwa imeingiza hasara asilimia 70 kama watavuna wale watu labda ni asilimia 30 tu na dawa ile wamekopa. Nilishasema Wizara zote mbili nalalamikia jambo hili nataka hata Waziri mmojawapo twende naye kule. Hata humu kwenye hotuba hakuna na namshukuru Mheshimiwa Waziri amesema uko uzembe kwa Watendaji. Sasa naomba tu ufafanuzi nani atalipia ile pamba na hasara ile nani atalipa, Serikali au wananchi ndio wameumia? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya malalamiko tunayapata baada ya kuja Dodoma na mimi niko tayari kwenda na Mheshimiwa Christopher Wegga, kuona tatizo hili. Wataalamu wangu wote wa pamba wako hapa, kwa hiyo, tutalichambua suala hili tutaona hii hasara ilitokeaje. Maelezo niliyopata mpaka sasa yanaonyesha kwamba, kuna watu walionunua dawa ikiwa na ukali unaotakiwa wakaiongeza takataka nyingine wakaenda wakawagonga wananchi. Kwa hiyo, tutachunguza hili tatizo na kama kuna mahali ambapo tunaweza kusaidiana kuparekebisha, tutaparekebisha na nitakwenda naye Morogoro tarehe 3 Julai, 2004 tutakwenda kuona hilo tatizo lilipotokea.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atamke kwamba, kama ikikutwa ni hasara na uzembe wa Wataalamu wake atalipa fidia? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama kujihukumu kabla hujaielewa kesi. Naomba twende tuelewe tatizo kwanza lilivyotokea na kwa hiyo, kwa pamoja nikiwa na Mheshimiwa Christopher Wegga, tutaelewa tatizo ni nini, nani aliyelisababisha na kwa hiyo ni hatua gani tuchukue kwa pamoja. Naomba nisitoe hukumu kabla hatujamaliza hiyo kazi.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Mbunge, umeelewa kwamba mtakwenda wote kule ndio mtapanga utaratibu. Tunaendelea.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wakati nikichangia hotuba jana nilimtahadharisha Waziri kwamba, mimi suingi mkono hoja yake hadi hapo atakapokuwa ametuletea nakala ya matangazo ya taratibu ambazo zilitumika katika kuipa *Exim Bank* utaratibu wa kugawa fedha hizi. Lakini kwa mshangao mkubwa hajaleta chochote. Amesema tu taratibu zilitumika, zilitumika. Sasa mimi nitaamini vipi wakati nlimwambia mimi suingi mkono mpaka tuone taratibu hizo kama ni kweli zilitumika? Kwa sababu Bunge lako hili lilishapitisha Sheria ya *Procurement,* ambayo inatakiwa tangazo la tenda litangaze kwenda sijui Benki gani mimi siamini kama *NMB, CRDB* ambazo ni Benki za Wananchi zikatae kitu kikubwa cha namna hii, kizuri kwa wananchi wao. Mimi siamini. Nilisema hivyo. *(Makofi)*

Lakini vile vile nilitoa na takwimu nikasema hii Benki pamoja na kwamba, Serikali imeamua kuipa mtaji wa kupeleka fedha kule, inafanya biashara kinyume inatoza riba kubwa kuliko Benki zingine. Sasa mimi ningedhani hapa angekuja angetoa na yeye takwimu za kunipinga mimi. Amekuja ameeleza amesema bila hata kusema hizo takwimu zangu. Kweli bado mimi nasimamia sijapata maelezo niko kifungu hicho hicho cha mshahara wake, mimi sikubaliani na maelezo aliyotoa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya jinsi Benki ya *Exim* ilivyopatikana ikapewa kazi hii ninayo na nitampa Mheshimiwa Lucas Selelii kama alivyotaka. Kwa hiyo, naomba aniunge mkono tumalizane na hili halafu maelezo yake atapewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selelii, muunge mkono halafu atakuletea.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anavunja utaratibu wa Bunge. Mimi niliomba alete Bungeni hapa. Mimi sikuomba peke yangu, niliomba kwa niaba ya Wabunge wote atuletee. Sio mimi peke yangu alete Bungeni tuone tusome taratibu zilivyofanyika, zilienda vizuri, matangazo yalitangazwa kwenye gazeti gani, basi angalau angesema gazeti fulani au basi sio kuniletea mimi aseme hapa atawapa Wabunge wote.

Lakini la pili, nimesema kwamba, hata zile takwimu mbona hajazitoa. Kwa nini *Exim Bank* itoe kwa hao *stockiest* asilimia 18. Ukishatoa asilimia 18 maana yake unafanya hata bei ya mbolea kule ipande. Ndiyo maana yake hiyo. Sasa angeniambia kwamba, *Exim Bank* hawatoi riba ya namna hiyo, mimi ningemwelewa. Lakini hata hivyo hakusema. Sasa mimi nitaunga vipi mkono. Bado sijakubali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba, nitasambaza kumbukumbu hii kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Hili la kwanza.

La pili, makubaliano yaliyopo kati ya *Exim Bank* na Mfuko ni kwamba, watatoza riba ya asilimia 12 sio 18. Kwa hiyo, kama kuna mtu yeyote aliyetozwa riba ya asilimia 18 naomba atuone ili tuweze kulichukua hilo kwamba, ni *preach of contract* na itusaidie sasa kuwashughulikia *Exim Bank.* Lakini makubaliano yetu ni asilimia 12. Hii asilimia

12 ndiyo iliyofanya Benki nyingi sasa zikakataa kujiunga na Mfuko huu kwa sababu wakati ule walikuwa wanatoza asilimia 24. Lakini wao wakasema wangeweza wakamudu na asilimia 12. Sasa kama wamekiuka tena tunaomba ushahidi ili tuwashughulikie. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa nieleze vipi ili nieleweke. Nadhani Waziri hataki kunielewa kwa nini hata asiseme kwamba hili lilifanyika na hili lilifanyika, ili baadaye aweze kusambaza hizo karatasi. Mimi bado sina imani kama taratibu kweli za tenda zilifuatwa angesema tu kwamba, hiki kilifanyika hiki hakikufanyika ili baadaye ikisambazwa mimi ningeelewa.

La pili, bado ile *percentage* ya Benki zingine kwa sababu Serikali ipo kwa nini haisemi. Mbolea ambayo Serikali inatoa *compensation* ni kwa ajili ya kusafirisha au ruzuku yoyote inayotolewa haimfikii mkulima kwa sababu inakuja inapanda mpaka shilingi 25,000/= kwa mfuko mmoja kwangu kule Nzega . Kwa maana hiyo, hizo fedha ambazo mkulima zingemfikia badala ya kwenda kulima zinarudi kwa wafanyabiashara wachache ambao wanadhulumu haki za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningeomba Kamati yako hii ikubali, iunde Tume ya Bunge ili ikachunguze ukweli wa tenda kama kweli ulifanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa utaratibu maelezo haya pia yanaweza kuwekwa mezani yakasambazwa kwa Wabunge wote. Halafu kama utakapokuwa umesoma una suala lolote ambalo unafikiria uitahadharishe Wizara katika hili unaweza pia ukatumia ile *document* atakayokuwa ameileta kuleta hoja zako binafsi wakati unaofaa ama kuleta hoja binafsi katika muda unaofaa. Kwa hiyo, *document* ile naomba iletwe kwenye meza.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuweka Mezani hii *document* yenye maelezo juu ya *Exim Bank* ilivyopatikana.

*(Hapa Waraka husika uliwekwa Mezani)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge ni utaratibu tu, hii *document* itatolewa kwa kila Mbunge, ataisoma na wale watakaokuwa na hoja juu ya hiyo *document* wana ruhusiwa kuiendeleza katika wakati mwingine wa vikao vya Bunge hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Tuna orodha ya watu tayari tunaendelea nao. Sasa hivi tunamwita Mheshimiwa Chubi.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa kifungu Na. 1001 - Mshahara wa Mheshimiwa Waziri, suala la *Exim Bank* limekuwa linapigiwa kelele tangu mwaka 2001, 2002...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa taratibu za kanuni hii kama suala lile lile limezungumziwa na Mbunge mwingine wewe huwezi kuendeleza tena suala hilo.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Kwa mtazamo tofauti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hebu sema tuone mtazamo

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie *discrimination* kwenye ile Benki. Hii ni *issue* nyingine tofauti. Halafu *PM* yupo kwa nini analifumbia macho hili suala? Kwa nini watu wasiende kuangalia kuna nini pale ndani? Watu wazima hawawezi wakapoteza muda wao kulalamikia suala la *Exim Bank* kama hakuna *anomalies. This is very serious* kwa sababu Mama yule amewekwa *as a rubber stamp.* Kuna Watendaji pale hawajui hata Kiswahili. Wametoka India utashughulikiaje mkopo wa wakulima kama mtaalamu hajui Kiswahili. *Is an adequacy?* Sasa mambo ya kudhalilisha na katika hali hii sisi msizibe masikio kama kuna uwezekano tunaomba tuyazungumze haya mambo hata kwenye *privacy* bila kuwagusa watu wengine. Mambo yanayofanyika pale ni mambo ya ovyo, tupo sisi tumenyanyaswa watu kama sio Wabunge. Kama Mbunge haheshimiwi ataheshimiwa nani? Katika haya mafiga matatu sisi tuko *top* bwana.

Sasa mimi sizungumzii wala sishiki shilingi wala sifanyi chochote, isipokuwa namwomba Mheshimiwa Waziri hili suala usilipuuzie. *Something should be done* na lazima kabisa pale ndani pana uharo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge maneno mengine sio ya Kibunge. Tunaomba urekebishe hilo neno la mwisho.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ndani pana uchafu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hakuna mtu ambaye anailinda hiyo Benki ya *Exim.* Waziri amesikia, Serikali imesikia, tutafuatilia hayo yote ambayo mmeeleza. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichangia katika hotuba ya Wizara hii, najaribu kushika kifungu Na. 1001 - Mshahara wa Waziri. Ugomvi wangu ni ule ule kwamba, kuna fedha za *STABEX* zimetengwa kutengeneza barabara. Hizi zingine zilivyogawiwa amegawa vizuri zimefanya utafiti wa pamba, katani Sheria ya Vijiji, maeneo ya chai. Mimi sina ugomvi japo *STABEX* ilitolewa kwa ajili ya Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi niliuliza swali hapa, sasa sijui na mimi nikifanya fujo nadhani hatutaelewana. Nikamwuliza Waziri wa TAMISEMI, bahati mbaya Waziri wa Ujenzi akajibu. Ningependa kutoa *caution* ninachotaka kuuliza asinijibu Waziri wa Ujenzi, kwa sababu katika Mkoa wa Kagera ni jimbo la kwangu tu barabara

hazikutengenezwa. Mimi siamini kwamba anafanya hivyo kwa sababu mimi natoka *opposition,* siamini hivyo. *Only a mad man* anaweza kuamini hivyo. Sasa ziko sababu. Kwa hiyo, ninapouliza ninakuwa na masuala ya msingi. Kwa hiyo, ninachotaka kuuliza amesema hapa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 58 kwamba, barabara katika maeneo ya Kahawa yametengewa *Euro* 10,000,000 ambazo ni bilioni 10 na zaidi.

Huku kwenye maelezo ukurasa wa 119 ameeleza kwamba, watafanya *rehabilitation of priority roads.* Halafu *reparation study* itachukua hizo na *provision for regional road maintenance*. Hata kama zimepelekwa *TANROAD* ambao hawa-*deal* na *feeder roads* kama tulivyoelezwa ilivyokuwa dhana ya *STABEX* katika kuwasaidia zile sehemu zinazolima kahawa. Tumeuliza hapa na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe jana alikuwa mkali, tunataka Waziri atuambie hao ambao wamekwenda kuangalia hizo barabara, sasa hivi wamepita Mkoa upi na Mkoa upi na barabara ipi na nilimwuliza Waziri, lakini hakujibu? Nilipouliza swali hilo juzi Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akajibu kwamba: "Aah, si walikuwa wanapita kule, mpaka wamwite Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi!" Nadhani hiyo ni lugha ya dharau kwa sababu wanapofika kule wanapita kwa Mkurugenzi, wanapita kwa Mkuu wa Wilaya na mimi nimepiga kule simu hawajapita, hata Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe hawakupita kwake.

Sasa tunachotaka kuelewa hapa ni kwamba, kabla hizi hela hazijapelekwa *TANROADS* wakazipeleka huko wanakojua na nyongeza Waziri wa Ujenzi akanijibu tena kwa dharau kwamba: "Hizo hela hazijatengwa, sasa tungeziwekaje kwenye bajeti?"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye maandishi nasema wanamaliza huo ukaguzi wao ambao siujui, lakini ujenzi utaanza Septemba, 2004. Sasa kama tumeambiwa wafadhili wameahidi hizi na mmezitenga hapa lile jibu la Waziri kama siyo kejeli aliyokuwa ananijibu kwamba, wangezitengaje hawajaziweka, alikuwa ana maana gani? Sasa ninachotaka turudi kwenye mstari. Nataka Mheshimiwa Waziri anijibu wamepita Kagera na kwangu wamepita? Wamepita Kilimanjaro na wapi walikopita ili watuambie tuelewe kama tunaweza kuona hapa tukirudi mwezi wa 11 tujue tunafanya nini? Ninaomba majibu sasa hivi, wewe uliyepiga simu wamepita Mkoa gani na Mkoa gani na ni barabara gani.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha iliwekeana mkataba na huyu mkandarasi na wakakubaliana muda wa kufanya hii kazi. Sasa tunatarajia kwamba, mkandarasi atakapokuwa amemaliza huo muda wa kufanya kazi ndipo atakapotoa taarifa. Kwa hiyo, sijui kwamba ni Mikoa gani ambayo ameshatembelea mpaka sasa kwa sababu nimekuwa sifuatilii. Naomba nirudie niliyosema wakati nikihitimisha hapa kwamba, suala hili itakuwa vizuri zaidi kulizungumza wakati tutakapokuwa tunazungumzia hotuba ya ujenzi kwa sababu ni suala linalohusiana na barabara na wakati huo tutakuwa tumetafuta kujua maendeleo ya huyu mkandarasi ambaye alitiliana mkataba na Serikali tarehe 1 Juni, 2004.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nijibu kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo katika kuongeza majibu kwa Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi kama ifuatavyo: -

Kwanza kabisa, napenda niseme wazi kwamba, sijawahi kumjibu Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi kwa jeuri. Lakini nataka pia nithibitishe hapa kwamba, barabara za Mheshimiwa Mutungirehi ni baadhi ya barabara ambazo zinaendelea kutengenezwa ikiwepo sehemu ya Rwabuninka ambapo palikuwa na daraja la kwenda mpaka Uganda, lile daraja limehamishwa, palikuwepo na *ferry* ikapelekwa kwenye sehemu ambayo inaitwa Kyanyabasi. Kwa hiyo, nataka kumwonyesha tu kwamba, barabara za Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi zinatengenezwa kwa sababu Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi haina ubaguzi. *(Makofi)*

Lakini la pili, kuhusu suala la fedha za *STABEX*, fedha za *STABEX* kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekwishazungumza hapa siku za nyuma, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amekwishazungumza hapa na mimi nimekwishazungumza hapa, kwa sababu Serikali ni moja, ziko jumla ya *Euro* milioni 10. Hizi fedha mkataba ulitiwa saini kati ya *European Union* pamoja na Hazina chini *EDF* 9 kwenye mwezi wa pili mwaka 2004. Masharti ya kupata fedha hizi ambayo waliyaweka *European Union* ilikuwa ni kwamba, lazima ateuliwe *consultant* na yule *consultant* ndiye atazipitia barabara zote za maeneo yanayolima kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri mkataba ule ulisainiwa kwenye mwezi wa tatu na wa nne na *consultant* aliyeteuliwa ni Kampuni ya *Roughton* ya Uingereza ikishirikiana na Kampuni ya Data. Kazi zilianza tarehe 01 Juni, 2004, inategemewa kukamilika mwishoni Novemba, 2004. Kwa hiyo, zikishakamilika zitapelekwa *European Union* kwa kupitia ili wakubali kutoa fedha au kutokutoa na ndiyo maana nimesema kwenye Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, hizi fedha hazikupangwa kwa sababu hatujazipata na pia kwenye Bajeti ya Wizara ya Kilimo hizi fedha hazikuwepo kwa sababu hazijaanza kupatikana. Kwa hiyo, tunasubiri mpaka *European Union* watakapokubaliana na tafiti zitakazofanywa na Kampuni ya *Roughton* na *Data* ili waweze kutoa hizo fedha na fedha hizo zimepangwa katika ma-*group* matatu. Mara ya kwanza zitatolewa shilingi bilioni mbili, baadaye shilingi bilioni nne na baadaye tena shilingi bilioni nne katika miaka mitatu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi bado anaweza akaenda akauliza kwa Mwakilishi wa *European Union* ili awaulize kama hizo fedha zimeshatolewa Serikalini. Mkataba umekwishasainiwa, lakini fedha hatujazipata, kwa hiyo, hatuwezi kutenga kwenye bajeti fedha ambayo hatujaipata kwa sababu tutakuwa tunadanganya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ilinibidi nijibu kwa sababu Serikali ni moja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, hawezi kunizuia kujibu swali ambalo mimi najibu kwa niaba ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitopenda kuendeleza malumbano kwenye kikao chako. Kwa heshima hiyo, naomba nisome hii.

**MWENYEKITI:** Soma.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Anasema: “Barabara katika maeneo ya kahawa, usimamizi wa utekelezaji wa matengenezo ya barabara na matumizi ya fedha za *STABEX* utakuwa chini ya Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Tenda ya kubainisha barabara zitakazotengenezwa ilifunguliwa tarehe 13 Februari, 2004 na Kampuni ijulikanayo kama *Roughton International Ltd. UK* ilishinda. Kazi ya kubaini barabara zitakazojengwa inatarajiwa kukamilishwa mwishoni mwa Juni au Julai, 2004 na ujenzi wa barabara unatarajiwa kuanza Septemba 2004.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuandika mimi, haya maneno siyo ya kwangu, ni maneno ya Kiongozi wa Serikali. Sasa umemsikia Mheshimiwa alivyokuwa anasema itakuwa mwezi sijui wa kumi na ngapi huko, wanaleta vitu ambavyo havipo! Tangu niingie hapa Bungeni yeye Waziri yuko pale, sikuwahi kuuliza swali lolote kwenye Wizara yake ya Ujenzi, kama niliuliza atamke hapa nitajiuzulu hapa hapa. Sasa, ninaposema haya masuala ninamwomba kwamba, tuheshimiane. Hizi hela wamesema ni za *feeder roads,* hivi yeye anahusikaje? *Feeder roads* haziko kwenye ile ya kwake! Nadhani sitaki kuendeleza malumbano, lakini ujumbe wameupata. Hii tabia ya kudhulumu mali ya wakulima kama mnadhulumu mali ya marehemu si sawa!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnapouliza muwe mnajielekeza kwa Mwenyekiti, mkianza kujielekeza huko mtanza kurushiana vitabu bure. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, nadhani limejibiwa tayari au kuna jibu lingine?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifafanue suala hili. Kama alivyoeleza Waziri wa Ujenzi, maelezo yake ndiyo sahihi kwa sababu Wakala anayesimamia fedha hizi ni *TANROAD* na *TANROAD* iko chini ya Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, Waziri wa Ujenzi ndiye Waziri anayehusika na pesa hizi. Sasa mimi namshangaa sana Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi kutoa amri kwamba yeye asishiriki katika kujibu swali hapa Bungeni.

*(Hapa Mheshimiwa Mutungirehi alisimama)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, mimi Mwenyekiti sijakuruhusu, naomba ukae. Kwa suala hili wala hamtofautiani, tunaosikiliza hatukuona tofauti yoyote. Tulichokiona ni kwamba, humu katika hotuba anasema kutakuwa na Wakala ambaye ameteuliwa na nilivyomsikiliza Waziri wa Ujenzi amesema hivyo hivyo na kwamba pesa kwa sasa hazipo ila *survey* itakapomalizika na huyu wakala ndiyo atamaliza Juni, 2004, ndiyo ulivyosoma, nadhani tusubiri. Malumbano mengine yoyote hayana msingi wowote. *(Makofi)*

Sasa tunarudia swali la Mheshimiwa Meja Jesse Makundi.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unasemaje?

**MWENYEKITI:** Enhee, ndiyo.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Nimeshamaliza au kuna lingine?

**MWENYEKITI:** Hapana, naomba ukae kidogo. Wakati umeuliza swali Waziri aliomba muda. Kwa hiyo, sasa tunamtaka ajibu.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu sahihi ni ile iliyoko ukurasa wa 59. Takwimu iliyoko kwenye jedwali imekosewa kwa sababu kuna Shilingi milioni mbili kwa ajili ya *pulparies* ambayo haikuwa imeongezwa. Kwa hiyo, naomba lile jedwali lisahihishwe kwa kuongeza *Euro* milioni mbili katika lile jedwali.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa manufaa ya majadiliano hakika hiyo ni sahihi. Ahsante sana. *(Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* .............................. Sh.232,821,700/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ................................. Sh.584,193,800/=

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Subvote 1003,* kifungu kidogo 250100 nikiambatanisha na kifungu kidogo 260100, ninataka Waziri anisaidie. Nashika Shilingi kwa hawa wote wanaosaidia kuishauri Serikali kwa ajili ya *policy* na *planning.* Kilimo kuanzia tumepata uhuru tumesema ni uti wa mgongo, angalau mgongo usiokuwa na kichwa, lakini tunasema tena ni Sekta Kiongozi, ila siku hadi siku mipango inazidi kudidimiza wakulima kuwa katika hali maskini. Naomba Waziri anisaidie ni lini ataleta ndani ya Bunge hili mipango ya Wizara hii kwenye suala la kilimo itakayoweza kuwafanya wakulima waondokane na jembe la mkono libaki tu kwa watoto wadogo na bustani na historia katika *museum* na lini nchi yetu polepole tutafikia sasa badala ya kusaini *contract* na Mungu kwa kumwomba atupe mvua tuamue tufanye *irrigation.* Nimeshika hiki kifungu 260100 kwa sababu ni mawasiliano na taarifa. Kwa hiyo, ni lini ataleta hapa taarifa? Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishaleta mbele ya Bunge hili *Agricultural Sector Development Strategy* na katika kuwasilisha hotuba hii nimeeleza kwamba, tumeandaa *Agricultural Sector Development Program,* ambayo inafafanua masuala mbalimbali yatakavyotekelezwa. Nimeeleza pia kwamba, tumeanza kupata mikopo na wahisani wanaochangia sasa katika utekelezaji wa *Agricultural Sector Development Program.* Ningeomba sana Mheshimiwa Mbunge asome sehemu ile ambapo tunazungumzia kazi zitakazofanyika mwaka 2004/2005, ataona kazi ambazo tunakusudia kufanya na kuna maeneo ambayo tumeyafafanua kwa

kirefu sana. Kuna miradi miwili ambayo tumeifafanua kwa kirefu sana, miradi hiyo ni *PADEP* na *DESEP*. Hii miradi pamoja na vitu vingine, itatoa mikopo kwa ajili ya kununulia zana za kilimo, kwa ajili ya kununulia pembejeo na kadhalika na mkulima anapata ruzuku kubwa sana ya kumuwezesha kufanya hivyo. Kwa hiyo, tulishaleta hapa Bungeni na hatukusudii kuleta tena mipango tofauti na hii ambayo tumeshaleta.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza hiyo kwa makusudi, bila kuwa na *timeframe* hatutafanikiwa. Kwa mfano, tuna *vision* ya 2025 na mipango imewekwa tu na itaendelea kuwekwa hivyo. Tunataka tumshike Waziri kwamba, siku moja ulisema ikifika mwaka 2025 kutakuwa hakuna jembe la mkono, tuweze kumshika kuliko kusema tu. Matokeo yake watu wa Mipango wameweka *projects* nyingi za maendeleo ni *donor dependents, donor* wakiondoka maana yake kilimo kimekwisha. Nataka hata kama siyo leo, lakini awa-*commit Planning Section* watuambie mwaka fulani mpaka mwaka fulani tunategemea kufanya hivi, mwaka fulani mpaka fulani tunategemea hivi na mwisho wetu.

Ninaizungumzia hiyo *reference* kwa sababu kesho tutakubana kaka yetu, japokuwa inawezekana sisi hatutakuwa hai, lakini watakaokuja watataka *reference*. Tukiiacha hivi hivi, ndugu yetu tutakuwa tunamsema tu kumbe mipango kaputi. Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali ushauri kwamba tuipe *timeframe*. Lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge atambue kwamba, hii kazi anayonipa ni ngumu kweli kweli, kwa sababu kuifanya kazi hii ni lazima tufanye *projection* ya uchumi wa Taifa ili utuonyeshe ni lini utakapoweza kutuwezesha kununua matrekta ya kutosha nchi nzima. Nitakwenda kukaa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, tutaangalia ni kiasi gani cha hiyo kazi tunaweza kufanya. Namshukuru kwa ushauri wake. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho *Subvote 1003*, kifungu kidogo cha 250100, mishahara ya hawa watu wa *policy and planning.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza sana hapa toka mwanzo kwamba, nisingeweza kushika mshahara wa Mheshimiwa Waziri kwa sababu ya yale mazuri ambayo ameyafanya katika Jimbo langu. Kwa hiyo, niko hapa kwa watendaji kwa sababu *issue* hii naiona kabisa ni kwa upande wa watendaji. Ameeleza hapa kuhusu suala la kuzuia ulimaji wa pamba Mbeya kwamba, wataalam watakaa. Ninaomba maelezo, nipewe *timeframe* kwa sababu hii ya kusema wanakaa, alikuja Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula Chunya alitoa ahadi hiyo kwamba, Serikali inaliangalia hilo. Amekuja Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM na akatoa ahadi kwamba Serikali inalifanyia kazi. Suala la ulimaji wa pamba, suala la mapato ni la kufa na kupona. Je, watu hawa mnataka wafe ndiyo tupate majibu? Nataka nipewe *timeframe* ni lini hili tatizo litakuwa limetatuliwa.Je, kama Wananchi wataamua kulima pamba Serikali mtaifyeka? Naomba maelezo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nahitimisha hotuba yangu hapa nilieleza, lakini pengine nianzie nyuma kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikaa hapa Dodoma na Waheshimiwa Wabunge wa hii Mikoa inayolima pamba, tukakubaliana kwamba tutume ujumbe mwingine Afrika ya Kusini na hizi nchi nyingine za Kusini zinazolima pamba waende wakaangalie huko nako wanafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulituma ule ujumbe na umerudi hivi karibuni, nimepata ripoti yao kama wiki mbili zilizopita. Kwa hiyo, ninalotakiwa kufanya la kwanza ni kuitisha tena kile kikao cha wale Waheshimiwa Wabunge, akiwepo Mheshimiwa Benson Mpesya tupitie taarifa zile tulizoletewa, lakini tutafanya zaidi ya hilo. Tutapitia vile vile kumbukumbu tulizonazo zinazotokana na kazi zilizofanywa na watafiti wetu kwa sababu waliuliza maswali mengi sana ambayo itabidi hizo taarifa zitusaidie kujibu pamoja na hawa wataalam wenyewe waliozifanya. Sasa tunaloomba waturuhusu ni kwamba, katika kipindi hiki tutakachokuwa hapa kwenye hili Bunge la Bajeti, tuchague siku moja ya Jumamosi ama Jumapili kwa kukubaliana tukae tupitie kumbukumbu zote hizi ili kila mmoja azielewe sawasawa na tujue kwamba kama tunafanya maamuzi, hayo maamuzi ni *based on what*. Vile vile, watakaoshiriki ni wadau wote wanaolima pamba katika nchi hii. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu ilikuwa ni kupewa *timeframe*. Nimeambiwa kwamba, ndani ya Kikao hiki cha Bajeti nitakuwa nimepata suluhisho na bahati nzuri tunaelekea katika msimu, upande wa Kusini nimeridhika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 - *Agriculture Training Institutes* .......... Sh.1,088,460,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Crop Development* .............................. Sh.16,839,736,700/=

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakishika kifungu 2001, kifungu kidogo 250100. Katika eneo hili nina masuala matatu. La kwanza, labda kufuatia aliyokuwa anaongelea Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, ni kweli kwamba, kuna kitu kinaitwa *DADPs*, lakini hakuna *comprehensive plan* ya kuendeleza kilimo katika Wilaya zetu, hakuna! Kama kwenye Wilaya zenu ninyi ipo, kwangu hakuna. Sasa na katika nchi yetu ndiyo tunayo *Agricultural Development Strategy,* lakini lazima tuwe na *plan* ya ku-*implement* hiyo *strategy* na *plan* hiyo hatuna.

Mheshimiwa Waziri tulimshauri jana kwamba, tungependa atuletee mapema iwezekanavyo kuwe na *plan* ambayo tunaifuata na ambayo tunaitumia ku-*invest* mapesa haya mengi ambayo tunapata kwenye kilimo, tusiombe kwamba kilimo kitaendelea tu kwa kukipa pesa nyingi. Angetueleza lini *comprehensive plans* za maendeleo, *modernization* ya Wilaya na kwenye Taifa itakuwa tayari? Hiyo moja. *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa hapa ndiyo kwenye *crop development,* hapa ndiyo njaa inapotokea au ndiyo tunaposhibia. Katika Serikali kutoa ruzuku na kuondoa kodi katika pembejeo na mbolea na vitu mbalimbali, *experience* tuliyonayo kama mwaka 2003 ni kwamba, mbolea hata iliyoondolewa kodi ilienda kuwa ghali kuliko hata mbolea ambayo ina kodi huko nyuma. Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba, kweli kodi hizo zote zilizoondoka mbolea itakapokuwa imekuja, imewafikia Wananchi itakuwa rahisi kweli? *Experience* iliyopita katika uagizaji wa vitu hivi vilivyoondolewa kodi tenda hazikuwa *open.* Je, sasa utaratibu wa tenda na sheria ile ya *procurement* utafuatwa ili kweli mkulima afaidike na unafuu huu ambao umetolewa na Serikali? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2003 Wizara zote zinazohusika na kilimo ziliitisha mkutano wa kuandaa hizi *DADPs* na zikaandaliwa *DADPs* ambazo zilianza kutekelezwa mwaka 2003 na fedha za mwaka 2003 zilitolewa kwa misingi ya zile *DADPs* zilizoandaliwa mwaka 2003. Kama Wilaya ya Mwanga ina tatizo la kuandaa *a Comprehensive Agricultural Development Plan,* tunazo fedha kwenye bajeti za kuwasaidia. Naomba watuambie tukae nao tuandae hiyo *Comprehensive Agricultural Plan* kwa ajili ya Mwanga na kama kuna Wilaya nyingine yoyote yenye tatizo hilo tunaomba watuambie pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni hili la mbolea. Mbolea ya mwaka 2003 ilikuwa imeelekezwa kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tu, Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma. Hiyo ndiyo Mikoa iliyoelekezewa ile mbolea. Kuna jambo linalojitokeza hapa ambalo silielewi sawa sawa, pengine Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe atapenda kunifafanulia, juu ya tenda. Hakuna tenda zilizohusika na suala hili kwa sababu tulichofanya tulisema mtu yeyote atakayefikisha mbolea pale mkoani na akaiuza atafidiwa gharama za usafiri. Kwa hiyo, halikuwepo suala la tenda na Naibu Waziri alitembelea Rukwa na Mbeya kuhakikisha kwamba huu utaratibu umewekwa na unafanya kazi na mimi nilikwenda Ruvuma na Iringa kuhakikisha kwamba utaratibu uliwekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliowekwa ulikuwa unaunda Kamati za Pembejeo za Mkoa chini ya usimamizi wa *RAS* na hizi zilikuwa zina-*support* Wilaya ambazo zingekuwa na Kamati zao za mbolea. Kwa hiyo, waliteua watu ambao ndiyo watakaouza mbolea, waliweka utaratibu wa kubaini nani aliyeleta mbolea kiasi gani, ameuza kiasi gani na ni kutokana na *returns* hizo ndiyo zilizowezesha wale waliohusika wakafidiwa kwa gharama za mbolea. Bei za mbolea ziliendelea kuwa nzuri sana mpaka mwezi Machi, baada ya Machi kulitokea upungufu wa mbolea nchini kwa sababu kupungua kwa bei kuliongeza *consumption,* hakukuongeza uingizaji wa mbolea kutoka nje. Kwa hiyo, kukawa na upungufu wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini unakuta wengi wameshapanda, wameshatumia mbolea za kupandia. Kwa hiyo, kwa kweli athari hazikuwa kubwa. Lakini tunajua kwamba, mbolea katika sehemu nyingine ya nchi ilipanda bei sana kwa sababu *by the time* walipoanza kulima kwa mfano, Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, kulikuwa tayari kuna upungufu wa mbolea nchini na ndiyo maana mbolea zikapanda. Kwa mwaka huu unaokuja tuta-*cover* eneo kubwa zaidi na kwa hiyo, tutasimamia eneo lote kwa wakati mmoja na tunatarajia kwamba, tutaweza kudhibiti bei zisipande. Vile vile, ule ulikuwa ni mwaka wa kwanza, kwa hiyo, ilikuwa ni mwaka wa kujifunza na kama kuna mapungufu yaliyotokea ilikuwa ni kwa sababu kwa kweli hatukuwa na mazoea ya kushughulikia suala hili. Sasa tuna mazoea ya kutosha.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ingekuwa kitu ambacho wote tungependa kujua. Kabla ya bei ya mafuta kuanza kupanda kwenye soko la dunia na ni mwaka 2003 bei ya mbolea kama *Urea, Calcium Ammonium Nitrate (CAN)* zilikuwa Dola tano *f.o.b.* Dubai kwa mfuko wa kilo 50. Sasa gunia lile likija Tanzania linauzwa mpaka Sh.25,000/= au Sh.30,000/=. Gunia hilo hilo likipelekwa na njia ya barabara hapa, likaenda mpaka Zambia huko ni Dola 10. Hivi kwetu kwa nini mbolea ni ghali sana, kwa nini? Katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika mbolea ni ghali sana Tanzania kuliko wenzake, kwa nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ninaloweza kujibu ni kueleza juu ya bei, lakini 'kwa nini' ni ngumu kwa sababu itabidi tumpate muuzaji wa mbolea ili atusaidie kujibu hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza huu utaratibu wa kutoa ruzuku, tulifanya utafiti juu ya bei *CIF* Dar es salaam. Kwa hiyo, tukachukua bei za kununulia na mtu yeyote anayetaka hizi bei ni rahisi ziko kwenye *internet.* Tukachukua bei za kununulia, kusafirisha na *insurance* mpaka kufika Dar es Salaam tukapata kwamba kwa mbolea zilizo nyingi mpaka kufika Dar es Salaam mfuko wa mbolea utagharimu Sh.10,000/=. Kwa hiyo, mfuko wa *urea* ukiwa *landed* Dar es Salaam pale bandarini bei yake ni Sh.10,000/=, bei ya *SA* na *CAN* ni chini, bei ya *DAP* iko juu zaidi kidogo. Kwa hiyo, hizi ndizo bei tulizotumia kama *basis* ya kulipa fidia ya gharama baada ya ku-*assess* vile vile gharama za kusafirisha hiyo mbolea kwenda kwenye vituo vikuu vya kupokelea mbolea mikoani. Kwa hiyo, bei za mbolea ndizo hizo. Sasa kinachotokea ni kwamba, mtu ana mbolea yake anangojea msimu ukifika anauza kwa bei anayotaka na kwa kuwa tatizo ni kwamba tuko katika soko huria, ambalo watu wengine wanali-*misuse* kutaka pesa. Kwa hiyo, bei ya mbolea ikiwa *landed* Dar es Salaam mfuko mmoja ni *approximately* Sh.10,000/=.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani suala hili kwa kuwa mbolea ndiyo itakuwa nyenzo muhimu katika kuboresha kilimo hapa nchini itatubidi tuendelee kuliongelea na tutafute njia ambayo tuta-*streamline* ili bei za mbolea zisipande juu kuwanufaisha hawa *vendors* kuliko Wananchi.

Kwa hiyo, tuendelee kuzungumzia suala hili na mimi nimeridhika mpaka hapa tulipofika. Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Directorate of Irrigation and Technical Service....* Sh.2,920,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Research Development* ......................... Sh. 3,978,174,500/=

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hicho 3001 kifungu kidogo 260100, ninamwomba Waziri aniambie mkulima wa kawaida kule kijijini akitaka kupata taarifa za *research* katika lugha nyepesi anayoweza kuitumia imsaidie kwenye kilimo chake na wakati *extension officers* hawaonekani ataipata wapi?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni swali gumu kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vyetu vyote vya utafiti vina machapisho ya Kiswahili kwenye vipeperushi kwa lugha nyepesi kabisa. Kwa mfano, ukienda Ukiriguru utapata vipeperushi juu ya kilimo cha muhogo, kilimo cha pamba, udhibiti wa visumbufu mbalimbali, utapata vipeperushi karibu juu ya kila kitu na ukienda kwenye vituo vyetu vyote ndiyo ilivyo. Isitoshe watafiti wetu mara nyingi sana hutoka nje kwenda kwa wakulima kusambaza matokeo ya utafiti wao. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge angetaka akusanye baadhi ya kumbukumbu atuambie, tutamtafutia kutoka kwenye vituo vyetu vyote ili vimsaidie wakati atakapokuwa kwenye jimbo lake. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo la kupata kumbukumbu, nikizihitaji na nikiamua kuwa mkulima nitazipata. Niko hapa nazungumzia wakulima kule vijijini, ukienda kwa Luhombo, ukienda Kijiji cha Kisarawe, ukienda kijijini kule ndani ndani Mwanza kule Magu, ndiyo ninachozungumzia. Nia yangu ni kuiomba Serikali, itafute utaratibu wa mkulima huyu ambaye huyu *researcher* hawezi kumfikia kwa sababu hata *extension officers* uliowaweka katika vijiji na kata hawaonekani. Sasa nia yangu Serikali itafute utaratibu ili imfikie mkulima huyu. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna njia mbili tunazojaribu kutumia kufikishia mkulima utaalama. Kuna vipindi vya redio ambavyo vinatolewa mara mbili kila wiki. Halafu tuna jarida la mkulima wa kisasa. Haya yalianzishwa ili kutusaidia kujaza hii *gape* iliyopo. Isitoshe katika vituo vyote vya utafiti tuna afisa ambaye kazi yake ni kiungo kati ya kituo na *extension officers* na wakulima. Kwa hiyo, naye akitafutwa akatusaidia kufanya hii kazi ya kiungo, hizi habari zitawafikia wakulima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani maelezo ni hayo. Fanya ushauri wako kwa muda mfupi maana dakika si nyingi.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina ushauri kama tuna *administrative channel* mpaka vijijini, ninaomba ikiwezekana kwenye ofisi za Watendaji aidha Kata au Kijiji, hivi vipeperushi viwepo ili waweze kuwafikia wakulima. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Sitaki kushika mshahara wa mtu yeyote, lakini naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake ametaja shughuli zitakazofanyika vituo vyote vya utafiti isipokuwa Naliendele. Je, ameamua kukifunga kituo hicho wakati kinatusaidia katika utafiti wa mihogo, karanga, korosho, ufuta na kadhalika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niombe radhi kama kuna hiyo *omission* kwa sababu kituo chetu cha Naliendele ni moja ya vituo muhimu sana. Nilikuwa nasoma kabrasha moja ambalo limeandikwa na mtalaam mmoja akizungumzia juu ya uzalishaji wa korosho wa nchi mbalimbali, India na kadhalika, kwamba tukifika *kilogram* kama 20 unaweza kupata mapato ya kutosha Tanzania kwa mikorosho yetu ya kawaida, hatukufika juu huko. Nilikwenda Naliendele nikakuta wana mikorosho ambayo waliniambia inaweza ikatoa kilo 100 kwa mti mmoja kwa hiyo imezidi mara kumi. Halafu kimefanya utafiti mwingi sana wa muhogo na shughuli nyingine mbalimbali. Kama tumekiacha ni *omission for which I regret,* hakijaondolewa hakuna hata utaratibu wa kukipunguzia hadhi yake. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Je, tutakuwa na uhakika kwamba wametengewa fedha maana humo hawajatajwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zao zipi na Mkurugenzi mwenyewe nafikiri yupo hapa namtazama, angekuwa hana fedha angekuwa ameshatushika shingo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *National Food Security* .......... ......... Sh. 734,388,700/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5002 - *Strategic Grain Reserve* ........................ Sh. 7,416,992,500/=

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nikisoma hapa naona kwamba, fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo ni shilingi bilioni saba. Lakini tulipata njaa juzi hapa tulitenga shilingi bilioni 24 na ni sehemu chache tu katika nchi hii. Waziri atatoa maelezo gani kwamba, kwa nini fedha ziko chache kiasi hicho katika hii *Strategic Grain Reserve* wakati anaelewa wazi kwamba, juzi tu tulitenga hela kidogo, shilingi bilioni 24 na alilalamika kwamba fedha ni chache, zilizotengewa hii *Strategic Grain Reserve.*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hili swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kwa sababu linanisaidia niweze kufafanua nini tunachofanya na *SGR* mwaka huu. Mwaka huu tunakusudia kununua tani kati ya 75,000 na tani100,000. Kwa mara ya kwanza *Strategic Grain Reserve* haijawahi kununua mazao mengi namna hiyo. Tunakusudia vile vile kununua mtama. Mwaka 2003 Waziri alitubana tutafute mtama, tukatafuta mtama mpaka Sudan haukupatikana. Kwa hiyo, tunataka tununue mtama tuwe na *stock* yetu ya mtama ili tukihitaji mbegu tuwe tunayo katika *Strategic Grain Reserve* na vile vile tukihitaji wa kula uwepo. Fedha zilizoandikwa hapa ni fedha zinazotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2004/2005. *Strategic Grain Reserve* wana *balance* ya pesa kwenye akaunti yao ambazo zinaongezea hii.

Tumepata vyakula kutoka India, mchele na ngano, ambavyo tutaviuza zile fedha zitakazopatikana zitaongezea ndiyo maana tunafika tani 100,000 za chakula. Kwa hiyo, mwaka huu tutanunua chakula kwa wingi kuliko tulivyowahi kununua miaka iliyopita. Vile vile tuna *stock* za karibu tani 30,000 kwenye *store*. Kwa hiyo, tutakuwa na tani zaidi ya 100,000 kwenye *Grain Reserve.* Kwa hiyo, maeneo yale ambayo yana upungufu wa chakula tuna uhakika tutakuwa na uwezo wa kuyakabiri. Nashukuru.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 43 - Wizara ya Kilimo na Chakula**

Kif. 1003 - *Policy and Planning*................................ . Sh. 10,262,998,008/=
Kif. 1004 - *Agriculture Training Institutes* ................ Sh. 654,000,000/=
Kif. 2001- *Crop Development* ............................... Sh. 10,613,133,592/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka maelezo, nilitaka tu Waziri atutoe wasiwasi hizi anakozipeleka kule kwa sababu nimechangia hapa asubuhi, *network* yake na utaratibu ambao atautoa ili sisi Waheshimiwa Wabunge, tuweze kuelewa kwamba zimetumwa shilingi 400, 000,000 Karagwe, ama Maswa ama kwingine na tunazisimamiaje ili kuhakikisha kwamba, zisije zikapotea kama zile za walimu ambazo zilitafunwa na Waziri Mkuu akaahidi kuzilipa, ndicho nilichoomba. Tunaomba ule utaratibu kwa sababu yeye hana *network* na uzoefu umeonyesha kwamba, hela zinapokwenda kule wanaziweka kwenye fungu la pamoja halafu wanazitafuna. Sasa ninaomba Waziri hapa kabisa atuhakikishie kwamba, ni

mpango gani umeupanga halafu atatoa maelezo ya ziada ya kuhakikisha kwamba, Watanzania wote huko Wilayani waliko wanaelewa kama walivyoelewa fedha za MMEM kwamba, hakuna anayeweza kuzichezea watamhoji. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwa huu wasiwasi alionao. Lakini ninakuwa na wasiwasi na mimi kwamba mnafahamu, tunachora picha mbaya sana ya watendaji wetu kwamba ni walaji tu ambayo mimi siamini hivyo, mimi kwa kweli siamini hivyo, maana wangekuwa ni walaji hizi kazi ambazo tunaona zikifanyika tusingeziona. Maana hawezi kula halafu akajenga barabara, akajenga shule, akafanya na shughuli nyingine. Inawezekana kuna wezi wawili, watatu, ambao watashughulikiwa na *system* ya Serikali. Lakini sidhani kama kweli watendaji wetu wote ni wezi kiasi hiki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nijibu swali lake, hizi fedha zitagawiwa na Waheshimiwa Wabunge, watajulishwa ni kiasi gani kimetolewa na kwa ajili gani. Sasa niwaombe mtakapokwenda kule sasa mfuatilie kuhakikisha kwamba, zinatumika kama Wilaya zenyewe zilivyoomba kwa sababu wanapewa kulingana na maombi yao, siyo kutokana na mapenzi yetu. Pili, Wabunge walipokuwa wanachangia hapa wamesisitiza kwamba, mgao huo utangazwe kwenye vyombo vya habari. Kwa hiyo, tutangaza kwenye vyombo vya habari halafu na Wabunge tutawapa *print out* inayoonyesha kila Wilaya imepewa kiasi gani na kwa ajili gani. Kwa hiyo, nafikiri tukisaidiana hizi fedha zitafanya lile ambalo tunataka lifanyike, nalo ni kuendeleza kilimo katika Wilaya. *(Makofi)*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Directorate of Irrigation and Technical Services* .... Sh. 4,121,733,200/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Research Development* ...................... Sh. 3,445,576,700/=

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika kifungu hiki kinaelezea mambo ya *Coffee STABEX.* Nilitaka tu ufafanuzi, ninajua Waziri amekwishaeleza sana lakini kuna taarifa mbalimbali kila tunapokuja hapa. Chini yake wameandika *STABEX Coffee.* Kwa hiyo, ninachotaka kujua hapa ni kwamba, tulivyoelezwa mwanzo ni kwamba, shilingi milioni 38 zilizotolewa na *European Union* zilikuwa kwa ajili ya kuboresha kahawa. Lakini nikisoma hapa matumizi ya hizi fedha na tukaambiwa haiwezekani namna nyingine yoyote kwa kununua kitochi sijui kuangalia watu fedha *cash* tukaambiwa hakuna namna nyingine yoyote ni maelezo ya wenye fedha, tukakubali. Lakini sasa nikiangalia hapa kuna mambo mengine unaona huku utafiti wa chai na pamba na nataka Waziri aelewe kwamba, watu walipata *STABEX* yao na waligawana na tulipouliza tukaambiwa ahaa hii ya chai na mambo yao, hii ya kahawa

imekuja na utaratibu. Sasa kwa nini tena leo hii, hii ya kwetu sisi ya wakulima wa kahawa inaingia hapa utafiti wa chai, utafiti wa pamba, bilioni ngapi sijui? Sasa hilo nilitaka ufafanuzi. *(Makofi)*

La pili, nilikuwa nataka vile vile ile *agreement* ya kwanza ya milioni 38 ambayo ni sawa na bilioni 42 za Kitanzania tupate hiyo *agreement* ili tusiwe tunababaika kwa kuona kila siku utaratibu unabadilika huko. Lakini mengi ni shilingi bilioni 12 zilizokuwa zimepelekwa Lyamungo kwenye *research,* sasa sisi tulikwenda mpaka Lyamungo wakasema fedha zimekuja nyingi sana, lakini imebidi tupeleke benki zizalishe ili tuweze kuendesha kituo. Hivi ndiyo ilikuwa madhumuni hayo au madhumuni ilikuwa kufanya kazi kwa wingi ili iweze kuzalisha ubora huo wa kahawa uweze kuboreshwa?

Mwisho, nilipokuwa nachangia hapa Bungeni nilisema kwamba, kuna madawa ya kahawa ambayo yalikuja na Serikali inafahamu yakaharibu kahawa baada ya miaka kumi sasa ndiyo zinatoa maua, wakulima wanalalamika wanasema hivi kama Serikali iliona hayo madawa ni mabaya, hivi hakuna fidia, nalo ningepata jibu au ningeambiwa kwamba nitajibiwa baadaye. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza sana watu wa Lyamungo, kwa kuweka fedha benki. Ingekuwa hatari sana wangeweka kwenye maboksi kwenye kituo maana jambo lolote lingeweza likatokea. Kama wameweka benki na wanapata ziada ambayo inawaongezea nguvu ya kufanya shughuli zao, nafikiri kumbe wana busara sana. Hizi fedha kwa ajili ya Lyamungo zinatakiwa zitumike katika kipindi cha miaka mitano, hazitumiki mwaka mmoja na kumalizika. Ni programu ya miaka mitano. Programu hii ya miaka mitano ina *components* mbalimbali ambazo Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, anazifahamu ikiwa ni pamoja na kuzalisha miche ambayo inastahimili *CBD* ambayo wana *varieties* tano pale ambazo wanahitaji fedha kuzi- *multiply* na kuzisambaza katika nchi. Kwa hiyo, fedha zinazozungumziwa hapa ni fedha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya angetaka hizi fedha zitumike tu kwenye sehemu ya kahawa, lakini nilipotoa maelezo hapa Bungeni, nilieleza kwamba, hizi fedha kwa kweli zinatolewa kwa Serikali ya Tanzania ili iangalie ni mambo gani ambayo wanaweza wakafanya ikaimarisha uchumi wa Tanzania. Sasa kama tukimega hapo kidogo tukasaidia chai na kidogo tukasaidia *cotton research* inatuongezea uwezo. Maana vinginevyo anachotaka ni kwamba, hizi zingekwenda zote Lyamungo zikakae pale miaka mitano wakati huku kwingine kunahitaji fedha ambazo pengine hazingepatikana. Kwa hiyo, hiyo ndiyo mantiki ya kusaidia *research* ya chai na *research* ya pamba. Vile vile napenda nimjulishe kwamba, mazao haya nayo yalikuwa yanapata fedha za *STABEX* mpaka *very recently,* kwa hiyo, siyo mazao ambayo hayakustahili huu msaada wa *European Union.* Nashukuru. Hii dawa ya kahawa taarifa ni lazima iwe imekuwa *verified* ndiyo tujue nini la kufanya. Mimi hii taarifa ambayo ananipa Mheshimiwa Thomas Ngawaiya naisikia tu Bungeni hapa, naomba aje ofisini tukae anipe ushahidi huo nitume na wasaidizi wangu waende wakaangalie nini kilichotokea, halafu tutaishauri Serikali nini la kufanya.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Kwanza namshukuru Waziri kwa majibu mazuri sana aliyojaribu kuyatoa hapa na hasa hii dawa iliyoharibu kahawa. Lakini nataka niseme moja tu kwamba, je, hiyo miche ambayo tumewapa Lyamungo bilioni 12 wananchi watagawiwa bure?

Sababu ya kuhoji maswali yote haya kahawa yetu ilipata ugonjwa wakati imeanza kuzaa, sasa kipindi hiki nikilalamika Serikalini kwamba tupatiwe hata bilioni moja tu katika hizi ili kahawa zile zipate madawa ili ziweze kukua vizuri kwa maana ya kuboresha kahawa, lakini sikupata. Sasa je, hiyo miche sasa kwa kuwa hela ni kwa ajili ya kahawa itatolewa bure, wakishapanda hiyo miche watatupa bure sisi wakulima? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Labda nianze na lile la kwanza, ambalo aliomba apewe fedha halafu hakupewa, hakuna utaratibu wa Serikali kutoa fedha bure. Mimi ni Mbunge wa Ubungo, hakuna hata siku moja Serikali nimeiomba ikanipa fedha isipokuwa zile kidogo wanazonipa za *jimbo allowance* na mambo kama haya. Sasa hizi nyingine inabidi zipitie katika utaratibu rasmi ndiyo ziweze kupatikana. Hili la kwamba miche itatolewa bure ama itatolewa kwa malipo, kwa kweli inategemea mipango itakavyowekwa na kituo. Kama italipiwa italipiwa kiasi kidogo sana, kwa sababu lengo ni kutumia hizi fedha ku-*subsidize* ile miche ili iweze kupatikana kwa wingi. Tulikuwa tunapenda sana na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya hapa ndiyo mahali pa kupatia maksi kama ungeweza kwenda kuhimiza yale mashamba yakajengwa upya tukawa na mashamba mapya ya kahawa na migomba, ungekuwa umefanya kazi nzuri sana katika miaka yako mitano Bungeni hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Namshukuru Mheshimiwa Waziri na mimi naahidi kufanya hivyo, lakini na nitakapokuja sasa kuomba namna ya kusaidia wale wananchi, naomba nisaidiwe vile vile. Ahsante. *(Kicheko)*

**MHE. BENSON MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika kifungu hicho hicho nilikuwa naomba maelezo sina matatizo na hizo fedha za *STABEX* kwa sababu Waziri wa *European Union* alizungumzia na alitoa majibu na anachokizungumza Waziri ndiyo hasa kilivyo. Lakini ingawa ni jimbo langu ni la Mjini nina mashamba ya Itendi JKT, nina mashamba ya kahawa Iyunga na Itende. Nilikuwa naomba kuuliza miche hii inayozalishwa Lyamungo itaanza lini kusambazwa kwa wananchi kwa sababu tayari wamepata hiyo picha? Lakini la pili hii mibuni ambayo tayari tunayo wananchi wanauliza tung’oe au tufanye nini au watatumia utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba, tunapanda hiyo mipya na ile ya zamani tunaifanya nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali zuri sana. Mimi kwanza kule kwake kazi ni ndogo zaidi kuliko ilivyo huku kwingine ambako tunashughulika na wakulima wadogo wadogo, kwa kuwa yeye ana mashamba makubwa yale mashamba yangeweza yakaenda yakachukua miche halafu wakafundishwa jinsi ya kukata vile vikonyo na kuviotesha, kwa hiyo, wakazalisha miche yao wenyewe kwa wingi, jambo ambalo litawapunguzia gharama na vile vile kuwapa miche kwa wingi zaidi na kwa haraka zaidi. Naomba utakaporudi uwasiliane na watu wa

Uyole na wako hapa kwa hiyo, nitazungumza nao ili muwasiliane muangalie ni vipi mtakavyofanya suala hili. Sasa juu ya ile kahawa ambayo tayari ipo wana utaratibu ambao wameweka unafyeka matawi ya upande huu na upande huu halafu unapata mstari katikati. Hii kahawa ikiota unaondoa hii nyingine unabakia na kahawa mpya na unakuwa unaendelea kupata mavuno kwa kipindi hicho kwa miaka miwili, miwili na nusu au mitatu wakati kahawa yako inaota. Lakini lazima ile miche ya zamani *eventually* iondoke ubaki na hii mipya. Nashukuru. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako likiwa limekaa kama Kamati ya Matumizi, limepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka 2004/2005, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa ya Kamati sasa ipokelewa na makisio haya yapitishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona kazi tuliyofanya ni nzuri, itabidi tuahirishe kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01. 28 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano tarehe 30 Juni, 2004 saa tatu asubuhi)*